

Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Sita - Tarehe 18 Juni, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 50

Upungufu wa Watumishi - Hospitali ya Wilaya ya Mbulu

MHE. PHILIP S. MARMO aliuliza:-

Kwa kuwa siku zilizopita Wizara imekiri upungufu mkubwa wa watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu katika fani zote kama Madaktari, Wauguzi, Wataalam wa *X-ray* na Famasia na mfano mmoja ukiwa ni kwamba mashine mpya za chumba cha *X-ray* hazitumiki kwa sababu ya ukosefu wa wataalam.

Je, ni lini Serikali itawaajiri wataalam niliowataja ili kutatua tatizo hilo sugu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tarehe 18 Julai, 2002 wakati nikijibu swali Na. 873 la Mheshimiwa Mbunge, nilikiri upungufu wa wataalam wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu.

Naomba kumpongeza kwanza Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu, kwa juhudzi zake kubwa sana anazozichukua katika kutatua matatizo yaliyoko katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ikiwa ni pamoja na upungufu wa watumishi. Halmashauri

za Wilaya nyingi hapa nchini bado zina upungufu wa wataalam katika fani mbalimbali. Ofisi ya Rais, pamoja na Idara Kuu ya Utumishi inajitahidi sana kutoa vibali vya ajira, lakini waombaji wa kazi hizo mara nyingi wamekuwa ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ni moja ya Hospitali za Wilaya ambazo zina upungufu wa Madaktari, Wauguzi na wataalam wengine. Hata hivyo hospitali hii ina Madaktari Wasaidizi saba kati yao watatu wamepelekwa masomoni na wanatarajiwu kurudi mwaka kesho 2004. Aidha, hospitali hii inahitaji Wakunga Wasaidizi 35 lakini hadi sasa waliopo ni 18 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtaalam wa kutumia *X-ray*, ni kweli kuwa Hospitali ya Wilaya ya Mbulu inayo *X-ray* mpya lakini hadi sasa hivi haitumiki kwa kukosa mtaalam. Mwaka 2003, Halmashauri hii ilipatiwa kibali cha kuajiri mtaalam, lakini hakuna aliyeomba.

Baada ya utaratibu huu kushindikana, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikutana na wahusika katika Wizara ya Afya ili kuwaomba wasaidie katika kumpata mtaalam huyo. Hadi sasa juhudhi hizo bado zinaendelea na tunayo matumaini makubwa kuwa mtaalam atapatikana ili huduma inayosubiriwa na wananchi kwa hamu iweze kutolewa.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, amelijibu swali langu vizuri sana lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huwa nikiwa Wilayani angalau mara moja kwa wiki natembelea hospitali hii kupitia kuangalia hali ya wagonjwa, lakini pia kuangalia hali ya hospitali na hali halisi ni kwamba hospitali hii inajaa sana kwa sababu inakuwa kama Hospitali ya Rufaa kwa Vituo vya Afya sita, licha ya hiyo kuna vituo vya nje ya Wilaya, Zahanati zaidi ya 20 na Zahanati tano katika hizo ni za nje ya Wilaya, kwa ajili hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hii kwa ujumla inaonaje namna gani tutatue tatizo hili, kuhamisha baadhi ya watumishi ambapo kuna vituo na zahanati hizi au kutafuta mkakati mpya kabisa ili kutatua tatizo hili la pekee kwa Hospitali ya Wilaya kuwa kama Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya uzuri na utendaji kwa wafanyakazi wake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ni kweli kabisa kwamba hospitali hii inatumika kama *Referral Hospital* kwa kiasi fulani na Halmashauri ya Kiteto ambapo vile vile kuna matatizo makubwa siyo ya wataalam tu lakini hata Hospitali yenyeewe ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoweza kusema tu ni kwamba pengine kisiasa haitakuwa jambo jema kujaribu kuwahamisha wataalam tulionao wachache kutoka katika eneo moja kwa kuzingatia hali halisi kwamba kila mahali demand hiyo ipo. Mimi nadhani juhudhi tunazozifanya za kujaribu kupata wataalam ili kuweza kukidhi haja ya kila hospitali pengine ndiyo jambo jema ambalo tunaweza tukasema litatusaidia sana.

MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana swalii na amekiri mwenyewe kwamba pamoja na Serikali kutoa vibali kwa Halmashauri ya Mbulu iweze kuajiri Madaktari imekuwa bado ni vigumu.

Je, Serikali haioni kwamba ni kutokana na mishahara midogo ambayo wanapewa Madaktari Wilayani ndiyo sababu inayofanya wasiende huko katika Wilaya kwa sababu Madaktari wengi wanaona bora wafanye kazi katika Miji mikubwa kama Dar es Salaam ama Miji ya Mikoa ili waweze kufungua na Zahanati zao au wakafanye katika ajira za ziada katika hospitali nyingine, katika Wilaya kitu kama hicho hakiwezekani ndiyo maana inakuwa vigumu.

Je, Serikali itakuwa tayari kuangalia uwezekano wa kuongeza mishahara ya Madaktari ili waweze kukubali kufanya kazi hata Wilayani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ziko sababu nyingi ambazo tunaweza tukazitoa zinazopelekeea kuwa na uhaba na ukosefu wa wataalam hawa. Moja ya jambo hilo katika baadhi ya maeneo inawezekana ni sababu anayoitoa Mheshimiwa Ismail Iwvatta, kwamba wanavutiwa zaidi na maeneo ya Miji kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka tu kwa kweli kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba sababu kubwa kabisa ni uchache wa wataalam waliopo hivi sasa hapa nchini. Hilo ndilo jambo kubwa na ndiyo tatizo kubwa, sababu nyingine kama zipo ni za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niongeze vile vile kwamba kwa kuwa swalii lake kusema kweli ni la kisera, siwezi nikazungumzia suala la mishahara kuongezwa kwa Madaktari wangu, Wizara zinazohusika nina hakika zinajua hilo na pengine wanafanya juhudii ili kujaribu kuona ni nini kinaweza kufanyika katika eneo hilo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee majibu ya ziada kwenye majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kuwa ni kweli mishahara ni moja ya mambo ambayo yanavutia watumishi wa Serikali kufanya kazi au kuwepo kazini. Lakini si mishahara peke yake ambayo kwa kweli ndiyo inayowafanya wabaki Serikalini. Naomba tuzingatie vile vile suala la mazingira mazuri ya watumishi wa Serikali kufanya kazi wakiwemo Madakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa vile vile kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua kazi nzuri wanayoifanya Madaktari na kwa hiyo pamoja na kuwaongeza watumishi wa Serikali mishahara kila mwaka wakati Serikali inapokuwa na nafasi, Madaktari wamekuwa wakipewa mshahara zaidi kuliko wengine na

bado Serikali itajitahidi kuboresha mazingira yao pamoja na kuwaongezea mishahara kila inapowezekana. (*Makofii*)

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba tatizo kubwa ni uchache wa Madaktari na Wauguzi katika hospitali zetu kama ilivyo katika Hospitali ya Mbulu, Korogwe na hospitali nyingine nyingi, sekta hii ya afya ni muhimu na katika Bajeti ya safari hii huduma za jamii zimeongezwa asilimia ya fedha.

Je, Serikali katika kutatua tatizo hilo haioni sasa kwa sababu ya umuhimu wa kupata Madaktari, kufanya programu maalum ya kuongeza wataalam hawa katika nchi hii ili kujaza mapengo ambayo ni mapungufu katika Wilaya na Zahanati zote katika nchi hii kama inavyofanya kwenye Sekta ya Elimu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo analizungumza Mheshimiwa Joel Bendera, ndilo ambalo limekwishafanyika au linaendelea kufanyika kila mwaka. Hivi sasa idadi ya Madaktari wanaoingia Muhibili imeongezeka, tuna vyuo vingine vya Bugando na *KCMC* na vile vile katika vyuo ambavyo viko chini ya Wizara ya Afya wale Matabibu au tuseme *AMOs* na *Clinical Officers* idadi yao pia imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Lengo la hatua hizi zote ni kuongeza idadi ya wataalam wanaoweza kutoa huduma katika Wilaya zetu.

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongeza kwenye majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa taaluma hizo muhimu hasa Madaktari ya kwamba sasa bado uwiano wa wagonjwa na Daktari ni Daktari mmoja kwa wagonjwa 24,000, Serikali imeamua kwamba itawasomesha Madaktari na kuwalipia bila kujali kama ni Chuo cha Umma ama kama ni Chuo cha Serikali. Kwa hiyo, tumetenga fedha katika suala hili. Ahsante. (*Makofii*)

Na. 51

Ushuru wa Maegesho ya Magari Jijini Dar es Salaam

MHE. MARGARETH J. BWANA aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Dar es Salaam wamekuwa wakitozwa shilingi 300/= kama ushuru wa maegesho ya magari kwa kila saa moja:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba hali hiyo imekuwa kero kwa wakazi wa Jiji na kuwaongeza mzigo wa kodi usio wa lazima?

(b) Kama kuna ulazima wa ushuru huo kutolewa; je, tangu utaratibu huo uanze, ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa; na Serikali imefaidika vipi na mapato hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru unaotozwa na Jiji la Dar es Salaam kwa kutoa huduma ya maegesho ya magari ulianzishwa kutokana na hali halisi ya mahitaji ya huduma hiyo na upo sehemu nyingi za Miji mikubwa katika nchi mbalimbali hapa duniani.

Uanzishaji na utekelezaji wake unafanywa kwa juhudi za pamoja kati ya Halmashauri ya Jiji na Wadau. Huduma hiyo hutolewa na Kampuni ya *Tanzania Parking System* kama wakala wa ukusanyaji ushuru huo. Huduma hii hutolewa kwa wananchi ambao hutumia magari yao kwenye maeneo ya katikati ya Jiji na Kariakoo na kwamba ushuru unaotozwa sio kero na wala hauwaongezei mzigo wa kodi wakazi wa Jiji hilo.

Tathmini iliyofanywa kuhusu huduma ya maegesho ya magari Jijini Dar es Salaam, imebaini kuwa huduma hiyo ni nzuri kwa wakazi wa Jiji hilo na kwamba imeleta mafanikio makubwa yafuatayo:-

- (i) Kupunguza msongamano wa magari;
- (ii) Kupungua kwa uchafuzi wa mazingira kutokana na kupungua kwa mizunguko ya magari kutafuta maegesho;
- (iii) Kupungua kwa ajali za barabarani;
- (iv) Kupungua kwa udokozi wa vifaa vyta ya magari na hata wizi wa magari;
- (v) Kuongezeka ajira kwa wakazi wa Jiji; na
- (vi) Kuongezeka mapato ya Halmashauri ya Jiji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umeanza mwaka 1997. Halmashauri ya Jiji kwa kutumia Sheria Ndogo ya Maegesho ya Magari hadi kufikia Aprili, 2003 imekusanya jumla ya shilingi bilioni 4.7 na imepokea fedha taslimu asilimia 25% yenye jumla ya makusanyo ya ushuru ambao ni sawa na shilingi milioni 763.0 na shilingi milioni 415.6 bado hazijawasilishwa na Wakala wa ukusanyaji ushuru huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa Halmashauri zetu hasa Miji mikubwa kama Mwanza na Manispaa kubwa kama Arusha kuiga mfano wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wa kubuni njia hii katika kuboresha mazingira ya Miji yetu.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali yafuatayo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *Tanzania Parking System* inayoendesha huduma hiyo imekuwa haihusiki kabisa na uharibifu wowote unaojitokeza katika gari lililokatiwa ushuru huo na wala haiboreshi maegesho hayo pamoja na fedha zinazopatikana; je, mwananchi mmoja mmoja ambaye anahusika na uegeshaji wa gari katika hiyo *Parking System* anafaidika vipi na huduma hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa nini Serikali isipige marufuku utaratibu huu ikizingatiwa kwamba hakuna jitihada zozote zinazofanywa za kuboresha huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua kama utaratibu huu umetunufaisha huna budi kujua kidogo *background* ya tatizo hili.

Mimi nina hakika Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi, hali ya uegeshaji wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kabla utaratibu huu haujaanza ilikuwa kwa kweli ni kero, ulikuwa ni mbaya sana kiasi kwamba Serikali ililazimika kuwashirikisha wadau mbalimbali Jijini Dar es Salaam wakakaa, wakazungumza na kwa pamoja wakafikia utaratibu huu. Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba, tunaamini kabisa utaratibu huu umeleta manufaa makubwa sana, sasa hivi hali ya uegeshaji wa magari Jijini Dar es Salaam ina ahueni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwamba Serikali ipige marufuku utaratibu huu. Kama nilivyosema, bado hatujaona ya kwamba kuna sababu za msingi za kufuta utaratibu huu kwanza kwa sababu Miji mikubwa ni lazima iwe na utaratibu huo. Lakini napenda kumkumbusha tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata kabla hatujaanza utaratibu wa kutumia Kampuni hii Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na utaratibu huo, lakini tulikuwa tunatumia *blots* na baadaye zilipokuja kuharibika ndiyo maana tukatafuta mbinu nytingine ya kuendeleza utaratibu huo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Margareth Bwana, akubali tuendelee na utaratibu huo kwa sasa. (*Makofi*)

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tume ya Jiji ilipopatana na *TPS* katika mikataba yao ya kuwaruhusu kutengeneza zile *Parking System* moja ya sharti ambalo lilikuwepo ni *TPS* kuendeleza maeneo mengine zaidi ya *parking*; na kwa kuwa mpaka sasa hivi wanashindwa kutengeneza maeneo mengine ya *parking* na wanawatoza watu ambao wana-park sehemu ambazo zisizo za *parking*; na pia wanashindwa kulipa ile *percentage* kwa Manispaa ya Jiji kama inavyopaswa; je, Serikali itachukua utaratibu gani au hatua gani ili kutafuta chombo kingine ambacho kitatoa huduma hii kwa ufanisi zaidi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, masharti yaliyomo katika mkataba kati ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Kampuni hii ya *TPS* yako bayana kabisa, yako

majukumu ambayo ni ya Jiji na pia yako majukumu ambayo ni ya kampuni. Kampuni hii ninaweza nikasema imejitahidi kwa kiasi chake kwa kuzingatia hali halisi ya Jiji la Dar es Salaam ilivyo kuongeza maeneo ya kuegesha magari na mimi nina hakika kabisa hata Mheshimiwa Sophia Simba, hilo analijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba hawalipi ushuru wowote unaotakiwa. Nilikiri katika jibu la msingi hapa kwamba ni kweli bado tunawadai zaidi ya shilingi milioni 400 lakini kwa kiasi fulani hali hiyo imesababishwa vile vile na utendaji ambao pengine haulizishi katika kufuatilia malipo haya kwa sababu unapoingia mkataba kama huo hapana budi kufanya kazi hiyo kwa pamoja ili muweze kupata mapato yenu kwa ujumla.

Hata hivyo, nilitaka kumwarifu Mheshimiwa Sophia Simba, kwamba, mkataba wa kampuni hiyo umemalizika tarehe 17 Aprili, 2003 kulingana na masharti yalivyokuwa na tayari tumekwishatoa tangazo la zabuni ili kujaribu kuwapata wawekezaji wengine katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea naye kwa sababu bado hatujafikia kikomo na tutakapofikia basi tutasitisha, lakini na ye ye yuko huru vile vile kuomba kuingia katika zabuni hiyo na kama atakuwa na sifa bado anaweza akapata.

Na. 52

Upanuzi wa Jengo la Maktaba Kuu ya Taifa

MHE. JOEL N. BENDERA (k.n.y. MHE. IBRAHIMU W. MARWA) aliuliza:-

Kwa kuwa mchoro halisi wa Jengo la Maktaba Kuu ya Taifa (*The Central Library*) uliochorwa na *Architect*, Almeida mwaka 1966, ambaye ni mwanachama wa *The Royal Institute of British Architects (RIBA)*, Taasisi ambayo ni maarufu kati ya Sekta ya Usanifu Majengo; na kwa kuwa jengo hilo kimchoro lilikusudiwa lisizidi ghorofa mbili baada ya *extension*.

Lakini jengo hilo limeongezwa hadi kufikia ghorofa tatu kinyume na ushauri wa kitaalam uliotolewa na vile vile ushauri huo haukupata maelekezo toka kwa msanifu wa jengo hilo (Pameila 1966) hivyo kusababisha kazi hiyo ifanyike katika mazingira ya kutatanisha:-

(a) Je, upanuzi (*extension*) wa jengo hilo hadi kufikia ghorofa tatu ulifanywa kwa kufuata taratibu zipi za zabuni, ushauri wa kitaalam toka kwa *architect* na kadhalika?

(b) Kwa kuwa suala hilo linahusu usalama wa jengo kwa watumiaji na watoaji huduma kwenye Taasisi hiyo; je, ni tahadhari zipi zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba hakuna madhara yanayoweza kutokea kutokana na uamuvi wa ujenzi usiofuata maelekezo ya msanifu wa majengo (Ndugu Pereila)?

(c) Je, Taifa limenufaika vipi na uamuzi huo uliopelekea hali niliyoelezea kwenye sehemu (a) na (b) ya swali hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba nitoe kwanza maelezo ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Maktaba Kuu ya Taifa ambalo lipo eneo la Upanga barabara ya Bibi Titi Mohomed, katika kiwanja Na. 1/1 lilijengwa kwa msaada wa Serikali ya Uingereza mnamo mwaka 1967. Mtaalam wa michoro ya jengo hilo ni Ndugu Anthony V. Almeida.

Mwaka 1968 Serikali ya Uingereza ilijitoa katika kumalizia ujenzi wa ghorofa ya pili kutokana na sababu za kisiasa na hasa kutokana na suala la iliyokuwa *Southern Rhodesia* ambayo ni Zimbabwe ya leo. Kutokana na kutokamilika kwa ujenzi kama ilivyokusudiwa tatizo la kuvuja kwa paa lilianza kujitokeza mwanzoni mwa miaka ya 1980. Licha ya jengo hilo kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara na Serikali, tatizo la kuvuja kwa paa liliendelea kuwa kero kwa wafanyakazi na watumiaji wa maktaba kwa ujumla

Katika jitihada za kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ilishauriwa kuongeza ghorofa nyingine juu. Bodi ya Huduma za Maktaba ilimtafuta mwekezaji kwa kugharamia upanuzi wa jengo kwenda juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1993 Bodi ya Huduma za Maktaba iliiteua Kampuni ya *M/S Mlundwa Studios* kwa ajili ya utaalam wa michoro (*architecture*) na ushauri na kuiagiza kampuni hiyo kufanya yafuatayo:-

- (1) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Bodi juu ya ujenzi wa ghorofa mbili;
- (2) Kutayarisha michoro; na
- (3) Kusimamia ujenzi.

Michoro ya kihandisi ilipitishwa na Halmashauri ya Jiji baada ya kuandaliwa na *Linda Concrete Designs* kutokana na michoro ya awali ya *Zevett International* ambao ni Wahandisi Washauri (*Consulting Engineers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hao *Linda Concrete Designs* waliandaa michoro ya kihandishi iliyotumika katika ujenzi.

Tarehe 23 Mei, 1994 zabuni ya kumpata mwekezaji ilitangazwa na tarehe 15 Agosti, 1994 Mwekezaji ajulikanaye kwa jina la *M/S Tidy Home Limited* alishinda zabuni na kuwekeana mkataba na Bodi ya Huduma za Maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwishoni mwa mwaka 1995, ujenzi ulianza baada ya kupata kibali cha ujenzi Na. 22959 cha tarehe 27 Juni, 1995 kilichotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na tarehe 1 Oktoba, 1998 jengo lilikabidhiwa kwa Bodi ya Huduma za Maktaba na kuanza kutumika rasmi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Septemba, 2000 Kamishna wa Ardhi alitoa kibali kwa mwekezaji kuruhusu jengo lipangishwe kama ilivyoonyeshwa katika makubaliano ya upangishaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zote muhimu zilichulikuwa kwa kuwashirikisha wataalam pamoja na mamlaka husika zilizotajwa hapo juu kwa lengo la kuepusha madhara yanayoweza kutokea hapo baadaye.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uamuzi wa kupanua jengo la Maktaba Kuu, Taifa letu limenufaika kama ifuatavyo:-

- (i) Tatizo la awali la kuvuja kwa jengo sasa limekwisha;
- (ii) Kutokana na mradi huu wa upanuzi Bodi imepata nafasi zaidi kwa ajili ya shughuli zake; na
- (iii) Mradi huu hatimaye utaiwezesha Bodi ya Huduma za Maktaba kupata fedha kutokana na kukodisha sehemu ya jengo, fedha ambayo itatumika kwa ajili ya maendeleo ya maktaba nchini.

Na. 53

Walimu Bora

MHE. LEONARD N. DEREFA (k.n.y. MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imeamua kuhakikisha kuwa watoto wote walio chini ya umri wa kwenda shule wanakwenda shule na kufuta michango yote ambayo ilikuwa ikitozwa huko nyuma; na kwa kuwa wanafunzi hao wanatakiwa kuwa na walimu bora ili watoto hao waweze kupata elimu bora:-

Je, ni lini Serikali hii itakuwa na walimu bora wa kuweza kuinua elimu kwa kiwango kinachotakiwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 mwalimu bora ni yule mwenye sifa za kitaaluma na kitaalam. Kiwango cha chini cha mwalimu wa cheti kwa sasa ni yule aliyemaliza kidato cha nne na kufaulu katika masomo atakayotakiwa kufundisha baada ya kuhitimu mafunzo ya ualimu.

Serikali imeacha kabisa utaratibu uliokuwepo wa wahitimu wa elimu ya msingi kusomea ualimu wa shule za msingi. Katika utekelezaji wa MMEM mwaka 2002 hadi 2006 watafundishwa na kuajiriwa walimu 45,796. Kwa hiyo, tulipoanza utekelezaji wa MMEM ndipo tulipoanza juhudhi maalum ya kuwa na walimu bora kwa kuweza kuinua elimu kwa kiwango kinachotakiwa.

Aidha, mafunzo ya walimu kazini yanaendeshwa kwa lengo la kuinua ubora wa walimu waliopo wa daraja la *IIIB* na *IIIC* ambao hawakubahatika kupata elimu kamilifu ya Sekondari. Mafunzo hayo yanawanoa katika ujuzi wa masomo wanayofundisha.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga umekuwa wa mwisho katika mitihani ya Taifa na hii inasababishwa na upungufu wa walimu; je, Serikali itatupa lini Mkoa wa Shinyanga walimu wa kutosha ili kukabiliana na tatizo hili la kuwa wa mwisho kila mwaka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Naibu Spika, katika upungufu wa hali halisi katika Sekta ya Elimu, upungufu wa walimu wa kutosha ni moja ya tatizo ambalo tunakiri tunalo. Lakini siamini kama upungufu wa walimu ndiyo sababu pekee ya kuwa wa mwisho katika Mkao wa Shinyanga kama alivyosema mwenyewe Mheshimiwa Mbunge na sina hakika ya kwamba Mkao ule unakuwa wa mwisho katika mitihani ya Taifa kila mwaka. Bila shaka ziko baadhi ya sababu nyingine na si upungufu huu ambao tunao kwa Taifa zima. (*Makofit*)

Na. 54

Majina ya Ukoo

MHE. LUCAS L. SELELII aliuliza:-

Kwa kuwa majina ya ukoo kama Selelii, Milambo, Lumambo na kadhalika ni mazuri na yenye maana katika utamaduni wa Kitanzania; na kwa kuwa imetokea kwamba siku hizi watu wanajiita kwa majina yote ya kigeni (Kizungu au Kiarabu) yaani jina lake, la Baba na la Ukoo:-

Je, Serikali haiwezi kuweka ulazima wa jina la ukoo liwe na asili ya Kitanzania?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kuwa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba majina ya koo ni mazuri na yenye maana zaidi katika utamaduni wa Kitanzania. Aidha, nakubaliana na ushauri wake kwa Watanzania kijiita kwa majina ya koo zao kuliko kwa majina ya kigeni ambayo mara nyingi maana zake ni ngeni kama yalivyo majina yenyewe.

Pamoja na hayo, ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania inazo jamii za makabila zaidi ya 120 na kila moja ya jamii hizo ina mila na desturi zake ambazo kimsingi huitofautisha na jamii nyingine. Hata katika lugha ukiondoa Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa ya jamii hizi hutofautiana.

Kutokana na tofauti hizo, majina mazuri kwa tafsiri na mantiki ya jamii moja yaweza yasiwe na maana, dhana na maudhui yale yale kwa jamii nyingine. Yapo majina mengine ya kiukoo ambayo pamoja na dhana nzuri yanayobeba katika koo na jamii husika yatajwapo watu wa asili ya jamii tofauti hushtuka na kuhisi utusi na maudhui yasiyopendeza. Wengine wenge majina kama hayo huona ni busara kuacha kuyatumia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haijapata kuwa Kisiwa kilichojitenga katika mkondo wa maendeleo ya dunia. Kwa karne nyingi, pamekuwepo maingiliano ya watu hapa nchini yaliyotokana na ujio wa jamii mbalimbali za kigeni. Maingiliano hayo yalijikita katika tamaduni za Watanzania na hata kuathiri nyanja mbalimbali za maisha yao ikiwa ni pamoja na taratibu za majina na utoaji wake. Hatuna budi tukumbuke mchangano wa dini, elimu na mabadiliko ya kiuchumi, sayansi na teknolojia katika mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya nchi yetu iko wazi katika suala zima la haki za binadamu. Katiba inatamka kwa mfano kwamba kila raia anayo haki ya kuabudu dini anayotaka, kujielimisha kadri ya uwezo wake na kwenda popote anapotaka ili mradi asivunje sheria za nchi. Kwa bahati nzuri, utoaji majina kwa watoto hauhusishwi na uvunjaji wa sheria yoyote maana hakuna sheria inayovunjwa katika taratibu zilizopo nchini za utoaji wa majina. Majina mengi ya kiukoo hutolewa na wazazi hasa mababu kulingana na aina ya mazingira yanayojitekeza zaidi wakati wa kuzaliwa kwa watoto husika. Majina kama vile Mwanvita, Shida, Tabu na kadhalika yatosha kuwa mifano michache ya majina yanayotolewa yakihuhsishwa na matukio ya hali halisi ya mambo yanayokuwepo wakati huo. Lakini pia majina mengine hutolewa kuonyesha hisia za mapenzi, utashi na matarajio ya wazazi kwa maisha ya watoto wao. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wanayo mifano lukiki kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo, Serikali haioni busara kuingilia taratibu na haki zilizopo za Watanzania za kuwapa watoto wao majina kwa kuweka kanuni au ulazima wowote wa kisheria wa majina ya koo kuwa na asili yoyote ile.

Hata hivyo, Wizara ya Elimu na Utamaduni, italifuatilia kwa makini suala hili kwa shabaha ya kuweka kumbukumbu majina yenye asili ya utamaduni wa Mtanzania na kutambua maana, maudhui na mantiki yake kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa asili majina ya Kiafrika yalibadilishwa na Wazungu na Waarabu hasa wamisionari wa Kiaarabu walioleta dini ya Kiislam na Wazungu walioleta dini ya Kikristo ndipo ikasemekana majina yetu ni ya kishenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu swalı langu la msingi amesema kwamba majina mengine yanatisha kwa kusikia katika koo nyingine, lakini hakutoa mfano wowote. Mimi nakaa na jirani yangu anaitwa Simba, sijatishika na nakaa naye sina matatizo. (*Kicheko*)

Sasa haoni kwamba majina hayo pamoja na kwamba yanatisha lakini kwa sababu yana asili ya Kiafrika na Kitanzania ni muhimu koo zetu na jamii zetu zikajulikana kama sisi ni Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili, kwa kuwa sisi Waafrika lazima tujivunie weusi wetu na sisi Watanzania lazima tujitambulishe. Unaposikia jina la Maganga au Masanja, anajulikana anatokea wapi, ukiita jina la Ole-Selelii, unajulikana ni wa Kabilia lipi, ukiita Akukweti, inajulikana ni wa wapi. Haoni kwamba majina haya ni mazuri kwa ajili ya kutambulisha sehemu tunazotoka bila kuficha utamaduni wetu? (*Makofsi/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba baadhi ya majina katika jamii moja yanaweza yakawa yanatisha katika jamii nyingine au kama nilivyosema kuhisi utusi. Sikutaka kutoa mifano, lakini nafikiri Mheshimiwa Mbunge anataka nitoe mfano, nitatoa mfano mmoja au miwili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Abdisalaam Issa Khatibu, katika Jimbo lake la Uchaguzi ukitaja kwa jina mnyama ndovu watahisi utusi.

MBUNGE FULANI: Tembo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Naambiwa ndovu jina lingine tembo na kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Kigoma kwa mfano, ninakotoka mimi jina la pili la Mheshimiwa Mbunge wa Makete...

MBUNGE FULANI: Nani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mnajua jina lake, kwa kuwa natoka huko naona vigumu kilitaja. Ni mifano miwili nilitaka niitumie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba ni vizuri tukatumia majina ili kujitambulisha kama Waafrika, napenda niamini zaidi kwamba kujitambulisha maeneo tunakotoka ni kitu kimoja, lakini nadhani kujitambulisha kwa maana ya utaifa na uzalendo wetu ni jambo la muhimu zaidi.

Na. 55

Ujambazi wa Kutumia Silaha

MHE. HAROUB SAID MASOUD aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni mionganini mwa nchi za Afrika zilizokumbwa na wimbi kubwa la ujambazi wa kutumia silaha na hivyo maisha ya watu yanapotea kutokana na hali hiyo:-

- (a) Je, kuanzia Januari 2002 hadi Machi, 2003 ni matukio mangapi ya aina hiyo yametokea hapa nchini?
- (b) Je, ni mali ya thamani gani iliyoporwa kwenye maeneo hayo na idadi ya watu waliouawa?
- (c) Je, ni Mikoa gani mitatu inayoongoza hapa nchini katika matukio hayo na ni Mikoa gani mitatu isiyo na matukio mengi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu inakabiliwa na wimbi la ujambazi wa kutumia silaha. Chimbuko la tatizo hili ni kutokana zaidi na baadhi ya majirani zetu kuwa katika hali ya vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kutokana na hali hiyo, silaha nyingi zinaingizwa nchini na wakimbizi ambazo huziuza kwa Watanzania wasio wema na kisha kuzitumia kwa uhalifu na wakati mwengine wao wenyewe wakimbizi hujiingiza katika ujambazi kwa kutumia silaha walizozificha.

Kwa kipindi cha Januari 2002 hadi Machi 2003 jumla ya matukio 1,494 ya unyang'anyi wa kutumia silaha yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini kote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika wimbi hili la unyang'anyi wa kutumia silaha mali zenyne thamani ya shilingi 2,402,763,799/= iliporwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini na jumla ya watu 311 waliuawa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma na Kagera imeongoza katika matukio hayo ya unyang'anyi wa kutumia silaha katika kipindi cha Januari 2002 hadi Machi 2003. Mkoa wa Dar es Salaam kulikuwa na matukio 315 na watu 96 kuliuawa. Mkoa wa Kigoma kulikuwa na matukio 156 watu 33 waliuawa na Mkoa wa Kagera ulikuwa na jumla ya matukio 149 na watu 33 waliuawa.

Vile vile katika kipindi hicho Mikoa mitatu iliyoongoza kwa utulivu hivyo kuwa na matukio machache ya unyang'anyi wa kutumia silaha ni Mtwara matukio matatu, Mikoa ya Tanzania Zanzibar matukio 11 na Mkoa wa Tanga matukio 16.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na jibu zuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kabla ya kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wameianzisha hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la kwanza, kwa kuwa tukio lilitokea hivi karibuni Jijini Dar es Salaam na kusababisha vifo vya Askari watatu ni ushahidi tosha kuwa asilimia kubwa ya majambazi yanayotikisa nchi yetu ni kutoka nchi nyingine, je, Serikali haioni kuwa kutokuwepo kwa vitambulisho vya Taifa inachangia kwa kiasi kikubwa majambazi kuzagaa hovyo bila kutambuliwa na Askari?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kutokana na kuuliwa ovyo kwa Askari na hawa majambazi, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Askari hawa hasa wa doria kukatiwa Bima ya maisha?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi, napokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi hivi sasa katika kupambana na majambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vitambulisho ni kweli katika kupambana na matatizo haya vitambulisho vitasaidia, hatukatai na hivi sasa Serikali inaendelea zoezi la kuandaa vitambulisho. Lakini jambo kubwa kabisa ni Watanzania wote kujizatiti kushirikiana na vyombo vya Dola katika kukabiliana na majambazi wakati zoezi la vitambulisho linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Askari kuandaliwa Bima za maisha, ni wazo zuri tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA aliuliza:-

Kwa kuwa Polisi, Mbeya Mjini haina pikipiki kubwa ya kuongoza magari ya misafara ya viongozi wanapokuwa kwenye ziara zao Mbeya na kwa kuwa kutokana na sababu hiyo hulazimika kuazima pikipiki kutoka Iringa umbali wa km. 341 wakati wa ziara za viongozi wa Kitaifa; je, ni lini Serikali itaipatia Polisi Mbeya chombo hicho muhimu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpresa, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si sahihi kwamba Polisi Mbeya Mjini hawana pikipiki ya kuongoza misafara ya viongozi wa ngazi za Kitaifa na kwamba wanapokuwa na misafara ya viongozi pikipiki huazimwa kutoka Mkao wa Iringa. Ukweli ni kwamba Polisi Mbeya Mjini wanayo pikipiki Na. *STH 7183*, *Honda* ambayo pamoja na kazi nyingine za doria katika barabara kuu hutumika kuongoza misafara ya viongozi wa Kitaifa. Iliwahi kutokea mara moja wakati Rais alipotembelea Mkao wa Mbeya mwezi Juni, 2002 pikipiki hiyo ilikuwa kwenye karakana ya Polisi Dar es Salaam kwa matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, ilibidi pikipiki nyingine iletwe kutoka Iringa kwa kazi za kuongoza msafara huo wa Mheshimiwa Rais. Pikipiki hiyo ya Mbeya sasa tayari imekwisharudishwa Mbeya na inafanya kazi.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi ni hatari sana kwa usalama wa Askari pamoja na wananchi hasa unapokuwa na chombo cha usafiri ambacho ni kibovu kama ilivyo kwa Maaskari wangu wa Mbeya mjini ambapo hawana gari la kufanya *patrol*, je, Serikali kupitia Bajeti hii itarekebisha tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vyaa usafiri kama magari au pikipiki ni vyombo ambavyo mara kwa mara vinaweza kuharibika, lakini vinatengenezwa na vinarudi tena barabarani hakuna *guarantee* kwamba ukishanunua gari au pikipiki haitaharibika. Kwa hiyo, ndio kilichotokea hata katika ile pikipiki ya Mbeya iliharibika ikategenezwa na sasa imerudi barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza magari ya doria na pikipiki nyingine, kwa sababu Bajeti yetu itakuja wiki chache zijazo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge muitazame kwa jicho la huruma ili mtupatia uwezo wa kuongeza vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi.

TPDC Kufanywa Wakala

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) limepunguziwa majukumu yake na kuanza utekelezaji kabla ya sheria ya kuanzishwa kwa Shirika hilo kufanyiwa marekebisho na kwa kuwa kutokana na mabadiliko hayo sasa *TPDC* inapata fedha za kuendesha kazi zake kutoka katika Bajeti finyu ya Wizara ya Nishati na Madini na hivyo kupunguza kasi ya jukumu lake la utafutaji wa mafuta:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kufanya *TPDC* ifanye kazi zake kama Wakala (*Agency*) kwa kujitegemea zaidi kuliko kuwa kama Idara ya Wizara ya Nishati na Madini?

(b) Kwa kuwa ufinyu wa Bajeti umepunguza kasi ya jukumu la *TPDC* kutangaza shughuli za ufuatiliaji wa mafuta (*Exploration and Promotion*), je, kwa kipindi tangu mwaka 1995 - 2003, *TPDC* imeshiriki katika mikutano mingapi ya utangazaji (*promotion*) kila mwaka na kuingia mikataba mingapi ya utafutaji wa mafuta kwa kampuni moja moja?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sasa Serikali haina mpango wa kufanya *TPDC* iwe Wakala wa Kujitegemea (*Agency*) na pia *TPDC* haifanyi kazi kama Idara ya Nishati na Wizara. Muundo wa Shirika la *TPDC* utaangaliwa tena kulingana na matokeo ya tathmini inayofanywa hivi sasa yaani *Gas Institutional and Regulatory Study* chini ya mradi wa Songo Songo. Matokeo ya tathmini hii yanategemewa kutolewa mapema mwakani.

Serikali imelazimika kugharamia fedha za uendeshaji wa *TPDC* kutokana na *TPDC* kutokuwa na chanzo cha fedha baada ya kuanzishwa kwa soko huru la mafuta yaliyosafishwa na kuondolewa kwa *TPDC* kwenye mfumo mzima wa biashara hiyo.

Aidha, shughuli za utafutaji mafuta na gesi ni za umuhimu mkubwa Kitaifa na ni za lazima zitekelezwe. Jukumu la Serikali kuisaidia kifedha *TPDC* linatarajiwakwisha mara mradi wa kuendeleza gesi ya Songo Songo utakapokamilika mwezi Mei, 2004. *TPDC* inategemea kupata fedha za kujientesha kutokana na kuuza gesi na hivyo kuondokana na kutegemea Bajeti ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 1995 - 2003, *TPDC* imeshiriki katika mikutano 35 ya utangazaji wa maeneo yaliyo wazi ili kuvutia wawekezaji katika utafutaji wa mafuta ya petroli kama ifuatavyo:-

Mwaka	1995	-	3
Mwaka	1996	-	4
Mwaka	1997	-	9
Mwaka	1998	-	3
Mwaka	1999	-	6
Mwaka	2000	-	2
Mwaka	2001	-	3
Mwaka	2002	-	5

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* imeingia mikataba na makampuni saba ya utafutaji mafuta na kwa sababu orodha yenyewe ni ndefu, nitampatia Mheshimiwa Mbunge orodha hii mara baada ya kujibu swalii hili.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa *TPDC* imekuwa ikifanya kazi ya utafutaji wa mafuta na kwa kuwa kuna minong'ono mingi inayozagaa kwamba mafuta yamepatikana maeneo ya Pemba na Mikoa ya Pwani, je, Serikali inasema nini kuhusu minong'ono hii ili wananchi waweze kupata uhakika wa hali halisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa ipo mikataba ya matarajio ya upatikanaji wa mafuta juu ya mgawanyo wa mapato yanayotokana na mafuta utakavyokuwa (*Sharing Agreement*) kama vile mikataba ya madini na kwa kuwa mikataba hii ilifanyika miaka mingi iliyopita je, Serikali ina mkakati gani ya kuipitia upya mikataba hii ili iweze kuoana na mabadiliko ya mfumo wa biashara hivi sasa duniani? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kumekuwa na minong'ono kwa maana ya kutangazwa katika vyombo vya habari mwezi Machi, 2003 kutokana na mkutano uliokuwa ukiendelea mjini Nairobi kwamba Tanzania ina mafuta. Serikali ilitoa ufanuzi wa taarifa zile na kusema kwa kweli kilichosemwa katika mkutano ule ni kwamba tathmini iliyofanyika baina ya *TPDC* na kampuni moja ya kutafuta mafuta katika kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi inaonyesha kwamba utafiti zaidi ukifanyika katika maeneo hayo basi huenda mafuta yakapatikana na kama yatapatikana yatakuwa pengine ya kiwango cha kuridhisha kibiashara. Lakini hakuna taarifa ambazo zimetolewa kwamba sasa hivi Tanzania mafuta yamepatikana. Nadhani ni muhimu kulizingatia suala hili ili tusije tukatoa matarajio yasiyokuwa na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu mikataba, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itafanya kazi ya kuipitia upya aina ya mikataba hii ambayo iliandikwa miaka ya nyuma hapo tutakapokuwa na uhakika kwamba mafuta yanaweza kupatikana na kampuni gani zinaweza kuingia katika utafutaji wa mafuta hayo. Hiyo ni kazi ambayo lazima itafanyika kutokana na muda wa kushughulikia masuala kama haya kupita.

Na. 58

Tetemeko Lililotokea Dodoma Novemba, 2002

MHE. KHERI KHATIB AMEIR aliuliza:-

Kwa kuwa tulipokuwa Bungeni Dodoma mwezi Novemba, 2002 palitokea tetemeko la ardhi na kwa kuwa Serikali ilitoa taarifa Bungeni iliyoeleza kuwa tetemeko hilo lilikuwa kubwa au la aina yake katika historia ya Tanzania na kwamba vipimo vyta tetemeko hilo vilichukuliwa na kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kuhakiki ukubwa wa tetemeko hilo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kulieleza Bunge hili ni nini matokeo ya vipimo hivyo na vina maana gani kwa tafsiri nyepesi?

(b) Kwa kuwa tetemeko hilo liliathiri sehemu fulani za Ukumbi wa Bunge pamoja na Jengo la Ofisi za Bunge, je, ni nini taathira za nyufa na mipasuko iliyotokea kwenye Ukumbi na Jengo la Ofisi za Bunge na Serikali imechukua hatua gani za matengenezo mpaka sasa na kama bado ni kwa nini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Ufa la Afrika ya Mashariki linapita Tanzania katika mikondo mikubwa miwili, mmoja upande wa Mashariki ukihusisha Maziwa Natron, Eyasi na Manyara na mwengine upande wa Magharibi, ukihusisha Maziwa Tanganyika, Rukwa na Nyasa. Sehemu nyingine za mikondo hii mikubwa zina mikondo midogo midogo inayokuwa na mielekeo tofauti na hii mikubwa.

Matetemeko ya ardhi husababishwa na misuguano ya miamba wakati miamba inapoachana chini ya ardhi. Aidha, matetemeko mengine husababishwa na Volkano. Hapa nchini kwetu matetemeko yanatokana na misuguano ya miamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6 Novemba, 2002, Serikali ilitoa taarifa Bungeni kuhusu tetemeko la ardhi lililoikumba Mkoa wa Dodoma na Mikoa ya jirani. Tetemeko lilitokea tarehe 4 Novemba, 2002 saa 12.20 asubuhi na pia kurejea saa 5.00

asubuhi. Uchunguzi ulifanyika mjini Dodoma na baadhi ya vitongoji vyake kama vile Zuzu, Chimwaga, Makole na kadhalika.

Ukubwa wa tetemeko ni kama ambavyo tulitangaza mwaka jana lilikuwa ni la ukubwa wa 5.6 katika kiwango cha Kimataifa kinachoitwa *Ritcher Scale*. Chimbuko la tetemeko (*Epicenter*) likuwa kilometra 60 Kaskazini ya Mashariki ya mji wa Dodoma katika kijiji cha Solowu maeneo ya Milima ya Chenene. Takwimu hizi zimepatikana kutokana na ushirikiano na vyombo mbalimbali vya kutathmini matetemeko ya ardhi hasa Shirika la Marekani linaloitwa *Geological Survey* kupitia mtandao wa *Internet* na pia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la tetemeko hilo lilikadiriwa kuwa la kina cha kilometra 10 chini ya ardhi ambacho kwa mtazamo wa matetemeko ni kina kifupi na hivyo madhara yake huwa yanakuwa makubwa kuliko yale yenyé kina kirefu.

Kulingana na maelezo haya, inategemewa kwamba maeneo yaliyo pembezoni mwa Bonde la Ufa kama Dodoma na mengineyo si ajabu kukumbwa na matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunashauri kwamba tuzingatie ujenzi wa makazi bora kwenye maeneo tarajiwa yaani maeneo haya ambayo yanaweza yakakumbwa na tetemeko la ardhi mara kwa mara ambayo yanaweza kuhimili na hatimaye kuzuia madhara makubwa yanayoambatana na matetemeko.

Serikali haikupeleka vipimo nje ya nchi bali vipimo vya ukubwa (*Magnitude*) na mahali pa chimbuko (*Epicenter*) vilipatikana katika mtandao wa *Internet* kutoka kituo cha kufuatilia matetemeko ya ardhi ya Marekani na vipimo hivi vilitumika katika kuwaelekeza wataalam wetu kufahamu chimbuko na mahali tetemeko lilipotokea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tetemeko liliathiri jengo la Bunge kama tulivyoeleza hapo awali. Tathmini ya kina ya kiufundi (*Engineering*), ilifanywa na Wizara ya Ujenzi na wataalam katika Kitengo cha Jiolojia walitathmimi uharibifu (*Intensity*) na kubaini kwamba uharibifu mkubwa ultioka karibu na chimbuko la tetemeko kwa viwango mbalimbali kulingana na maeneo ambayo yalikuwa karibu na tetemeko la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la matengenezo ya Jengo la Bunge yaliyotokana na uharibifu uliofanywa na tetemeko hilo lililotokea mwaka 2002 hasa kuhusu ukumbi wa Bunge, nadhani Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima Ofisi ya Spika ndio ambayo inaweza ikatoa taarifa nzuri zaidi kuhusu suala hili.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa vile Dodoma imeamuliwa kuwa ni Makao Makuu ya Serikali na kwa vile kumekuwa na hii tabia ya kuwepo kwa tetemeko kila baada ya muda fulani hata juzi tu

tarehe 14 Juni, 2003 kulitokea tetemeko, je, Serikali inatuambia nini kuhusu uamuzi huo na usalama wa majengo ambayo yanatarajiwa kujengwa siku za baadaye?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, Mheshimiwa Waziri anashauri nini kuhusu milango ya kutokea katika jengo hili wakati ambapo janga litatokea mfano tetemeko lililotokea siku ile?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kama ambavyo tumejibu kwenye swalilizwa eneo letu la Dodoma ni moja ya maeneo ambayo yana matetemeko ya mara kwa mara na juzi lilitokea tetemeko saa 12.10 na likuwa la sekunde tatu na likuwa la kiwango cha Kimataifa (*Ritcher Scale*), 5.2 la pili kwa ukubwa ukilinganisha na lile lililotokea tarehe 4 Novembra, 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kama ambavyo nimejibu katika swal la msingi ni kwamba Idara za Serikali zinazohusika ikiwa ni pamoja na Wizara ya Nishati na Madini, Ujenzi na kadhalika wanathathmini haya na kama nilivyosema awali taarifa zilizoandaliwa pia zilijumuisha Taasisi au Idara mbalimbali. Naamini kabisa kwamba wanaohusika na majengo na kama ambavyo tulitangaza mwaka jana watakuwa na uwezo wa kupata ushauri wa aina ya matetemeko na viwango ambavyo vimetokea.

Kwa bahati mbaya matetemeko haya huwezi kutabiri kwamba kesho litakuja lingine la kiwango gani. Lakini kutokana na historia ya matetemeko ya nyuma basi inawezekana kutoa takwimu za aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kusema kama mnavyofahamu wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha anawasilisha Bajeti yake hapa, Serikali ilitamka kwamba zimetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi mpya wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa ujenzi huu mpya unaokuja pamoja na mambo mengine masuala haya ya matetemekona kujenga ukumbi ambao una nafasi zaidi na kadhalika yatatiliwa maanani.

Na. 59

Mikataba

MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA aliuliza:-

Kwa kuwa Mikataba yoyote inayofanywa kati ya nchi yetu na nchi nyingine kupitia Wizara zinazohusika hufanywa kwa niaba ya wananchi, wakiamini kwamba Serikali hifanya hivyo kwa kutambua na kuzingatia maslahi ya Taifa kwanza na masuala mengine yafuate baadaye:-

(a) Je, wananchi wanaruhusiwa kuiona na kuelimishwa juu ya Mikataba hiyo kabla ya kuwekewa saini kama wangependa kufanya hivyo na je, wanaruhusiwa kutoa maoni na mapendekezo yao na yakaheshimika kwa manufaa ya Taifa?

(b) Je, Wabunge wanaweza kupatiwa nakala za Mikataba ya Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), *NBC* na *TANESCO* katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti ili wajielimishe kwa kuwa tayari kutoa majibu sahihi kwa wananchi?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatana na fungu la 80 la Mkataba wa Kimataifa unaohusu Mikataba yaani *Vienna Convention on the Law of Treaties* wa mwaka 1969, Mikataba baina ya nchi moja na nyingine inatakiwa baada ya kusainiwa na wawakilishi wa nchi husika, kusajiliwa na Ofisi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kuchapishwa. Hatua hii huifanya Mikataba hiyo kuwa wazi baada ya kuchapishwa kwenye kumbukumbu za Umoja wa Mataifa. Mikataba ya aina hiyo inaweza kupatikana. Aidha, katika hatua za awali, wananchi wanaweza kushirikishwa kufikia makubaliano yatakayokuwa kwenye Mikataba hiyo kutegemea na maudhui na mahitaji ya Mikataba inayohusika.

(b) Katika mgawanyo wa madaraka baina ya nguzo tatu za uendeshaji na nchi, jukumu la kuingia Mikataba ya biashara ni la Serikali (*Executive*). Serikali hupaswa kuheshimu desturi mbalimbali za biashara kuhusu Mikataba. Siyo mila kwa nakala za Mikataba kugawiwa, ikiwa ni pamoja na ya *TTCL*, *NBC* na *TANESCO*.

Hata hivyo kwa Wabunge, wakiwa kama wawakilishi wa wananchi, wanazo njia mbalimbali za kuweza kuihoji Serikali katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwemo Mikataba inayoingia, kupertia maswali kwa Mawaziri, katika kujadili utekelezaji wa kila Wizara katika Mkutano wa Bajeti, katika jukumu zima la kutunga sheria na pia kupertia shughuli za Kamati za Bunge.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Je, Serikali haioni kwamba ili kupunguza mivutano kati yake na Wabunge kwa Mikataba ambayo baadaye inakuja kuonekana haifai kwa nchi yetu, ni vema hatua za mwanzo za kusaini Mikataba hii zikahusisha Wabunge ili baadaye Wabunge na Serikali wawe na sauti moja katika kuelezea wananchi juu ya jambo lililotendeka, haioni kwamba kuna ulazima wa kufanya hivyo?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, aliyozungumza ni sahihi na haya ambayo anayazungumzia ya kutoa mvutano baina ya Serikali na Bunge ni sahihi. Lakini suala la msingi ni kwamba shughuli za Serikali ikiwa ni pamoja na kuingia Mikataba, shughuli za Bunge kwa kweli ni kutunga sheria na shughuli za Serikali ni kuendesha shughuli za Serikali kufuatana na Ilani, kuweka sera na kuwa na mawasiliano na wafanyabiashara, benki mbalimbali kama *IMF*

na *World Bank* na baada ya hapo kuweza kuwasilisha matokeo ya shughuli hizo katika Bunge. Lakini tukisema kwamba tulete Mikataba ndani ya Bunge, hii haifanyiki mahali popote na kutakuwa na athari kubwa kwa sababu utapoteza usiri. Haya ni makubaliano baina ya pande mbili na italeta urasimu.

Sasa hivi tunazungumzia kuwa na *one stop centre* kwamba wawekezaji waende mahali pamoja na shughuli zao ziweze kushughulikiwa haraka. Sasa kama tutakuwa tunaleta katika Bunge, hii italeta urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, akiwa ni Mwalimu, hii siyo cheti cha shule, ni Mikataba, upo usiri mkubwa. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na tupo kipindi cha Bajeti, kwa hiyo, nafasi ipo wazi kuijua hiyo siri wakati wa mijadala ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea kuna matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, anaomba Kamati ya Uongozi wa Kambi hiyo iikutane Ofisi ya Kambi ya Upinzani mara baada ya kipindi hiki cha maswali. Pia Mheshimiwa Getrude Mongella, anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, wakutane chumba Na. 56 mara baada ya maswali.

Vile vile Mheshimiwa Leonard Derefa, anawatangazia Wabunge wote wa Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Singida, Kigoma na Rukwa, wakutane chumba Na. 81. Yeye alitaka wakutane saa 5.00 asubuhi, lakini namshauri iwe baada ya Bunge saa 7.00 mchana, saa 5.00 asubuhi siyo muafaka sana. Baada ya maswali ni zile Kamati ambazo zipo kwenye Kanuni ndizo mara nyingi zinakutana, lakini Kamati hii wakutane baada ya kuahirishwa Bunge saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, pia kwa wale ambao mnazo *Order Paper*, nadhani wote mnazo kuna *Order Paper* mbili zimetolewa lakini nyingine ilitolewa kwa makosa, mojawapo ina kipengele cha kauli za Mawaziri na kwamba Waziri wa Fedha atoe kauli, hiyo haimo. *Order paper* ambayo itatumika ni ile ambayo hoja za Serikali zinaendelea na tunaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu Bajeti.

Baada ya maelezo hayo sasa tunaendelea. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/04 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/04

(*Majadiliano Yanaendelea*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza leo asubuhi. Naomba na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nitangulize neno la kwamba naiunga mkono hoja hii toka mwanzoni tu. Namwunga kabisa mkono Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa mara ya kwanza ni nzuri kuliko zilizotangulia. Nawapongeza sana kwa mambo makubwa mawili, kwamba wameangalia kero za wananchi na hususan mambo mbalimbali ya kodi, lakini vile vile kwa kuwezesha uchumi kuendelea kukua. Hapo tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niwapongeze Wabunge wote waliochaguliwa wa Chama cha Mapinduzi na Vyama vyta Upinzani, karibuni sana Bungeni. Napenda vile vile niwapongeze Bwana Kitilya na Bwana Luoga, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, kushika nafasi ya wenzao kule *TRA* na nawapongeza wale waliokuwa wametangulia ndugu Sanare na wenzake kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najua kwamba hakuna kazi ngumu kama kuanzisha jambo. *TRA* imeanzhishwa mikononi mwa ndugu Sanare na kundi lake na ndiyo imetoea mwelekeo wa makusanyo mazuri ya mapato kutoka bilioni 25 mpaka bilioni 105. Wanastahili pongezi watu hawa.

Sasa Ndugu yangu Kitilya, sisi walimu tunasema ukirithi shule mbaya sana *you are very lucky*, kama shule ile chafu chafu, wewe ukaenda, una bahati, kwa sababu wewe ukifagia tu barabara watu wanasma kuna mabadiliko. Lakini ukirithi shule nzuri sana, una bahati mbaya, hata Wizara hivyo hivyo, kwa sababu hata jani likianguka wanasma shule imeshaanza kuwa mbaya, angalia majani barabarani. Kwa hiyo, una kazi, Ndugu Sanare amefikisha makusanyo, mahali pazuri sana. Kazi unayo baba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba kuchangia katika sehemu mbili. Moja ni suala la nishati kwamba nishati ya umeme katika nchi yetu ni ya juu kupita kiasi na matokeo yake miti inakwisha, maana zamani huko kulikuwa na *category* tatu za watu. Kuna waliokuwa wanatumia umeme ambao ni wengi, kuna waliokuwa wanatumia mkaa, walionekana kidogo wamepiga hatua na kuna waliokuwa wanatumia kuni. Kwa hiyo, kwanza wa umeme, halafu kuna wa mkaa na halafu kuna wa kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme walikuwa wanatumia watu wazito maofisa wa *Oysterbay*, halafu mkaa watu wa katikati kama walimu, madaktari na kadhalika, halafu kuni ni raia wetu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hakuna cha bosi wala nani kila mmoja nyumbani kwake ni mkaa. Watu walishayafungia majiko ya umeme, tulishayafungia zamani mende tu ndiyo wanaojaa, nani atawenza bili za umeme? Matokeo yake sasa wananchi wa kawaida wamejiajiri katika suala la kuchoma mkaa na kukata miti kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maliasili na Utalii, anayeshughulikia mambo ya wanyama na miti, upande wa miti ameshindwa. Lakini kwa wanyama na mambo ya utalii, Waziri huyu tunampa hongera sana, kwenye suala la miti imeshhindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unabisha, nitaje maeneo, maana yake mimi kila mahali nikipita niko *very sensitive on the road kuangalia what is happening*.

Naomba atume watu wake sasa hivi waangalie kutoka Morogoro kwenda Dodoma, kutoka Dar es Salaam mpaka Mikese - Morogoro, kutoka Chalinze mpaka Segera, kutoka Ruaha Mbuyuni mpaka njia panda ya *IDM*, kutoka Senjele mpaka Songwe kule Mbozi na barabara ya kwenda Sumbawanga, aende hivi sasa. Mimi naita hivi umeanzishwa ushirika wa mkaa. Kuna ushirika mdogo, unakuta kwenye nyumba barabarani magunia 10 au 20, lakini unakuta *union* kubwa kabisa ya mkaa, tena kama vile ruhusa kila mmoja afanye anavyotaka, kule zamani kulikuwa na watu ambao wamekata leseni ndiyo wanachoma mkaa.

Siku hizi hakuna leseni, kila mmoja ni mchoma mkaa na mradi huu ni rahisi mno, kwa sababu unakata mti kisha unafukia na kesho hela inapatikana. Sasa kila mmoja ameijajiri kwenye miti.

Kwa kweli mimi nasema simlaumu Waziri kwa sababu kuna Makamishna wake au sijui Wakurugenzi wake wa mambo ya misitu. Yeye Mheshimiwa Zakia Meghji, anafanya kazi nzuri sana. *She is very hard working lady*, lakini kwa suala hili la miti kama tutaendelea hivi ikifika miaka 10 ijayo nchi itakuwa jangwa. Kuna Mswahili mmoja ameandika kwenye nyumba yake: “Kama unaona misitu ni tatizo jaribu jangwa.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *union* za mkaa tunaomba ziondolewe barabarani zinatutia kinyaa sisi Waheshimiwa Wabunge, maana hapa tunaongea juu ya hifadhi, tunakazana juu ya mazingira, lakini ndiyo wanatuonyesha kwamba oneni sasa. Lakini Mheshimiwa Daniel Yona, aangalie hiyo *TANESCO* yake inayopandisha umeme kiasi hiki ni *TANESCO* ya wapi, hawawezi kwenda kwenye nchi nyingine wajifunze? Kwa nini mambo haya ambayo ni ya msingi yanakuwa na bili za juu? Sisi tumekuwa maskini kiasi hicho kwa kupandisha mara mia moja? Mimi nadhani tufike mahali tuhurumiane. Hilo moja ambalo nilitaka kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la madini, mimi kwangu kuna milima mingi na madini mengi sana, lakini bado watu hawaja-survey. Kwa hiyo, sasa hivi nitazungumzia yale ninayoyafahamu, madini ya Geita, *Tanzanite* ambapo bahati nzuri nilikwenda kule na Tume. Sasa mambo ambayo mimi nayaona kwenye madini ni kwamba Mikataba hiyo ni bora itazamwe sawasawa, kwamba mtu atachimba miaka mingapi bure na kwamba Mikataba hiyo ina ubora gani kwetu sisi Watanzania. Hilo lazima litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana niliuliza swali hili la Mkataba, Mheshimiwa Waziri amenijibu hapa, mimi nilikuwa nacheka kwa sababu ni rafiki yangu sana. Nasema siyo lazima Mkataba uje hapa Bungeni, lakini kuna Kamati za Bunge. Kuna Kamati tunayo hapa ambayo ingeweza kushughulika kwa niaba ya Bunge. Mkataba uletwe hapa Bungeni kufanya nini, sisi hatuwezi kuwa watu ambao tunafanya vitu kienyeji. Kama kuna Mkataba mwingine, wanaufikisha kwenye Kamati na Kamati ikiridhika basi, mbona mambo mengi Kamati inatumika, ni kitu cha namna hii, siyo lazima iletwe Bungeni, itakuwa ni kichekesho ikiletwa hapa. Lakini kuwe na Mikataba mizuri juu ya madini ili imwezeshe Mtanzania kufaidi zaidi kuliko mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni kidogo sana na kwa kweli kwa mtu maskini. Sisi Wanyamwanga, kabilia langu kuna kanguo kanaitwa Mupetee. Mupetee ni kanguo ka kufunga hapa tu, kwingine achana nako. Kanafunga kwenye uzi hivi, unafunga tu hapa basi.

Sasa akija mtu akasema niuzie shamba ambalo utapata *billions of money*, anakupatia Mupetee, kama kweli ulikuwa unatembea uchi utampenda na utapiga vigelegele, unaweza kucheza hata ngoma, maana kwanza ulikuwa *naked*, lakini sasa bahati nzuri amekuletea kamupetee. Kwa hiyo, wewe kamupetee unaona umepata kweli, ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno. Ukiona wamejenga sekondari wewe unaona umefaidika sana. Hii ni dalili ya umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unasema wamefyeka kabarabara hapa, wameweka kokoto yaani wewe unashangilia wakati mtu kapata *billions of money*, lakini kakufykeea kabarabara kwa shilingi milioni tano, sita au kumi, unasema hawa ndiyo wenyewe, hawa ndiyo wenyewe. Jaman! Hivi kweli umaskini umefika kiwango hiki kwamba unashangilia hata Mupetee wakati hujapata suruali wala kaptula bado? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi angalau watupe kaptula. Mheshimiwa Rais, Benjamin Mkapa, anasema tumekosa suruali basi tupate kaptula, potelea mbali. Hiyo ndiyo lugha nzuri kwamba tukose suruali lakini tupate kaptula, lakini sasa mupetee ndiyo inakuwa mbaya zaidi halafu unashangilia na kurukaruka kwamba enhee nimevaa nguo na kenyewe kanaruka kanasogea lakini bado. Tusishangilie vitu ambavyo kwa kweli watu wakikaa wanakunywa bia wanaanza kushangaa, wanasesma hivi hawa watu tumewaokota kweli, hawa ni viokote.

Mimi nashangaa watu wote tunashangilia vitu vidogo, hata kama wangejenga majengo makubwa, lakini tuangalie wao wanapata nini kwa sababu lazima haya madini yawenze kutukomboa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima ujiulize kama mimi umenipa kumi wewe umepata ngapi *is a good comparison* na bahati nzuri hizi *internet* tumeweka ulimwengu upo wazi katika *globalization* hii. Kwa hiyo, Mbunge au mtu yejote akitaka kujua *Tanzanite* inauzwa kwa kiasi gani kwa mwaka, anaipata kwa dakika moja tu. Kwa hiyo, ukimjibu hivi hivi tu kwa kumdanganya, anakushangaa. Sasa mupetee hatuwezi kwenda nayo sisi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hii Mikataba tuangalie wananchi wanafaidi nini na tunalinganisha nini na nini. Kuhamisha migodi hili jambo liishe kabisa, wale watu wasibebe udongo wowote, wanapeleka wapi? Kwa nini wanahamisha udongo na hii habari ya *Tanzanite* kusema ipo kwenye EPZ aanze pale Mheshimiwa Daniel Yona. Aanzishe hapo uchongaji asilimia zote mia ziwe pale, ajira itapatikana kwa watoto na mapato yatakuwa makubwa. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, aweke pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mimi naijuliza, sisi Serikali imetutuma, imemtuma Jenerali Mstaafu Robert Mboma na sisi wengine kwenda kufanya tathmini ya mambo yanavyokwenda kule na mapendekezo mbalimbali kwenye Serikali ili *Tanzanite* iweze kuzalishwa vizuri na migongano kati ya wale wa makundi mbalimbali iweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kule, tumefanya kazi, tumelipwa hela nydingi tu, halafu ripoti tumetoa, hakuna ripoti inayotangazwa kokote wala kutolewa kwa Wabunge. Hivi kweli Mheshimiwa Daniel Yona, *ana-implement*, kwa sababu mimi masuala yanayofanyika sasa hivi sielewi ni kwa nini? *Why don't you make that report available? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ninyi mlitutuma na vile vile mmetusaidia sana na sisi tulisaadiana, mlitumia hela nydingi, sasa ripoti katika uwazi si leteni Wabunge waisome! Kweli sisi mwaka mzima, inabidi tutoe ripoti ili Wabunge nao wasaidie, mna-*implement* ndiyo, lakini kwa nini ripoti hii ya Jenerali Mstaafu Robert Mboma, isitolewe kuhusu *Tanzanite*?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumependekeza mambo ya nembo hakuna. Sasa kunaonekana kama kuna usiri wakati kitu kipo wazi. Mimi naona hili la *Tanzanite* madini pekee katika ulimwengu huu halihitaji nembo wala nini yenye ni nembo *by being unique*. Yote tumependekeza na kwamba wale wengine wanataka kuhamisha asilimia 90 wapeleke *South Africa*. *In course of two, three years or ten* wanakuwa wamehamishia madini yote kule, kwa hiyo *Tanzanite* ionekane ipo *South Africa*. Jamani tuwe waangalifu kidogo, nchi ni yetu, sisi ni wao na bahati nzuri wote hapa tunashukuru Mungu ametujaalia, tunesoma soma kwa niaba ya wananchi. Hatuwezi kuwa tunapewa vitu vidogo vidogo tunashangilia *the whole night and morning*, kumbe tumepewa mupetee tu basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali isiwe ni mupetee, kiwe ni kitu kikubwa, ukinipa kumi, *how much do you get?* Haya ndiyo maswali ya kujiuliza. Inatisha sana. Ukikuta *gold* kule inasombwa, udongo unasombwa, kwa kweli wakikaa peke yao wanacheka. Kweli wanajenga shule, lakini haisaidii, bado tunahitaji kulinda madini yetu pamoa na kulinda miti yetu. Lakini kamwe tusikubali mupetee, tukubali angalau kaptula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza kabisa ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Makomredi walioingia hapa kwenye nafasi ya Ubunge, Ndugu yangu Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Edward Ndeka kutoka Kigoma Kusini na Mbunge mwingine Mheshimiwa Nazir Karamagi kutoka Bukoba Vijijini na mwisho kabisa Komredi tokta Mpanda Magharibi, Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed. Nawapongeza Wabunge hawa kwa furaha kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kuipongeza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu Wabunge ambao waliondoka hapa Bungeni kwa kutokuhudhuria Vikao vya Bunge mara tatu. Mimi siwapongezi wao, naipongeza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyowaruhusu kurudi tena hapa. Nina hakika nimeelewaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza wenzetu ambao kwa bahati nzuri kabisa wamepata nafasi ya kuongoza chombo kizito *TRA*. Yupo mwenzetu Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga. Wamepewa nafasi hiyo, mimi nina matumaini makubwa kwa sababu gani wale waliopita hasa kabisa *Commission General*, Ndugu Sanare amefikisha nchi yetu hapa, sasa tunakusanya bilioni mia moja.

Ninampongeza mno, ametuonyesha njia, amepewa chombo hicho kikiwa kichanga kabisa na amekifikisha hapa. Sasa komredi Kitilya ninamfahamu, sisi ni marafiki tangu Arusha pia Dar es Salaam, sasa anza hapo, piga bilioni 140 au bilioni 150 na bahati nzuri una timu nzuri sana ya akina Lauwo. Nasema tunakutakia kila la kheri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu maalum naomba nimpongeze *Accountant General* Mama mmoja anaitwa Blandina Nyoni. Kwa kipindi kilichopita nilikuwa kwenye Kamati ya *PAC*. Ameonyesha uwezo mzuri sana na naomba Bunge lijue kwamba haya ni matunda ya *TRA*, huyu mama ametokea *TRA*, ni matunda ya Sanare. Mama huyu ana uwezo mkubwa ningeshauri kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amlinde huyu komredi, anafanya uchambuzi wa kina kabisa juu ya namna Serikali na mapato yake na jinsi yanavyotumika, anapambana na *system*. Sasa mlinde na tutauliza mwezi Desemba, je bado yupo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja kwa dhati kabisa nampongeza ndugu yangu, rafiki yangu aliyekuwa Mweka Hazina Mkoo wa Chama, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, safi sana na barabara kabisa umetukumbusha sera za Chama katika hoja yake. Nimepata moyo kweli kwa jinsi Waziri wa Fedha, alivyokuwa na upeo mzuri na mimi nadhani upeo wake unatokana na maeneo mawili.

Kwanza, kuwa katika *Cabinet* kwa muda mrefu, lakini kubwa zaidi ni kuwa Mkoo wa Mkoa wa Mbeya, ile lugha ya mjini anajua, ndijo maana Bajeti yake

inazungumzia habari ya watu wa chini, hawa ndiyo nawaita ma-*comrade* wengine wote ndugu tu, lakini *comrade* ni suala lingine. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifike mahali nifanye jambo moja tu, nalo ni kwamba naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hakuna kitu ambacho wananchi kimewapa faraja upya kabisa kama suala la kuondoa kodi ya maendeleo.

Mimi napenda kuwathibitishia kwamba nimekuwa Mkuu wa Wilaya kwa miaka 20 mfululizo, nimekuwa Katibu wa Chama kwa miaka 35. Lakini napenda kuliambia Bunge leo katika miaka yote niliyokuwa *DC* miaka 20 sijazungumzia kodi. Nilikuwa naamini kwamba madhari watu wa Mbeya wamejenga uwanja wao wa Sokoine, Iringa wamejenga uwanja wa Samora Machelle, Mwanza wamejenga uwanja wa Kilumba, Tabora uwanja wa Ali Hassan Mwinyi na Morogoro uwanja wa Jamhuri.

Watanzania hawa wamejenga viwanja hivyo kwa kodi ilioongezwa kwenye soda ya Fanta, Cocacola, Bia, Sigara, nikafanya uchambuzi kwamba mimi kwa miaka 20 sitazungumza habari ya kodi. Kwa sababu Fanta hiyo ingekatwa kwa nchi nzima ingekuwa kodi ya maendeleo imeondoka, tuige mfano wa kukata Fanta, Songea, *Maji Maji Stadium* wamejenga uwanja, Fanta ile ingekatwa kwa nchi nzima kodi ya maendeleo ingeondoka zamani sana. Kwa hiyo, nikasema sizungumzii mpaka Waziri wa Fedha atapofuta kodi hiyo, *comrade* Basil Mramba, ahsante sana umefuta kodi ya maendeleo. Nakushukuru sana. Kodi ya maendeleo imeleta kero kubwa sana, lakini nasema kwamba kero hii imeshughulikiwa vizuri sana na Waziri wetu wa Fedha na hasa kabisa Amiri Jeshi Mkuu, Afande Benjamin William Mkapa na Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije eneo ambalo linazungumzia habari ya kilimo. Kilimo kimezungumzwa sana katika ukurasa wa 28, sasa kilimo wote tunakubali ni uti wa mgongo, lakini inaonekana nadharia hiyo imekuwa kwa miaka yote iliyopita. Sasa tukubaliane kabisa kwamba asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na nchi yetu inategemea kilimo tuseme sasa basi tutekeleze. Kwa hiyo, napata taabu sana wakati kitabu hiki kinazungumzia habari ya Mikoa minne kwamba tuanze nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mito inayotoka Iringa, Njombe, Makambako, Ruvuma, Songea ndiyo mafuriko tunayoyapata Morogoro, ukisikia Pantoni imezama Morogoro siyo mvua ya Kilombero ni mvua za Iringa, Njombe, Songea kutokana na mito ile. Sasa nashangaa wanasema umuhimu wa kwanza ni Mikoa minne, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa, unasahau yale mabonde ya Kilombero, nikaseme eeh, hapa yapo matatizo hapa. Yapo mabonde mazuri ukipeleka mbolea leo kwenye Wilaya ya Kilombero na Wilaya ya Ulanga wanakushangaa mbolea ya nini, pale unapanda chochote mwaka mzima na unavuna.

Mheshimiwa Charles Kagonji, ametukumbusha, pale kuna Mito siyo Mito ya muda mfupi ni Mito ya kudumu, sasa unaachaje Bonde la Kilombero, mabonde ya Ruaha, mabonde ya Mtimbira, mabonde ya Itete, mabonde ya Minaya, unasema tukusanye nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nadhani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, atakapokuwa anawasilisha hotuba yake hapa atusaidie, maana Waziri wa Kilimo na Chakula, ametoka hapa amekwenda mpaka Mwanya ameona mabonde yale. Sasa yale mahindi mabichi mnayonunua Dumila mwaka mzima halafu Mkoa wa Morogoro mnauacha na mahindi mnanunua ya kuchoma.

Kwa hiyo, kwa kweli napata taabu sana kabisa, Mkoa wa Morogoro tunaitwa *a sleeping giant*. Sasa mimi naomba sana kwamba hitaji letu sisi Mkoa wa Morogoro ni matrekta wala siyo ardhi wala siyo mbolea, mtuletee matrekta tutafanya kazi ya kuwalisha Watanzania tukiungana na wenzetu wa Mikoa hiyo iliyotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine huwezi kufanya kazi katika nchi kama hii ukasema mazao yote ni *first priority* una matatizo. Kwa hiyo, ninakubali kabisa na ninaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuwa na mazao mawili kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu nilikuwa *DC* wako Tunduru, wananchi wa Tunduru wanalima mihogo, mpunga, korosho na kila kitu. Lakini nikasema watu hawa hawawezi kuwa na njaa kila mwaka, nikaamua kwamba kila mmoja analima heka mbili za mhogo, *operation Kunjatu* (Kumaliza Njaa Tunduru), tukafuta njaa mpaka leo hakuna njaa. Je, ningesema watu wote walime mhogo, viazi, mahindi, lazima uwe na *priority* unapoongoza nchi.

Kwa hiyo, naungana kabisa na hotuba ya Waziri wa Fedha kwamba lazima Wilaya zetu zigaiwe maeneo na walime mazao mawili, zao moja la biashara na zao moja la chakula na wala hii haiwazuii kulima maharage na kuendelea kulima na mazao mengine . Lakini angalau mwelekeo wa nchi tunapita hapo kwa sasa, mambo yakienda vizuri tunakwenda zao lingine. Nasema hilo ni jambo la msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali inazungumzwa mfuko wa kuwasaidia wananchi mikopo kwa ajili ya uvuvi na kadhalika. Mimi nashangaa sana, mimi nadhani tukubaliane kwamba kuna haja Waziri wa Fedha, kuna na Mfuko mwингine ikiwa Benki ya wananchi (*NMB*) ipo, peleka fedha hizo pale tuwe na chombo kimoja kizuri chenye mwelekeo wa aina moja.

Mimi nina mfano, ninayo hapa hundi ya *NBC* na mimi ni mteja wa *NBC*, lakini hundi hii nikienda kwenye Jimbo ambako kuna Benki ya *NMB* nachukua fedha bila matatizo, benki ya watu iko Mahenge, iko Kilombero, Handeni, Lushoto, Tunduru, Kilosa, weka fedha hizo *NMB* pale huhitaji mfuko mwингine weka fedha *NMB*, mkulima aende, mvuvi aende tuimarishe benki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo hayo ni masuala ya utaratibu tu kwamba nini umuhimu wa kwanza. Kwa hiyo, tunasema kwamba lugha ya mfuko huu haipo, lugha ya mfuko huu iimarishe *NMB*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja zote mbili kwa dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Ulanga Mashariki. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, naona ndiyo anaingia, kama uko tayari endelea.

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwenzangu aanze wakati mimi najiandaa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Abdula Lutavi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda.

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe maoni yangu kuhusu hoja hizi mbili tulizonazo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii na mimi niungane na wenzangu walionitangulia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walionungana nasi kwenye Bunge hili sasa hivi kupitia kwenye uchaguzi mdogo uliofanyika mwezi uliopita na vile vile wale ambao wamerejeshwa Bungeni baada ya kushinda kesi zao Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeza Serikali na Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba zao mbili ambazo zipo mbele yetu hapa. Nawapongeza kwa sababu kwenye hotuba zao unaona kweli usikivu wa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Unaonekana wazi kwa sababu kero nyingi ambazo zimekuwa zikitusumbua kwa muda mrefu zimeshughulikiwa na zimezingatiwa kwenye hotuba hizi, zikiwemo na zile kero za kodi ambazo nyingi zake zimeondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi haijapata kuwa kitu ambacho kinaridhiwa kwa urahisi na wananchi kwenye jamii yoyote ile, historia inatwambia hivi, tunasoma kwenye misahafu na tunasoma kwenye Biblia. Lakini ninachotaka kusema hapa ni kwamba kodi hasa hii ya maendeleo ambayo imeondolewa, kodi hii ilikuwa kero kubwa kuliko zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu adha hii tuliiiona siku nyingi, tuliiiondoa kodi hii na tukaweka utaratibu mbadala sasa yapata miaka 10. Lakini Serikali inapochukua hatua hii sisi tuna kila sababu ya kushangilia na kusema kwamba Serikali sasa imeona vyema. Tunaipongeza Serikali na tunaishukuru kwamba yale manufaa ambayo yanapatikana kwetu kwa kuondokana na kodi hii sasa yamesambazwa ndani ya nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi hii vilevile niitumie kwa kuipongeza Serikali tena kupitia Wizara hizi mbili kwa umahiri ulioonyeshwa na Wizara hizi kwenye

kusimamia utekelezaji wa mpango wa Bajeti zilizotangulia za mwaka 2002/2003. Nasema hivyo kwa sababu kuna mafanikio yanayoelezeka, kuna maendeleo makubwa katika utaratibu mzima wa uchumi wetu. Tumeona kuna ukuaji wa uchumi, tumeona sekta ya utalii imekua mpaka asilimia 7, sekta ya ujenzi imekua kufikia asilimia 11, viwanda vimekua asilimia 8, kilimo kimefika asilimia 5 na kuna ukuaji mkubwa kwenye sekta ya madini tumefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Serikali yetu imesimamia na kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei umeendelea kushuka mpaka imefikia asilimia 4.3 hivi mwezi Aprili uliopita, si hilo tu, akiba ya fedha za kigeni imepanda kwa zaidi ya asilimia 32 tumefikia sasa Dola bilioni 1.5 haya ni ya kushangiliwa. Hizi Dola bilioni 1.5 inasemekana zinatosha sasa kukidhi mahitaji yetu ya bidhaa kutoka nje kwa muda wa zaidi ya miezi nane. Lengo letu ilikuwa miezi nne, hili ni la kushangiliwa, naipongeza sana Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya haya ni kwamba sasa uchumi wetu umekua kwa ujumla, umekua kwa asilimia 6.2 na sasa hivi tunalenga asilimia 6.3. Baada ya kuyaona haya hatuna sababu yoyote ya kukosa matumaini kwamba lengo hili la asilimia 6.3 tunalolilenga kwenye Bajeti hii ambayo iko mbele yetu litafikiwa *inshallah*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya yamejitokeza pamoja na kwamba mapato ya ndani yameendelea kusuasua katika kiwango cha asilimia 12.3 tu ya Pato la Taifa, lakini lengo letu lilikuwa asilimia 12.5 na hii si ajabu ndiyo imesababisha Bajeti yetu kuendelea kuwa tegemezi kwa kiwango kikubwa cha asilimia 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza habari ya ukuaji wa uchumi kwa asilimia 6.2, sasa tunalenga asilimia 6.3 maana yetu ni nini. Hivi kwa maeleo ya Waheshimiwa hapa wanaita viashiria, asilimia 6.3, hivi ni viashiria tu vya mafanikio katika uchumi jumla. Sasa tatizo tulilonalo hapa ni kwamba uchumi jumla unakua, lakini maeleo yake kwa wananchi yanakuwa magumu, kwa sababu mwananchi anataka kuhusisha hili na kuwezeshwa kwake yeze kumudu kwa njia iliyo rahisi kabisa maisha yake ya kila siku, hili ndiyo changamoto tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafanyaje kwenye hali hii. Pamoja na hatua na mikakati ambayo tunatakiwa tuichukue kuweka kipaumbele katika sekta ambazo zinagusa watu wengi sekta kama ya kilimo, ambayo tunazungumza hapa kwa tafsiri ya Kitaifa ya ajira ndani ya nchi hii tunasema inaajiri watu milioni 13 katika wale watu milioni 17 wanaotajwa kwamba ndiyo wanafaa kupata ajira.

Pamoja na mkakati tunaotakiwa tuuveke kwamba lazima twende kule tuweke kipaumbele kule ndipo mafanikio haya katika ngazi ya uchumi mkuu yanaweza kutafsirika kwa urahisi kwa wananchi wa kawaida, basi mimi naona vile vile kwamba iko haja ya kuangalia mchango wa mapato ya ndani kwa Pato letu la Taifa, tukiweza hapo kupaangalia vile vile nadhani tutakuwa tunapiga hatua ambayo inatuelekeza kule tunakotarajia kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye Bajeti yetu mchango wa mapato ya ndani kwenye uchumi wetu, nimekuta kwamba chanzo kikuu ni kodi mbalimbali na hapa nataka kuisifu Serikali kwamba kwa muda mrefu wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba wanaainisha mifumo ya kodi, wanahakikisha kwamba mapato yanasmamiwa na kuhakikisha kwamba yanaelekezwa kule ambako yanatarajiwa kupelekwa. Lakini sasa ni kwamba asilimia 91 inatokana na kodi tu. Mimi nilikuwa naona kwamba kuna haja ya kutazama kama tunaweza vile vile kupata uwezekano wa kuongeza mapato ya ndani kwa kuchangiwa na mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Bajeti mwaka 1999, nimesoma Bajeti ya mwaka ya 2000/2001 na Bajeti ya mwaka 2001/2002, mpaka hii ya leo tunayokwenda nayo nimeona kwamba *Non Tax Revenue* kwa mfano wa mwaka 2002/2003 hii iliyomalizika ni asilimia 8.6 tu ya mapato ya ndani, lakini hii ndiyo ilikuwa lengo, halisi tulioipata ni asilimia 5.3 na leo tunalenga kwamba *Non Tax Revenue* iwe asilimia 8 ya mapato ya ndani, kiwango hiki ni kidogo.

Mimi nina hakika kabisa kwamba tukipata kiwango kikubwa kwenye eneo hili likachanganywa na kodi tutakuwa na kila sababu ya kutegemea kwamba sasa tutapiga hatua, hata hii kutafsiri uchumi mkuu unavyokua, kutafsiri kwenye mafanikio katika ngazi ya wananchi wa kawaida itawezekana kwa urahisi zaidi. Sasa tutaendaje kwenye hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naangalia nimerudi kwenye zile sekta nilizozitaja kwamba ziliwu zimeonyesha mabadiliko makubwa na ukuaji mkubwa kwamba zinawezaje kuchangia hizi. Nilichokiona nimechukua mfano kama wa madini na hili nalitaka nilizungumze kwa kirefu kidogo. Madini hivi hapa tulipofika ukuaji wake tunasema umefika sasa kiwango kikubwa cha asilimia 15.

Lakini mchango wa madini kama sekta katika Pato la Taifa hapa tulipo sasa hivi hajifikia hata asilimia 3 haya hayaendi sawa na hii ni kweli kwamba haiwezi kufikia kiwango hicho kwa sababu kwani tunategemea nini kutoka kwenye sekta ya madini, hapa imesambazwa karatasi hapa, tunategemea mrabaha asilimia 3, tunategemea watu wetu kuajiriwa, ndiyo vyanzo vyetu vya kupata mapato katika madini, tunategemea ushuru wa stempu ndiyo vyanzo vyetu hivyo, tunategemea ushuru wa forodha wanapoingiza bidhaa kutoka nje kwa ajili ya kazi za kwenye migodi, tunategemea eti tupate ushuru wa *VAT* humo humo, hata *Withholding Tax* imekuwa listed kwamba ndiyo namna yetu ya kupata mapato kutoka kwenye madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nadhani kwa namna yoyote utaratibu huu ambao mnasema mapato yetu kutoka kwenye madini utokane na vitu hivi tu, hii haizingatii maslahi ya Taifa letu. Sasa imani yangu mimi ni kwamba ukiwa na madini huwezi kuwa maskini. Kwa nchi kama Tanzania ambayo inazalisha dhahabu zaidi ya tani 30 kwa mwaka na hivi ni viwango vya mwaka 2001, sisi umaskini hauwezi kuwa majaliwa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata taabu sana ninapoangalia hivi Waarabu kwa mfano, wakati wanapata kugundua mafuta walikuwa hawana teknolojia, hawana utaalal wala hawana mtaji, mafuta yale yanachimbwa na Makampuni ya nje, Botswana walivyogundua almasi walikuwa hawana utaalal, hawana mtaji wala hawana teknolojia, yanachimbwa na Kampuni za nje, kama utaratibu mwenyewe ungekuwa kungojea *Royalty, Stamp Duty, Import Duty, VAT* na mambo ya *Withholding Tax*, Botswana isinge kuwa pale leo wala ujeuri huu tunaouona kwa Waarabu usingekuwa upo pale leo. Mimi nadhani kuna tatizo la msingi hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbuka Marehemu Baba wa Taifa, Julius Nyerere, alikuwa anazungumza kwenye mazungumzo yake habari ya mikataba tuliyonayo baina ya Serikali na Williamson Diamonds, akasema wakati sisi tunagundua haya machimbo ya almasi, alisema kwamba sisi hatuna teknolojia, hatuna mtaji na wala hatuna utaalal tumeweka Kampuni ile itufanyie kazi ya kuchimba, sasa akasema hivi. Wakati huo anazungumza hatukuwa tunazungumza habari ya asilimia 25 hii tuliyonayo sasa hivi hisa za Tanzania, tulizungumza kwenye viwango vya 49 mpaka 51. Akasema wakivuna kama bakuli mbili hivi za almasi, sisi tunawambia kwamba bakuli moja yetu, bakuli nyininge baki nayo, lakini ile bakuli wanayobaki nayo wao sisi tunawambia lipeni na kodi, alisema Marehemu Julius Nyerere. Mimi nauona utaratibu huo ndiyo unatuwezesha sisi kuona kwamba tunayo milki katika madini yanayochimbwa ndani ya ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka uwekwe utaratibu hivi sasa tunavyozungumza na ninataka kuungana na wasemaji wote ambao wamezungumza kabla yangu na wale ambao watasema baada ya mimi kwamba mikataba hii ya madini lazima itizamwe katika misingi ya kuona sisi kama Tanzania tuna maslahi katika madini yanayochimbwa ndani ya nchi hii.

Sisi kama wananchi, kama Tanzania lazima ifahamike dhana iwe kwamba Makampuni ya kigeni yanapokuja hapa yanakuja kuchimba dhahabu, *Tanzanite*, almasi ya Tanzania kwa sababu wamekuja na utaalal, *capital*, teknolojia, basi wao wajilipe kwa hilo. Lakini sisi lazima tubakiwe na kitu ambacho kitasaidia katika kukuza mapato yetu ya ndani, ili na sisi tuweze kufikisha mafanikio haya tunayosema yako katika ngazi ya uchumi mkuu kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie tu kwa kusema nataka niishukuru na kuipongeza Serikali kwa mpango wake unaoendelea sasa hivi wa kujenga barabara zetu hizi kwa kutumia fedha za ndani. Tumeshapata daraja, sasa tunategemea barabara za Lindi - Kibiti, zitamalizwa na hii barabara ya kwenda Shelui - Singida, itamalizwa na nchi hii sasa itasonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii vile vile kuishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kutoa ruzuku kwa pembejeo katika maeneo yale ambayo yanalima mahindi, kwa sababu hii itatuhakikishia kupata chakula kwa wingi. Lakini nataka niungane na wote ambao wamekwishasema kabla ya mimi, kwamba Serikali ishauriwe na iona na ichukue ushauri huu kwamba iangarie upya msimamo wake wa

kupandisha kodi katika vyandarua na dawa za mbu. Tunajua tuna viwanda hapa, lakini kabla hatujawa na hakika kwamba uwezo wa viwanda hivi siyo tu kuzalisha, lakini pia kusambaza vyandarua hivi na dawa za mbu vinawafikia wananchi wote ambao wanavihitaji, basi kwa sasa hivi tuendelee na utaratibu ambao unatuwezesha sisi kuhakikisha kwamba vyandarua na dawa za mbu vyote vinapati kana bila uzito mkubwa huu ulioongezwa sasa hivi kwa kodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nahofia nitagongewa kengele ya pili. Lakini nataka kusisitiza kwamba umuhimu kwa Tanzania kuangalia upya mikataba tuliyonayo katika Sekta ya Madini. Nasisitiza kwamba madini haya ni yetu, madini siyo ya wachimbaji, utaratibu uwekwe ambao utazingatia dhana ya sisi kuwa na madini haya, yanayochimbwa ni madini yetu, kinachotoka ni chetu, wale wajilipe kwa sababu ya ufundi, utaalalm, mtaji pamoja na ile teknolojia ambayo wameileta. Jeuri hii ambayo wanaonyesha wenzetu wa Botswana na wenzetu Waarabu, mimi nina hakika kabisa wale wasingekuwa nao kama wangkuwa wanatumia utaratibu wa kupata mrabaha wa asilimia 3 na labda wananchi kuajiriwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hizi mbili mia kwa mia. (*Makofî*)

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba samahani kwa kuvuruga utaratibu, nimechelewa kidogo kwa sababu sijisikii vizuri. Lakini nashukuru pia kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi pia nichukue nafasi hii niweze kuwapongeza wale Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamejiunga nasi katika Bunge hili. Mimi nawatakia kheri nikitegemea kwamba tutashirikiana vizuri katika kuwashudumia wananchi. Nawapongeza sana na karibuni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kuchukua nafasi hii niweze kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri ambazo wameziwasilisha mbele yetu na ambazo zina picha nzuri na matumaini. Baada ya kuwapongeza kabla sijasahau niunge mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa labda nichangie kidogo katika maeneo mawili, matatu, kama ambavyo wenzangu wamepata nafasi ya kuchangia.

Kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali kwa vile inaendelea kuweka malengo ya mipango na kutoa motisha kwa wananchi ili kutumia nguvu kazi kuijendeleza na kuleta maendeleo endelevu kwao wao binafsi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri na vile vile kwa vile Serikali sasa imewe ka kipaumbele kwenye nyanja mbalimbali kama vile kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nichangie upande wa kilimo mambo yale ambayo yamezingatiwa kwa mfano, katika Ibara ya 34 ukurasa wa 28 mpaka 31. Pale ambapo Mheshimiwa Waziri alizungumzia kwamba Wilaya zipendekeze zao moja la chakula na zao moja la biashara, mimi naomba labda nitoe rai kwamba hili wazo ni zuri, kwa kuwa Serikali inataka kuweka msukumo maalum ili kibajeti iweze kuhakikisha kwamba kila Wilaya inapata zao lake la chakula na la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nafikiri katika kufanya hili lazima tuweke tahadhari kwa sababu kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia ni kwamba kweli katika Wilaya nyingine unakuta kuna maeneo mengine kuna mazao ambayo yanastawi zaidi kuliko upande mwengine wa Wilaya ile na hii wakati mwengine inajitokeza kwamba kuna aina ya makabila fulani katika Wilaya ile ile au aina ya ukanda fulani ambao wanapanda mazao yale tofauti na Wilaya nyingine.

Kwa hiyo, hapa ni lazima tuwe waangalifu tutakapokuwa tunachagua mazao ya kulima isije ikaonekana kwamba tunapendelea upande mmoja katika yale maamuzi tutakayofanya kiwilaya. Kwa mfano, ukichukulia Wilaya ambazo ziko katika nyanda za Pwani, unakuta wengi sana wanaokaa upande wa Pwani inawezekana wakawa ni kabilia fulani au ni dini fulani, sasa watakavyoambiwa labda upande huu mwengine wanalima zao la Kipwani na wengine zao la Bara, sasa hapo mimi nadhani italeta mtafaruku. Kwa hiyo, ni lazima tuchukue tahadhari ili tusiweze kuleta ubaguzi fulani. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu napenda kuipongeza Serikali vile vile kwa kutoa ruzuku kwa ile Mikoa minne ambayo inazalisha sana zao la mahindi, Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma.

Lakini vile vile napenda tufahamishwe kwamba hii ruzuku itakuwa endelevu, kila wakati watakuwa wanapata na itachukua muda gani na mikoa gani mingine labda inaweza ikasaidiwa. Kwa sababu iko mikoa mingine ambayo pia ina matatizo nafikiri pia inahitaji kusaidiwa. Kwa hiyo, ningependekeza pia na mimi kuwaunga mkono wenzangu kwamba hata ile mikoa mingine basi baadaye Bajeti inavyoruhusu na wenyewe pia wasaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuipongeza Serikali kwa kweli ni upande wa kodi ya maendeleo. Naipongeza sana Serikali kwa kuondoa hii kodi ya maendeleo na kweli kabisa ilikuwa ni kero na usumbufu mkubwa. Najua kabisa hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu hapo mwanzo pia kulikuwa na kero ile ya ada, watoto walikuwa wanalipa ada, wazazi tulikuwa tunapata taabu lakin kutokana na sera safi za Chama cha Mapinduzi iliondoa ile ada, kwa hiyo, ni mojawapo ya kero iliyoiiondoa. Pia ndiyo kero walivotoa kwenye kodi nadhani pia tunaendeleza sera yetu ya Chama cha Mapinduzi na mimi naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana kwa sababu kodi ya maendeleo kwa kweli ilikuwa inatesa sana hasa akinamama. Unakuta waume zao wanakimbia majumbani inapofikia wakati wa msako, wanaume wale wanalala porini akinamama

wanabaki peke yao na watoto kwa kweli ilikuwa inawapa kero. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kuwa imetuondolea kero kubwa sana kule majimboni kwetu. Lakini pia naomba nipongeze kwa kutoa ule ushuru amba o ulikuwa unaitwa kero mbaya. Kwa mfano, ushuru wa wale wakulima wanapopeleka bidhaa zao katika masoko. Hii tulikuwa tunaiona kwamba walikuwa wanaumia wengi ni wanawake kwa sababu akinamama wakitoka mashambani kwao walikuwa wakileta bidhaa ndogo ndogo wakifika katika masoko walikuwa wanatozwa ushuru mdogo mdogo amba o kwa kweli kipato chao ni kidogo wanatembea sehemu kubwa lakini vile vile ilibidi walipie ushuru huu mdogo amba o ulikuwa unakera. Kwa hiyo, pia mimi naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningezungumzia kidogo suala la viwango vya ushuru ambavyo vingine vimepunguzwa, vimeondolewa na vingine vimeongezwa. Ibara ya 51, ukurasa 53 hadi 54 naomba na mimi nizungumzie suala hili la ushuru wa vyandarua na dawa za mbu za kuchoma amba o umepanda hadi kufikia asilimia 10. Kama tunavyofahamu sasa hivi kuna programu ya kupiga vita Malaria, kwa sababu Malaria kabisa inaleta vifo vingi hasa kwa watoto wadogo na akinamama wajawazito. Inapokuwa tunapandisha bei, nafahamu nia ya Serikali ni kwamba kudhibiti uingizaji wa vile vyandarua vinavyotoka nje. Lakini tujiulize swali, je sisi tunapokuwa kule vijijini tunaona tunaponunua vyandarua ni nani mwana kijiji anajua kwamba hiki ni chandarua cha kutoka nje au cha kutoka ndani na ile bei inayouzwa pale yule muuzaji pale kijijini anatofautishaje bei ya chandarua kinachotoka nje na cha ndani.

Mimi naona kwa kweli mwananchi anaumia. Kwa sababu wote bei ikifika *irrespective* kwamba ye ye amenunua kwa bei kubwa kile chandarua kinachotoka nje, lakini ikifika kwenye soko unakuta huyu mwananchi wa chini kabisa ye ye ananunua kwa bei ile ile. Kwa hiyo, kwa kweli mimi ningombia niungane na wenzangu kwamba tuisaidie basi Serikali hasa Wizara ya Afya na programu nyingine kuweza kupunguza tatizo la maralia ambalo linua watu wengi sana. (*Makofsi*)

Katika hotuba ya Mipango napenda kuipongeza Serikali kwa kugusa katika sekta ya elimu. Kama ilivyosema ni kwamba maeneo mengi Shule za Msingi kwa programu ya *MMEM* ni kweli kabisa kwamba majengo yameongezeka, uandikishaji wa watoto umepanda, asilimia kubwa ya watoto wa kike wanaojiunga kwenda Kidato cha Tano, halafu vile vile Serikali na yenyewe pia imechangia katika kuwasomesha watoto amba o wazazi wao wameshindwa na wana uwezo mdogo. Mimi naona tungeshauri katika Bajeti ya Waheshimiwa Mawaziri mliviyopanga tujaribu pia kuandaa programu ambayo itasaidia hii Elimu ya Sekondari kwa sababu katika hotuba hii imetaja Elimu ya Msingi halafu ikarukia kwenye Vyuo vya Ufundu na Vyuo vya Juu. Sasa itakuwaje imuandae mtoto vizuri katika Elimu ya Msingi hapo hapo katikati unamuacha kidogo halafu unakwenda kuviiimarisha vile vyuo. Kwa hiyo, ningombia pia kuwe na programu ambayo Serikali itashughulikia Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa afya, naipongeza vile vile Serikali kwamba imeweka mikakati na mipango ya kuendeleza sekta ya afya katika kuboresha huduma za mwananchi. Hii ni pamoja ya kukarabati vituo, upatikanaji wa urahisi wa huduma na

tiba, lakini vile vile tungeomba basi kama Wizara ya Afya itakapofikia kuzungumzia basi isiwe kuboresha tu majengo na vitendea kazi na kadhalika lakini vile vile wakarabati hata hawa watumishi ambao wanakwenda kufanya ile kazi ili kuweza kutoa huduma nzuri.

Mwisho kabisa nigosie kidogo Wizara ya Viwanda na Biashara hususan nikogosia viwanda vidogo vidogo. Naipongeza Serikali kwamba inaendelea kuona umuhimu wa kuweka viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati (*Small Medium Enterprises*). Ni kweli kabisa kwamba vinatusaidia akinamama hasa wale ambao wana biashara zao ndogo ndogo wanasaidiwa, lakini tungeomba vile vile pamoja na kusaidia basi hii elimu ambayo wale wataalamu kutoka viwanda vidogo vidogo ifike kule kwa wananchi hasa vijijini. Kwa sababu unakuta ghamama wanayoitoa akinamama kuchangia hasa kwenye upande wa *food processing* unakuta kwamba ghamama ni kubwa sana kiasi kwamba wale wana vikundi wanashindwa kule kuchangia ili waweze kupata ule utaalamu. Kwa hiyo, Serikali itazame ili ione itakapokuwa viwanda vidogo inapeleka kule huduma basi ikibidi hata kuwaondoshea ule mchango wanaotakiwa wautoe kabla hata hawajapata ile elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niseme nawapongeza sana na nawatakia kila la kheri na vile vile naunga mkono tena hoja zote mbili asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi mbili, hoja ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji.

Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha, kwa kazi nzuri aliyoifanya na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa kazi nzuri tu aliyoionyesha hapa ya kuweza kubainisha na kuweza kutuletea Bajeti au maelezo mazuri yanayojali watu. Kitendo hicho cha kuweza kujali watu basi kinapokelewa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu. Hilo linaleweka katika sehemu zote unapozunguka hadi katika maeneo mbalimbali. Kama ukiona unakubalika kwa watu basi unajua kwamba kuna Mwenyezi Mungu karibu. (*Makofi*)

Pili, ningependa kuwashukuru tu Waheshimiwa Wabunge wote na kuwapa pongezi walioingia katika Bunge kuja kujumuika na sisi katika suala zima la kuwakilisha wananchi katika masuala yao mbalimbali, sitawenza kutofautisha kati ya chama na chama uwakilishi, lakini nawapa pongezi sana. (*Makofi*)

Tatu, napenda kutoa pongezi kwa viongozi waliochaguliwa wapya wa *TRA*, Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga, ni kazi ngumu ambayo wamepewa na ni kazi ambayo itaonyesha dira na nafikiri sasa hivi tunaweza tukaonyesha dira na tukasema na kuonyesha kwamba Bajeti hii ni nzuri, Bajeti ina mwelekeo lakini kutoekana na *TRA* hasa kwa viongozi walioanza, Ndugu yangu mzee wangu Mzee Sanare, nafikiri ndiye aliyeanzisha haya mambo ya *TRA* kwa mwanzo kabisa amefanya kazi kubwa na sasa hivi tunaiendeleza. (*Makofi*)

Tanzania tukikumbuka hatukuwa na fedha kabisa katika mfuko wa Serikali lakini baada ya kuanza kwa *TRA* tumeweza kupata fedha nyingi na sasa hivi tunaweza kujivunia na Mawaziri wetu wakazigawa na wakabajeti zikaonekana kwamba tuna fedha katika mfuko wa Serikali. Lakini kubwa ningeweza kutoa pongezi kwa Manaibu Waziri ambao ni watendaji wakuu kabisa katika Mawizara yote na ambao kila kitu wanabebeshwa wao na ndio wanaobeba mizigo kwa kweli nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Lakini isitoshe katika Bajeti hii ningependa kutoa shukrani za pekee kwa Wahasibu wote kwa sababu kazi ya Uhasibu ni kazi ambayo kila mtu anaidharau, ni kazi ambayo anaiona kila mtu kwamba unapokuwa Mhasibu wanakuita kwamba unakuwa ni mwizi, kumbe ni kazi ya ukuli kama uko Bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Uhasibu katika Wizara yoyote unakuta kwamba Mhasibu anafanya kazi saa zote na Mhasibu ukimwona amenenepa basi itakuwa ni balaa, wote ni wembamba tu. Kwa kweli nawapongeza sana kwa kazi wanayofanya na nawapa pole kwa kazi ngumu wanayofanya ambayo nafikiri hata Serikali haiwatambui kwa undani zaidi kwa kupitia sasa hivi nilikuwa naomba tu Waziri anayehusika hasa katika utumishi basi waweze kubadilisha hata ikama yao angalau wafikiriwe kupandishwa mishahara yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza shukrani hizo nafikiri mimi nianze kuangalia ni sehemu gani, Serikali imejaribu angalau kutuletea unafuu katika Majimbo yetu. Kwanza kabisa, ningependa nielekeze katika uondoaji wa kodi ya maendeleo. Kodi ya maendeleo ilikuwa ni kero katika maeneo yote, sehemu zote ulipokuwa unakwenda wananchi walikuwa wanalamika kuhusu kodi ya maendeleo.

Bahati nzuri wenzetu wa Dar es Salaam, wananchi wengi walikuwa hawalipi kodi ya maendeleo. Sasa hata ukiwaambia kodi ya maendeleo hawaioni kama kuna umuhimu. Lakini ukienda vijiji ambapo kuna Watendaji wa Vijiji au Watendaji wa Kata ambao wako karibu na wananchi wale walikuwa ndio wanalionka kama ndio Pato lao la kuweza kujinufaisha kwa sababu wengi walikuwa hawafikishi kodi ile katika Halmashauri husika.

Kwa hiyo, nyingi zilikuwa zinaingia mifukoni mwao. Kwa kweli wananchi katika vijiji wamefurahi sana kutokana na kuondolewa kwa kodi hii. Kwa kufurahishwa kwa watu wengi kama nilivyosema mwanzoni basi Bajeti hii ina mwelekeo mzuri wa kuweza kulipeleka Taifa hili katika mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kulizungumzia tu na ni kubwa kabisa ni kuhusu suala la madini. Ndugu zangu nafikiri maeneo ya madini wengi wanaposema kwamba Wilaya hii ina madini basi wanajua Wilaya ile ni tajiri hasa ukiangalia kwamba kuna Wilaya ya Kahama, Geita, Simanjiro, Shinyanga Vijiji na maeneo mengine yote hayo wote wanajua kabisa kwamba wale ni watu matajiri kumbe kuna dhana tofauti, watu wanafikiria dhana tofauti.

Kuna umaskini wa kupindukia kuliko sehemu zingine zozote. Matajiri ni wale wanaokuja tu. Nafikiri hata jana hapa Mheshimiwa Oscar Mloka, alibainisha wazi akasema kwamba baada ya kupatikana machimbo katika maeneo yake vijana wote waliokuwa mjini waliokuwa wanazurura basi walikimbilia kule. Lakini kukimbilia kule sio kwamba wanakwenda kutajirika, kule wanakwenda kuzoa umaskini wa kutosha. Sasa unakuta kuna mambo mengi yanayoweza yakajitokeza kule. Kuna mambo ya magonjwa, mambo ya kutopata ajira, mambo ya kubadilisha tabia mbalimbali, sasa yote haya wanaona kwamba wawekezaji wameshakuja katika maeneo yetu wamepata neema kumbe wamepata matatizo.

Sasa ndugu zangu nilitaka kuwaambia tu kwamba suala la madini katika maeneo mbalimbali tumelipokea Tanzania kwa hisia tofauti kabisa. Ndiyo maana tulitegemea kwamba tutapata utajiri, lakini badala yake tumewaweka wananchi wetu katika hali ya umaskini wa kupindukia. Kwa kuuangalia umaskini huu na kwa kuangalia ni jinsi gani namna tutakavyouokoa basi mikataba tuliyordhia wakati ule yote nafikiri tuifute na tuiweke wazi au tuweze kufunga mikataba mingine mipy. Mikataba ipo na wamesema na wamesema kwamba ni siri, siri gani ambayo inaweza ikafanywa na watu wachache na wengine wasijue. Mkataba wa *Geita Gold Mine* bahati nzuri nimeupata, ule mkataba kwa kweli unatuua. Zamani nilikuwa nagombana sana na wawekezaji *Geita Gold Mine*, sasa hivi nimeshawaacha nimeona wana haki hata kama ningkuwa mimi katika kutafuta fedha ile, basi mimi nisingeweza hata kutoa senti moja katika Serikali. Mkataba upo wazi, unawaruhusu wafanye lolote. Sisi viongozi au Wabunge wa maeneo yale tunakuwa ombaomba. Anaweza akakubali au akakataa. Sasa ndugu zangu, kwa kweli mikataba hii haifai kabisa. Mkataba nimeshaupata huo sasa kama Serikali imesema kwamba ni siri basi sisi tumeupata. Sasa tutaona je Serikali itafanya nini. Kama itabidi basi tuutawanye kwa wengine na wenyewe wauone mimi sasa hivi bado nauona kama siri. Je, Serikali itakubali tubadilishe hii mikataba kwa sababu inatuua sisi wananchi katika maeneo yale.

Sasa ndugu zangu, mimi nilikuwa naomba tu kwa mfano baada ya kuja wawekezaji Wilaya ya Geita, kuna watu waliowapisha maeneo yale. Walipowapisha mpaka leo hii hawajalipwa fidia yao, wananchi kama hao wanafikiria nini. Tunasema kwamba Bajeti hii inaondoa kero kwa wananchi, hii sio kero. Nilikuwa namwomba Waziri nimeona katika ukurasa wake wa 78 kuna fedha za dharura zile shilingi bilioni 8.6 basi naomba zile shilingi 600,000 zote zichukuliwe wakalipwe wananchi wa Geita ambao wanadai fidia yao kwa kuupisha ule mgodi. Sasa nafikiri Waziri anaweza akanijibu hilo wakati akijumuisha katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi ambalo nilikuwa nalionta tu katika maeneo yale kumekuwa na matatizo mengi katika maeneo yote ya madini. Matatizo yamekuwa ni mengi mno kiasi ambacho hawa wawekezaji kwa kweli wameamua kuwa na ubaguzi wa hali ya juu. Kumekuwa na ubaguzi katika ajira, kumekuwa na ubaguzi hata katika uwekaji wa fedha zao. Fedha nyingi walizonazo wao mpaka sasa akaunti zao ziko nchi za nje. Sasa kama ni kujenga uchumi kwa nini wasifungue akaunti zao zikawa hapa Tanzania. Wakaweka hapa Benki Kuu, wakitaka kununua bidhaa *Foreign Currency* inakuwa pale Benki Kuu basi wanunuua bidhaa kupitia Benki Kuu.

Kwa hiyo, unakuta kwamba hata Serikali itakuwa inafaidika kwa njia moja nyingine kufuatana na zile *transactions*. Lakini sasa hivi unakuta mishahara yao iko nje, kila kitu kiko nje hata wakitaka kuagiza matunda, wanaagiza kutoka nje, wakitaka kuagiza chochote kile kinatoka nje, sasa Tanzania tunafaidika nini. Kwa hiyo, unakuta kwamba hata ajira sana sana tunayoipata sisi labda kuendesha hayo ma-*caterpillar*, ma-*bulldozer* na kufyekafyeka nyasi, lakini hata hivyo unakuta mwangalizi wa pale ni mtu kutoka nje. Ndugu zangu, nilikuwa naomba kabisa muielewe dhana ya kwamba sehemu ya madini ni watu maskini wa kupindukia na naiomba Wizara au Serikali ijaribu kuangalia maeneo yale, kuweza kuiangalia au kuiwekea miundombinu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukiangalia mikoa yote yenye madini hakuna miundombinu, watu wanakwenda ovyo tu. Unakuta watu wengi wamefukuzwa kwenye maeneo yao. Wachimbaji wadogo wadogo ambao wanaweza wakagundua katika maeneo basi wanawekwa wachimbaji wakubwa wakubwa, kwa hiyo hawa wanakosa kupata hata soko. Kwa hiyo, unakuta kwamba katika maeneo yale umaskini umekithiri na ni mkubwa sana. Naiomba Serikali iangalie pamoa na Bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja ambacho ni cha mwisho nataka kuzungumza kwamba ni sehemu gani nyingine ambayo tunaweza tukapata angalau fedha kidogo ya kuweza kuziba mapengo haya. Nilipokuwa naangalia na kuzunguka nikaona kwamba kuna Kitengo kimoja kimeanzishwa nje ya nchi kinakagua magari. Gari linapotaka kuingia humu lazima likaguliwe kutoka nje na Kampuni ziko kule nje zinakagua. Kwa nini tuanzishe Kampuni nje tusije tukayakagua magari hapa nyumbani na fedha ikaingia hapa hapa nyumbani. Tunamlipa mtu wa nje ambaye hana faida na sisi je, kuna nini huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, huenda ikawa mimi katika akili yangu labda ni ndogo labda sielewi, lakini najua kabisa kwamba hapo kutakuwa na kitu fulani. Huenda ikawa kuna mtu ambaye ameidanganya Serikali akaweka Kampuni yake kule, lakini na yeye labda huenda tunaye huku akawa anachukua kidogo kidogo kule, si Kampuni ambayo kwa kweli tumeiweka kwa utaratibu ambao na sisi Watanzania tumeukubali. Nilikuwa naomba kabisa *Tanzania Bureau of Standard* inaweza ikaangalia viwango, je, hili gari linafaa, au hili gari halifai. Katika kuangalia hilo na ukiangalia gari ngapi zinaingia Tanzania, ukiingiza moja moja kwa dola ya 150 kila gari nafikiri tunaweza tukapata fedha nyingi mno kuliko ambavyo tunaziacha huko nje hatumjui ni nani tunayemnufaisha na ni nani analeta kitu gani katika Serikali yetu. Sana sana tunapata kitu kidogo tu ambacho labda tunaongeza kodi kubwa katika magari yetu unakuta hata watu wa uwezo wa chini wanashindwa hata kununua magari kwa sababu ya kodi ambazo zinaongezwa kutoka huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisizungumze mpaka nikagongewa kengele, lakini nilikuwa naomba tu kwamba yote niliyoyaongea hasa la fidia la wananchi wangu wa Geita lifikiriwe kutoka katika mfuko ule wa *contingency fund* ambayo imewekwa ya shilingi bilioni 8.6 wamegewe pale tusiangalie kwamba walilipwa na nani, tuangalie hawa wananchi tuwaondolee kero. Tangu mwaka 1999 mpake leo wengine wanakuwa hawajui Serikali yao itawalipa nini. Sasa nilikuwa naomba tu kwa sababu vifedha hivi

nimeviona na huwezi ukasema kwamba havipo na ni vya dharura na vile kama ni vya dharura nilikuwa naomba walipwe hawa wananchi ili na wao waweze kufaidi matunda ya Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naunga hoja mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Bajeti kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia nimpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango na Ubinafshajji, Manaibu wao wote wawili, Makatibu wao Wakuu wote, Makamishna wote, Wakurugenzi kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti hii nzuri kabisa ambayo yenye mwelekeo mzuri sana wa Chama cha Mapinduzi na pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wale waliofuzu katika chaguzi ndogo ndogo hizi kuingia Bungeni, nasema ahsante sana na karibuni kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaanza kupongeza Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano kifungu cha 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Nalipongeza sana suala hili kwa muda mrefu sana tulikuwa tumelizungumza humu ndani ya Bunge na wananchi wote takriban walikuwa wanaizungumza sana kuhusu Tume hii kwa hivyo nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, kuiteua Tume hiyo na kuipa nafasi na kuanza kazi yake mara moja, nasema hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti inasema hivi na imetenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada *Programme Assistance* ya nje kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hii ni kwa mujibu wa muafaka uliokwisha kubaliwa huko nyuma na matumaini ya Serikali kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano ambayo imeshaundwa itashauri Serikali zetu kuhusu utaratibu wa kudumu wa kugawa mapato ya Muungano. Hapa mimi ninapapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika hali ngumu sana ya kiuchumi. Hii ndiyo maana manung'uniko mengi ambayo yanajitokeza kutokana na ukwasi na unyonge wa wananchi wake. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetegemea sana uchumi wake ni karafuu na hali ya karafuu ni mbaya sana kimasoko ya dunia. Uchumi wa pili ilikuwa ni nazi ambaeo pia hazifahamiki. Hivi sasa uchumi unaotegemewa sana ni utalii na utalii pia una matatizo yake. Tume hii ya Pamoja asilimia 4.5 ni moja katika afueni kubwa ambayo itaweza kuiletea manufaa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mimi nasema hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunasema ni nchi moja. Lakini ukiangalia kiuchumi Serikali ya Jamhuri ya Muungano uchumi wake umekwenda kimapani sana ukilinganisha na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utaona kwamba hatua ya maendeleo tunapishana

kwa *gap* kubwa sana. Sasa hili la kuzingatia na kuiangalia Serikali ya Mapinduzi hali iliyokuwa nayo na upungufu wa uchumi wao ulivyokuwa nao.

Sasa Tume hii ningeiomba sana ifanye kazi vizuri kwa uangalifu, kwa busara na hali na mali kuhakikisha kwamba shughuli hii ya ugawaji wa fedha hizi inafanyika kwa uangalifu sana. Manung'uniko sasa hivi naamini ni moja katika kero ya Muungano ilikuwa ni hili. Hii ni hatua kubwa sana ambayo kero hii imekuwa imepungua sana. Kwa hiyo, nasema tena naipongeza sana Serikali.

Suala la pili, nitapenda kuipongeza Serikali kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu kutoka hapo walipo na kufika shilingi 20,000. Mheshimiwa Waziri hongera sana, kweli wastaafu wetu wamefanya kazi kwa muda mrefu, waliisaidia nchi hii kwa nguvu zao zote, ukweli kitendo cha kuongeza pensheni kufikia shilingi 20,000 ni kitendo cha uzalendo na kuapenda wananchi wake. Nasema hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja ambacho tungeliomba Serikali ikizingatie pensheni kwa mujibu wa mkataba ukishaacha kazi ulipwe mafao yako na ulipwe pensheni yako mpaka kufa. Lakini kuna baadhi ambaao waliochukua ile kitu kwa mkupuo na kwa mujibu wa mikataba wamekubaliana wataishi kiwango cha muda wa miaka 12 na nusu kama sikosei, lakini mkataba ule anaujua Mungu tu sisi hatuelewi na bado wanaishi. Fedha zile ambaao wamezichukua zimekwisha na wao wapo wanaitumikia nchi hii na kulijenga Taifa lao. Ninaionba Serikali ilizingatie suala hili na ilette Muswada Bungeni kurekebisha hali hii ili na wao wafaidike na jukumu hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa ni wengi nao wana maneno si mazuri, ni haki yao kwa sababu ya unyonge. Wamefanya kazi hii kwa hali na mali, wameisaidia nchi hii kwa hali na mali, wamefanya kwa nguvu zao zote mpaka wamezeeka, lakini kile ambacho wamekichukua kwa mkupuo kimekwisha. Kitu cha mkupuo kimesaidia kwa mipango yao kimekwisha, fedha zile sasa hivi hawana, wanahangaika sana. Ninaionba sana Serikali ilitizame jambo hili kwa jicho la huruma. Licha ya kuongeza hizi Sh. 20,000/=, lakini na hawa nao tuwasogeze kuwaingiza sehemu ili na wao wapate chochote kwa kila mwezi cha kujikimu maisha yao na kuweza kulijenga Taifa hili kwa heri na amani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo napenda kuzungumza ni kuhusu ajira kwa vijana. Tuna wimbi kubwa sana la vijana hapa nchini Tanzania ambaao hawana kazi na walishamaliza shule, lakini la kufanya hawana! Ninaionba Serikali tusiwaache vijana hawa kwa kuwa eti hatuna nafasi za kazi. Kweli Serikali haina uwezo wa kuwapa nafasi za kazi wote ambaao wamemaliza shule, lakini naomba uandaliwe utaratibu maalum kwa vijana hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna hii Mifuko ya Akinamama na Vijana, lakini utaratibu wake bado siyo mzuri, urasimu ni mkubwa. Tupunguze huu urasimu, vijana wajikusanye, tuwape fedha wafanye kazi/wajajiri. Kwa kuwa nafasi za kuajiriwa

katika kazi hazipo, basi angalau tuwape nafuu ili wasipate tabu ya kupata mifuko hii. Haidhuru mifuko hii ipo, lakini hata kupata fedha za kujajiri katika shughuli zao za maendeleo ni ngumu sana. Ninaiomba Serikali kabisa itazame utaratibu huu na iweke nafuu kabisa ili vijana hawa wakawa wanapata mfuko huu bila matatizo na wao wajisikie kwamba wako katika nchi yao na kujenga Taifa hili. Najua kwamba vijana ndiyo Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu nguvu kazi. Kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi, hiyo ndiyo kujikwamua kiuchumi, huko ndiyo kuondokana na umaskini. Watanzania wengi amba wana nguvu ya kufanya kazi, hawafanyi kazi, hiyo ni lazima tukubali! Ninaiomba Serikali, iandae sera maalum kuhusu suala la nguvu kazi ya kuhakikisha kwamba kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi na ikiwa hakufanya ashtakiwe kwa mujibu wa sheria. Hii itatusaidia sana katika kujikwamua na hali ngumu ya kiuchumi na itatukwamua sana katika kuleta maendeleo yetu kwenye maeneo yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuandae sera maalum ya nguvukazi ambayo kila mtu ambaye hataweza kutekeleza wajibu wake, hataweza kufanya kazi zake na ana nguvu, basi sheria ichukue mkondo wake na imtie hatiani kwa mujibu wa sheria hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kuzungumza ni namna ya kuondoa umaskini. Hii lugha tunaizungumza sana, kuondoa umaskini, kuondoa umaskini. Je, tukisema kuondoa umaskini tunamaanisha nini? Kuondoa umaskini ni kufanya kazi. Wanasema kwamba mtu unajiondoa wewe mwenyewe katika umaskini. Utaratibu wa mikopo uwekwe vizuri katika kuhakikisha kwamba mtu anajiondoa katika umaskini na hasa ninazungumzia *NGO's*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *NGOs* tulizonazo zitatekeleza wajibu wake ipasavyo, naamini kwamba matatizo mengi ya Wananchi wanyonge hasa hawa akinamama na vijana wangeondokana na umaskini, lakini sijui Serikali imeweka utaratibu gani kuhusu kusimamia *NGOs* hizi na kutekeleza wajibu wake wa kuwaondosha katika tatizo hili la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba *NGOs* hizi tuziangalie. *NGOs* nyingi tulizonazo nyingine zinafanya kazi vizuri ni lazima tuzisifu. Lakini kuna nyingine ni *NGOs* za mifukoni, zimepitwa na wakati hazitusaidii katika nchi hii kwenye kuleta maendeleo. Ninashauri hizi *NGOs* ziangaliwe vizuri na zile ambazo hazitusaidii tuachane nazo, lakini tuzipe zile ambazo zinafanya kazi, zifanye kazi ziisaidie nchi hii kwa manufaa ya Wananchi wetu kwa kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, kabla kengele ya pili kugonga , mimi binafsi sipendi hilo, nasema kwamba naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hizi mbili za bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi uliopita na kuingia Bungeni. Ninawakaribisha sana ili tuweze kusaidiana kusimamia na kuchambua mambo mbalimbali ya Serikali badala ya kuchambuana sisi wenyewe kwa wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niwapongeze sana Mawaziri wawili; Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Pesambilii Mramba, kwa bajeti ambayo wameiandaa mwaka huu. Bajeti hii imelenga kuondoa kero za Wananchi na sisi sote ni mashahidi. Wananchi wameipokea vizuri na wameisifu kwa sababu muda mrefu walikuwa wakilalamikia kero mbalimbali, pia, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakilalamikia kero mbalimbali na bahati nzuri bajeti hii imesaidia kuzipunguza na kama si kuzimaliza kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naomba niipongeze bajeti hii kwanza kwa kufuta kodi ya maendeleo, kufuta kodi ya ushuru wa balskeli na mbogamboga. Vitu hivi vilikuwa ni kero kubwa kwa Wananchi. Suala la kodi ya maendeleo lilikuwa linaleta hatari, Wananchi wengi walikuwa wanaishi huko vijijini kwa wasiwasi. Vile vile, watendaji walikuwa wanapata shida wakati mwingine hata kupambana na kupigwa na Wananchi baada ya kero hizi kuzidi. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali kwa haya ambayo wameyaona kwamba ni kero na wakayaondoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nipongeze kwa kuongeza kima cha pensheni. Sasa hivi wastaafu nao wameishukuru Serikali, lakini wanachoomba ni kuona baada ya kima cha chini kutajwa je, vima vingine vyâ juu nyongeza yake itakuwaje? Labda hili nalo lingefafanuliwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wastaafu wale amba waliafa kabla ya muda, ni kweli sheria ilipitishwa kusitisha pensheni zao, lakini bado na wenyewe wanailalamikia Serikali kwamba waliafishwa kazi na Serikali na hawakuwa tayari kuacha kazi katika muda huo. Naomba Serikali iangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Sspika, ni mambo mengi sana ambayo yamefanywa na Serikali hii kupunguza kero mbalimbali, lakini sasa napenda nijielekeze katika suala la kuondoa umaskini. Katika suala hili niishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha kilimo. Sisi sote ni mashahidi, kilimo kikisimamiwa vizuri na kila mmoja akatimiza wajibu wake, kwa wale amba wanaweza kulima wakalima nina uhakika maisha ya Wananchi wetu vijijini yataboreka.

Mheshimiwa Spika, Ninaishauri Serikali kwamba, ili kusimamia vizuri suala la kilimo watumishi wa Wizara hii ya Kilimo na Chakula waongezwe ili kuweza kusimamia vizuri hasa huko vijijini. Kwa sababu pengine unakuta mtumishi mmoja wa Idara ya Kilimo ana vijiji labda vitano/sita au tarafa nzima, kwa hiyo unakuta kwamba usimamizi wake si mzuri sana na wakati mwingine hawana hata usafiri! Suala hili likiboreshwa wakaajiriwa watumishi, wakapewa vijiji vichache nina uhakika wanaweza wakasimamia vizuri zaidi na hasa wakipatiwa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kilimo nizungumzie kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Suala hili ni ufumbuzi wa kudumu kwa sababu itakuwa hakuna muda, ni wakati wote ni kulima na kubadilisha mazao kwa kiangazi na masika. Ningombi Serikali iliangalie suala la kilimo cha umwagiliaji na iweze kuwasaidia Wananchi hasa katika suala la kuwatafutia zana mbalimbali na kwa sisi wa Mkoa wa Dodoma hasa kuimarisha uchimbaji wa mabwawa ambayo yatatusaidia sana katika kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naomba nizungumzie kuhusu biashara ndogondogo. Suala hili nalo ni muhimu na napenda kuishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwakopesha vijana na akinamama kwa sababu ndiyo wanaoshughulika na biashara hii. Biashara hii inawasaidia akinamama kuwapatia kipato na ndiyo inawawezesha kupata mahitaji yao ya kila siku na hata kusomesha watoto na mambo mengine.

Kinachokera hapa katika biashara hizi za akinamama na vijana ni kukosa sehemu maalum za kufanya biashara zao hasa katika maeneo ya Mjini. Bahati mbaya wafanyabiashara hawa wanapoona mikusanyiko ya watu kwa mfano *stand*, hapo ndiyo anaona soko lake ni zuri.

Utakuta pengine mama ana chakula chake na sahani zake anawaandaa watu waweze kununua na kula pale, ye ye anapata pesa yake. Lakini inasikitisha sana unapokuta Serikali inapambana na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, kitu ambacho kwa kweli kinawavurugia biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukiangalia akinamama wakati mwingine biashara anayoifanya mchele kakopa, sufuria anazopikia kakopa, kila kitu kakopa anategemea akiiza aende akalipe! Badala ya kulipa vitu anavyokopa Serikali inakusanya vyombo vyake, inachukua chakula chake, matokeo yake anabaki na deni ambalo hana uhakika na mahali ambapo atapata tena pesa ya kuanza biashara ile. (*Makofi*)

Mheshimwia Naibu Spika, naishauri Serikali kwamba, badala ya kuwafukuza fukuza kila siku, ijaribu kuwatengea maeneo ambayo watafanya biashara hizo. Hii itasaidia sana kuliko kukimbizana nao kila kukicha! Kwa mfano, Serikali inaweza kuangalia maeneo ya *stand*, maeneo ya soko na maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ikajenga vibanda ili akinamama na vijana hawa wakakodisha kwa ajili ya kufanya biashara zao. Matokeo yake ni kwamba Serikali itakuwa imepata ushuru wake na wale akinamama na vijana watakuwa wamefaidika na biashara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nizungumzie juu ya suala la Serikali kuhamia Dodoma maana mpaka sasa hatuna uhakika na kinachoendelea. Nakumbuka Serikali ilishasema kwamba Wizara zitahamia Dodoma hatua kwa hatua na kwamba kila mwaka kuna Wizara ambazo zitatengwa kuhamia Dodoma, lakini hadi leo hatujajua ni Wizara gani zitaanza kuhamia mwaka huu na mwaka kesho ni Wizara gani! Kwa sisi wakazi wa Dodoma tunasikitika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoona Serikali inahamia Dodoma, uongo, mbaya maisha ya Wananchi wa Dodoma yanaboreka. Kwa mfano, sasa hivi Bunge linapokuwa Dodoma, kwa kweli Wananchi wa hapa wanafurahi sana na wafanyabiashara wote wanafaidika. Wale wenye mahotelii, wenye guest houses na kadhalika wanafaidika sana. Serikali ikiendelea kuhamia Dodoma, Wananchi wa Dodoma wataboreka kwa mambo mengi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la kuhamia Dodoma, miundombinu ya hapa Mjini iangaliwe vizuri. Mfano barabara na maeneo mengine. Tunaishukuru Serikali kwa sababu baadhi ya barabara zetu zimebekwa lami, lakini kwa sababu sasa hivi kuna wageni wengi wa nje ya nchi wanaokuja katika Mji huu wanakuta umekaa hivi hivi inasikitisha sana. Tunaiomba Serikali iuangalie upya na hasa kufuata *Master Plan* ambayo tayari ipo toka mamlaka ihamishiwe Dodoma. Tunaomba *Master Plan* ile ifuatwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa niendelee kurudia yale ambayo yamezungumzwa na wenzangu. Naomba niishie hapo na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuungana na wenzangu walionitangulia na kutoa pongezi kubwa kwa Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya kutayarisha bajeti hii. Wamefanya kazi nzuri na wametupa kweli mwelekeo ambao unafaa sana hasa kwa sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza maneno mengi, napenda kusema kwamba naunga mkono Hoja hii ya Bajeti kwa asilimia mia moja na pia ile ya Mipango ninaiunga kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna tatizo moja dogo ambalo ningependa kulisema linalohusu speech ya Bajeti aliyoitoa Mheshimiwa Basil Mramba ambayo ipo ukurasa wa 33 na ninaomba kunukuu: “Itakumbukwa kwamba Chombo cha Udhamini wa Hisa za Mashirika ya Umma Yanayobinafsishwa (*Privatisation Trust*) kilianzishwa mwaka 1997.

Chombo hiki kilianzishwa kwa madhumuni ya kudhamini (hold in trust) hisa za Serikali zinazobaki kutoka wenye Mashirika yanayobinafsishwa ili hatimaye hisa hizo zihamishwe kwenye Chombo cha Uwekezaji Pamoja (*Unit Trust*), ili zigawanywe kwa Wananchi wengi. Nia ya uamuhi huu ni kuwezesha Wananchi wengi zaidi hasa wale wa kipato kidogo kushiriki katika ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Muda wa maisha ya Chombo cha Udhamini unakwisha mwezi huu tarehe 15 Juni, 2003. Kwa mujibu wa Sheria ilioanzisha Chombo hiki muda wake ukiisha kinapaswa kujigeuza ili kiwe Chombo cha Uwekezaji wa Pamoja (*Unit Trust of Tanzania*).

Napenda kutoa taarifa kwamba, matayarisho yote ya kuanzisha *Unit Trust of Tanzania* yamekamilika na Chombo hicho kipyä kitaanza kazi tarehe 16 Juni mwaka huu 2003". Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema hadi jana hatuna Chombo cha *Unit Trust of Tanzania* kilichoundwa! Hakuna chombo! Ninayo hati ya Mdhamsini Mkuu wa Serikali ya tarehe 17 ameniandikia ikitaka kufanya *search* ya kutaka kujua juu ya Usajili wa Chombo hicho hapo juu. Napenda kukujulisha rasmi, kwamba hadi kufikia leo hii Chombo hiki bado hakijasajiliwa na ofisi yangu kwa sababu hakimo kwenye kumbukumbu ya ofisi ninayoitunza" mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Bunge, toleo la mwaka huu, Kanuni ya 50 inasema, ninanukuu: "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, kwa sababu hiyo Mbunge ye yote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au kubabaisha tu." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati wa maswali, Naibu Waziri wa Fedha wakati akimjibu Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, alisema na ninamukuu kama walivyomnukuu kwenye gazeti la *Daily News*: "The Unit Trust of Tanzania which replaces the Privatisation Trust has been established under the Trustees Ordinance and will be supervised by the Capital Market and Security Authority."

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya si kweli! Si kweli na juzi tu hapa tumetoa adhabu kali sana kwa Waheshimiwa Wabunge waliolidanganya Bunge na ningependa kupata mwongozo wako kama inawezekana kutoa hoja ya kuwafukuza Mawaziri, Mheshimiwa Basil Mramba na Naibu wake Bungeni kwa kusema uongo Bungeni.

Ningependa kupata utaratibu, kwa sababu jambo hili linaanza kuwa kero Bungeni. Mawaziri wanakuja wanatuambia mambo unayachukua *for granted* kwamba ni mambo ya kweli, lakini kumbe siyo kweli! Binafsi yananipeleka kwenye hali mbaya kabisa maana sijui!

Kwa mfano, kama hayo mengine ambayo siku-*check* kama ni ya kweli, sijui! Binafsi sina tatizo na bajeti, bajeti itapita bila matatizo, lakini suala la muhimu hapa ni kwamba hapa Bungeni ni patakatifu. Hatuwezi kuwa tunasema maneno ya kubabaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wanategemea hiyo dhamana yao ya *Privatisation Trust*. Watu wangu huko Musoma Vijijini ni walala hoi, wameambiwa na Serikali kwamba kuna fedha zimebekwa na wao watapata hisa kwa kupitia kivuli cha *Privatisatin Trust*. Hii *Privatisation Trust* imekwisha muda wake, sasa hizi fedha Shilingi bilioni 12 zinashikiliwa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana *Privatisation Trust* imekufa, kwa mujibu wa Sheria ya *Privatisation Trust*. Chombo cha *Unit Trust* hakuna! Hizi fedha ziko mifukoni mwa Mawaziri wawili ama vipi! *I take this matter to be serious.*

Lakini ningependa kwanza kupata mwongozo kutoka kwako Mheshimiwa Naibu Spika kabla sijamaliza hotuba yangu kuhusu utaratibu utakaofanywa kwa Kanuni Namba 50 ya Kanuni za Bunge letu Tukufu kuwa imekiukwa. Ningependa kupata mwongozo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, alichosema Mheshimiwa Mbunge hapa ni sahihi, kifungu namba 50 (i). “Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Kwa sababu hiyo Mbunge ye yote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na uhakika kuwa maelezo aliyoyatoa ni sahihi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sahihi kabisa, lakini kwa sababu umeitoa katika mchango wa hotuba yako na upande mwengine hawajapata nafasi ya kujibu pengine wao watasema hayo unayoyasema si sahihi au ni sahihi.

Kwa hiyo, tutasikiliza majibu kutoka kwa Waziri kwamba je, unachosema ni sahihi? Kwa sababu ni kweli kama unachosema ni sahihi, basi yaliyosemwa si kweli, lakini tutasikiliza majibu upande wa pili. Nashauri umalizie hotuba yako halafu tutasikia majibu wakati wanachangia. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la *Privatisation Trust* ni kubwa. Maana ya *Trust* pengine haileleweki vizuri. *Trust* ni kivuli cha mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unamiliki mali yoyote kwa niaba ya mtu ambaye hana uwezo wa kukimiliki. Hao ndiyo Watanzania wengi amba wanamiliki mali kwa kupitia *Privatization Trust*. Hii *Privatization Trust* imekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya chombo cha zamani kama ilivyoelezwa kwenye hiyo sheria iliyopita ni kwamba *Privatization Trust* itashikilia hizi hisa kwa niaba ya Watanzania wanaoishi vijijini wakiwemo watu wangu walioko Musoma Vijijini ambao hawana uwezo wa kuzinunua. Mpaka jana wakati nachunguza mambo haya sikuona hata *certificate* ya hizo hisa zikilimilikiwa na *Privatization Trust*. Nimeona kwenye Ofisi yao barua kutoka hazina inasema inapeleka asilimia tatu ya hisa za *TCC* kwa chombo hicho. Sasa kama hicho chombo hakiko basi hakina maisha tena nani anashikilia hizo hisa?

Ningependa kushauri kwamba kwa kuwa chombo hicho hakipo, Bunge lako tukufu litoe azimio kwamba fedha hizo zishikiliwe na *Administrator General* mpaka hapo Bunge litakapopitisha Muswada mzuri wa kulinda mali ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Unit Trust* yoyote haiwezi ku-be created bila chombo cha Serikali kujua na kuna vyombo viwili, kuna Msajili wa Kampuni anawenza ku-create an Investment Trust aka-hold hizo hisa. Pia *Administrator General* anawenza kusajili Trust vyombo hivi viwili bado havijafanya kazi. Lakini kama kuna Trust lazima kuwepo na *Trust Deed* ambayo ina-set out obligation za *Truees* na niwa kina nani? Mpaka leo hakuna *Trustee* amba ni mkataba kati ya *Trustees* na *Manager* wa kushikilia hizo fedha. Ni hatari sana kuona fedha za Watanzania nyingi namna hiyo, zimekaa kiholela bila msimamizi wa Kanuni. Siamini kweli kabisa sisi Wabunge, tunaweza kukakaa hapa, tukasema mambo yaliyosemwa na Waziri wa Fedha katika ukurasa wa 33 ni sawa. (*Makofi*)

Lakini kama nime-differ na page 33 siyo maana kama nimekiuka utaratibu wa kwamba siungi mkono Bajeti isipite. Bajeti nzima nasema ipite kwa asilimia mia kwa mia. Lakini haya ya 37 yafutwe na chombo kingine kiundwe mapema na Bunge hili iwezekanavyo ili kuweza kulinda maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache haya nilivyosema narudia kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie hoja hizi. Nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri kwa Bajeti yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeza Wabunge wote wapya, niwatakie kila la heri katika kazi zao majimboni. Hasa hasa nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kukomboa Jimbo la Kigoma Kusini ambalo lilikuwa la Wapinzani. Naomba nitamke wazi kwamba mshindi hapa ni CCM kwa sababu wamekomboa jimbo lao la Upinzani. Hayo majimbo mengine yalikuwa yao. Kwa hiyo, mshindi hapa ni CCM kuchukua jumbo lake la Kigoma hilo ndiyo tunataka ieleweke hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa kweli na mimi nizungumze machache kwa sababu mimi niko kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara nikiwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa William Shellukindo. Nawapongeza wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Tumepata fursa ya kuzungukia Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa. Maajabu tuliyoyakuta huko hatuwezi kusimulia, lakini kwa sababu Mheshimiwa Nimrod Mkono amesema Wabunge lazima tuwe wakweli ni lazima tuseme ukweli. Kwa kweli uongo humu ndani haufai. Tunataka Bajeti inapozungumzwa humu, izungumzwe kwa uwazi na ukweli, ndiyo tutaweza kuliokoa taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachotaka kuzungumza ni wale wawekezaji wabovu sijaona kwenye Bajeti ya mipango, kwamba wanawafanya nini? Hawa watu wamechukua mashirika bila mikataba ya kueleweka, wamefungua vifaa ndani ya mashirika hayo wameuza, tuna hatihati ya kwamba wamepewa mashirika yale bila hata kulipa fedha. Mikataba inayosema nenda kwanza kaangalie namna ya kufufua baadaye ukifufua tutakuja tuzungumze hatuna uhakika na maneno hayo. Lakini kinachoonyesha hayo ni kitendo cha kufungua fungua vifaa na kuuza hicho tumeuona. Kwa mfano

tumeuona kwenye Shirika la Nguo Morogoro na Kiwanda cha Magunia cha Moshi, yule mwekezaji aondoke hata kama ana wakubwa wake huko juu wanaomlinda sisi tunataka aje atueleze humu Bungeni. Sisi tulitaka tukutane naye anasema yeye ana wafadhili wa juu. Juu wapi? Mbinguni au ndani ya Bunge hili au wapi? Tanzania hii kuna wakubwa juu dhidi ya wananchi wadau wenyewe Kiwanda cha Magunia? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amekwenda Mkuu wa Mkoa pale amefungiwa wanasema hakuna sababu wao hawatambui Serikali, wanatambua mkubwa mmoja tu aliywapa kiwanja. Sasa humu nilitegemea hayo yanatokea huyo mwekezaji, ukubwa huo anaupata kwa nani? Maneno hayo yamesemwa kama mtataka ushahidi Mwenyekiti wa Kamati anayafahamu na sisi Kamati nzima tunayafahamu. Sasa tunataka Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Ubinafsishaji Dr. Abdallah Kigoda, aseme humu ndani, yule bwana ule ukubwa anaupata wapi? Je, kwa Mheshimiwa Rais? Kwa sababu ndiyo wakubwa wa nchi hii. Kwanza kabisa ni Mwenyekiti wa Taifa Mheshimiwa Rais, ndiyo huyo anayempa? Ili aue viwanda vyetu? Hapo ndipo tulipofikia? Tunataka kujuu hili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli ya Moshi haina hadhi kabisa. Mbaya zaidi na mtu huyo ameishitaki Serikali tukashindwa kufanya kazi yetu. Huo ndiyo uwekezaji? Hoteli imekwisha kabisa tunamwuliza anasema mimi nimewashitaki ninyi Serikali.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshiwa Zakia Meghji, nilizungumza sana humu Bungeni tatizo la Hoteli ya Mikumi, wamemnyang'anya mwekezaji wa zamkani wa hoteli ya Mikumi na sasa wanatafuta mwekezaji mwengine. Lakini nakuomba Mheshimiwa Waziri ufanye haraka kutafuta mwekezaji mwengine. Tunalo tatizo la pale watalii wanashindwa kuja. Hoteli zetu bado si nzuri, tungelipenda sasa tupate mwekezaji mzuri ili tufanye biashara kwa sababu tunataka kuondokana na umaskini. Bunge hili ndiyo linazungumzia kuondoa umaskini wa kweli. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatugombani na mashirika yanayofanya vizuri lazima tuyapongeze. Tumekwenda *TPC* tukakuta wazalishaji wazuri, walikuwa wakizalisha tani 32 sasa wako kwenye tani 64 kiwanda kimoja. *Kilombero Sugar* leo tunazungumzia sukari tani laki moja, tani laki moja ya sukari siyo suala la mchezo. Mtibwa wanazungumzia habari ya tani 35 za sukari. Sasa hapo nataka napo nisaidiwe na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba tulishazungumza sukari inayohitajika kutumika hapa nchini ni laki tatu. Hiyo sukari ninayoizungumza tani 64 na 100,000 tani 35 tunashindwa kupata soko, tunataka kupata ufanuzi kwa nini soko halitoshi. Kwa sababu mahitaji ni laki tatu, inayozalishwa haijafikia laki tatu, sukari ya *industrial sugar* inaingia bila utaratibu. Nataka kuzungumzia hili Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ulifahamu kwamba uingizaji wa sukari si mzuri bado unaendelea. Tumeukemea mwaka jana, tumevana kidogo lakini tunaona bado sukari inaingizwa nchini bila utaratibu. Hata Kariokoo napata shida kidogo mimi nakuta Tanzania wanakunywa sukari ya nje kwa nini? Mbeya, Songea, Iringa tunapata tabu kuuza sukari ya Kilombero kwa nini Waziri uko wapi? Umaskini mtautoaji namna hii? Hivi mnataka kusema leo hii Mheshimiwa Eliachim Simpasa Jimboni kwake hawaonji sukari ya kilombero. Vile vile Kagera,

Rukwa bado hawajapata sukari ya Kilombero. Tulikuwa tunazungumza uzalishaji mzuri, sasa uzibaji mianya ya rushwa hamtaki kuziba halafu mnatuambia humu tumefanya vizuri tupongezeni, tutawapongeza, lakini mengine tutawasema. Tunataka mfanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Kazi za siasa na utendaji vyote ni kitu kimoja sisi tumekabidhiwa siasa na kusema uwazi na ukweli tutabaki kusema ukweli. Ninyi wenzetu tendeni haki lakini tunapotaka kufanya kazi ya kuwatendea Watanzania haki sisi ndiyo kazi tuliyoomba ya kuwatendea haki yao? Mimi faili langu liko Mikumi kwa wakulima, wapiga kura, ndiko faili langu liliko. Haya ninayosema ndiyo waliyonituma kwamba sukari yangu wakiiuza pale Kilombero, ikiuzwa haraka watalipwa kwenye miwa wanayovuna ndiyo maana yake. Lakini sukari yao ikicheleweshwa kuuzwa kwa sababu *industries sugar* imeingia nyingi inasababisha ile isiuzwe wanachelewa kulipwa, inasababisha kutokulipwa na faili langu linachafuka mimi nakosa kuchaguliwa pale. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina ugomvi na *breweries* bia zipo mambo mazuri. Sina ugomvi na viwanda vya nguo tunamshukuru sana Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa pale kazi yake anaifanya vizuri. Tumetembelea viwanda viko safi. Kwa kweli mimi sitasita mahali ambapo nimeona safi kupasifu kwa sababu tumetembelea na tunamshukuru Mheshimiwa Spika, kutuwezesha tatembelee viwanda hivyo. *Oh my God* muda unaanza kuishia maneno machache haya, maana kengele ya kwanza maana yake muda umekwisha. (*Makofi/Kicheko*)

Mkoa wa Morogoro sisi tumesema kama ipo haja ya mbolea tupeni matrekti. Mbolea pelekeni mikoa mliyosema ni *Big four*. Lakini Mkoa wa Morogoro tunahitaji trekta za kulima, hatuna haja ya mbolea, tunahitaji trekta. Mkoa wa Morogoro watu wote ni wasaarabu hivi mnawenza kuwaacha watumie jembe la mkono mpaka leo? Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo wa kutumia jembe la mkono wale kweli? Tunachoomba fanyeni utaratibu, mikopo sasa mmesema ipo, mashirika yashirikiane tukopeshwe matreka sisi tutalipa. (*Makofi*)

Mfano mzuri uko Kilombero wametukopesha trekta zao tumelipa. Leo nilikuwa na nazungumza na Kilombero leo wamelipa *cheque* shilingi bilioni kwa wakulima wa nje. Kwa nini ninyi mnashindwa kukopesha matrekti watu walime pamba, mboga mboga, miwa? Sasa kweli mikopo ikianza kutoka mkulima wa Kilombero kwangu unapomwambie aende *Exim Bank* halafu akutane na yule Mhindi wa *Exim Bank* akaonyeshe hati ya nyumba, kule Kitete hati za nyumba nzuri atapata wapi? Zombo, Kisanga, Malolo utapata wapi nyumba yenye hati? Tukubaliane kukopeshana kuitia ardhi yake. Wekeni mipango mizuri ya ardhi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umebakiki dogo. Nimeona katika *paragraph 62* ukurasa wa 37 ardhi ekari milioni 4. Hizo ekari milioni 4 ziko mkoa gani mlizozikuta wenzetu Serikali? Mimi napata wasiwasi kwa sababu Mkoa wa Morogoro ekari zote zimebaki mikononi mwa Serikali za Viji. Sasa huku kuna ekari milioni 4 zimekaa zinangoja utaratibu wa kugawiwa wawekezaji. Ni mkoa gani wenye hizo ekari? Msije Morogoro! Morogoro ardhi yote tuna msimamo nayo tunataka mtupe trekta, tuanze

kulima. Sisi tunavyo viwanda ambavyo tulishindwa kuendesha lakini ardhi tunayo tunayoweza kulima mkitupa trekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sitaki kengele ya pili inigongee, naunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na hoja ya Waziri wa Fedha.

Kwanza kabisa ningependa na mimi niungane na wenzangu Waheshimiwa Wabunge kuanza kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa, katika chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni na Wabunge kuanza kuingia katika Bunge hili la Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili naomba nitoe angalizo dogo kutoka kwa wapiga kura wangu, wamezungumzia hii hoja ya kufuta kodi ambako nimeelezwa mpaka sasa hivi sherehe zinaendelea za kikipongeza Chama cha Mapinduzi kwa maamuzi yao muafaka, watu wamekesha wakishangilia. Lakini wanalo sikitiko moja kama Wabunge wote tungelikuwa na busara zetu na maamuzi kama yanavyofanywa na Chama cha Mapinduzi zile bilioni 6 zilizotumika kwa ajili ya uchaguzi mdogo bila sababu ya msingi zingetusaidia katika kuimarisha pato la Taifa. Huo ndiyo ujumbe wanaoutoa wapiga kura wa Mbeya. Kwa hiyo, unaweza ukapima ni nani mwenye busara, ni yule anayefuta au ni yule anayeongeza matumizi ya kwa taifa shilingi bilioni sita kwa majimbo 15 si lelema. Kwa sababu jimbo moja ni karibu milioni 400. Nakipongeza sana Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina furaha sana katika kipindi hiki cha Bajeti. Furaha yangu iko katika maeneo mawili. Kwanza nimepata mwenzangu wa kutoka Kigoma Kusini, ambaye tumemaliza wote Shahada ya Uzamili katika mambo ya uchumi, Mheshimiwa Edward Ndeka. Kwa hiyo, nimefurahi sana kwa hilo, amekuja kuungana na mimi humu Bungeni. Kwa hiyo nimefurahi. Lakini furaha yangu ya pili ni kilio cha watu Mbeya cha muda mrefu cha kuangalia namna gani pato la taifa litaleta maendeleo kwa wananchi bajeti hii imekidhi hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 mwezi 6 mimi ndiyo nilikuwa jimboni namalizia m Kutano wa mwisho na wananchi. Walikuwa na kero zaidi ya 16. Katika Bajeti hii kero 15 zimeondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema usilinganishe Tanzania na nchi nyingine ya Ulaya, bali mwangalie jirani yako. Nilikuwa nikiiangalia *trend* ya kukua kwa uchumi wa Tanzania toka 1998. Nimeona tunafanya vizuri sana kuliko hata majirani zetu Kenya. Tumeendelea hivyo mpaka hapa tulipo. Ukitosha katika takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa linasema sisi Tanzania hatuna *setback* kwenye *human development index*, lakini ndiyo kipimo halisi hatuna *setback*. Zipo nchi zenyе majina

yao makubwa ambazo zina *setback* katika uchumi huu. Sasa kama tusiposhukuru na kupongezana katika hili basi hatuwezi kwenda mbele hata kidogo.

Kwa sababu mimi nilitaka kuchanganyikiwa na ndipo kwa mara ya kwanza nikagundua kwamba kumbe kazi ya Uwaziri ni kubwa mno kwa sababu kwa kiasi kikubwa hawa Mawaziri Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba wamekidhi yale matakwa ambayo tulikuwa tunayataka kwa muda mrefu. Bajeti hii imetumia *bottom up approach*, wadau wote wamechukuliwa na sisi wenyewe tuko mle ndani. Sasa na mimi nawapongeza sana kwa hiyo *accommodation phylosophy* kwa sababu wengine wasingeweza ku-accommodate mawazo haya. Naipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Sasa kitu cha msingi ambacho nafikiri kaka yangu Mheshimiwa Aggrey Mwanri amekieleza vizuri jana, ni kwamba katika ufanuzi wa sasa hivi wa uchumi hakuna taifa lenye uwezo wa kubeba makontena ya maendeleo na kuwapelekea wananchi. Jukumu la nchi ni kutengeneza mazingira mazuri. *Definition* ya sasa hivi inapatikana kwa yule mtaalam mwana harakati wa uchumi ambayo ndiyo *contemporary definition*. Usichukulie ile hali ya zamani ya kufikiri unapoboresha uchumi basi unapeleka vitu ambavyo ni *physical*, unawabebea kwenye makontena hapana! *Contemporary definition* ya uchumi wa sasa hivi ni kwamba una-create enabling enviroment for the people to enjoy long healthy and a creative life hiyo ndiyo *definition* ya sasa hivi. Wewe tengeneza mazingira lakini wao wenyewe watajisukuma. (*Makofi*)

Sasa kama tumeondoa kodi nimeshawaelezea kwamba watu wana-*celebrate* huko wanashilingilia hiyo siyo *enjoyment*? Watu sasa wataungana na familia zao hawatakimbia kodi siyo *enjoyment* hiyo? Sasa mlifikiri ni *enjoyment* ipi inayozungumzwa hapa? Wameanza tayari toka filimbi ilipopigwa wanafurahia. Kuwa na watoto ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Kwa hiyo, nataka niwaambie kabisa ndugu zangu mimi ninaafikiana kabisa na Bajeti hii. Lakini tatizo langu kubwa ni hili pato la taifa. Sidhani kama tunakoelezeke labda tutaomba maoni zaidi, lakini ukisoma kuanzia ukurasa ule wa 40 pato la Taifa tumekuwa tukielekeza zaidi katika mambo mbalimbali na kutenga fedha. Lakini mimi nina mambo mawili ambayo nafikiri tunayasahau.

La kwanza katika nchi zote zilizoendelea ambazo mwaka 1992 nitatolea mfano wa Korea ya Kusini *per capital income* ilikuwa sambamba na Tanzania wakati sisi tuna *export sisal* wao zao lao kubwa lilikuwa ni hizi *wig* ndiyo walikuwa wanazisafirisha nje na kupata fedha za kigeni. Tanzania wakati huo tulikuwa na katani kama zao letu kuu. Lakini wenzetu walipofika mwaka 1970 waliimarisha *heavy industries*. Sisi tukawa *stagnant* kidogo. Walipoingia karne ya sasa hivi wameamua ku-*adopt* sayansi na teknolojia. Lakini wamefanyaje, katika pato la taifa wametenga fedha *specifically* kwa ajili ya utafiti. Lakini sasa sisi tunafikiri kwamba tunaweza kwenda katika *trend* hii bila *kuji-engage* katika utafiti wa uhakika. Haiwezekani tutafika mahali katika kukua kwa uchumi tutakuwa tunaelea pale. Nafikiri kuna Mheshimiwa alizungumza sana juu ya kuchakaa kwa *computer* Mzumbe, siyo Mzumbe tu, bali vyuo vikuu vyetu vyote wana *computers* ambazo zimechakaa. Pale chuo kikuu nilibahatika kutembelea kitengo cha (*ERB*) *Economic Research Bureau*, *computer* zao ni za muda mrefu akifungua inachukua

dakika 15 ku-*react*. Sasa unamtegemea akufanyie utafiti haiwezekani. Kwa hiyo, utafiti ni lazima tuupatie ufumbuzi wa kutosha. Vituo kama kilimo Uyole - Mbeya, vituo kama IKiruguru - Mwanza, Ilonga - Morogoro, lazima vipewe fedha za kutosha kufanya utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwapatia fedha wale watalaan wangu wa kituo cha utafiti Uyole, kwa mfano, ekari moja kuna uwezekano wa kuzalisha mahindi kuanzia gunia 35 mpaka 40. Sasa mkulima ukimwezesha kumpa mbegu bora iliyozalishwa na watafiti hawa hatakuwa na shida ndiyo *enabling environment* hiyo. Wananchi hawataki uwa-cash mkononi na wala hakuna taifa linalowa-cash watu mkononi. Lakini watengenezee mazingira wao wenye waweze kwenda kuzalisha. Kwa kweli bado utafiti tumeupa kisogo katika Taifa hili. Bado hatufanyi kazi nzuri ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la umeme. Mimi kidogo sielewi kwamba ni nini nia ya taifa juu ya tatizo la umeme. Katika karne hii ya 21 watu wameachana na *hydro electricity*. Afrika ya Kusini wao ni ya tano katika uzalishaji wa umeme katika dunia lakini hawatumii *hydro*, wanatumia makaa ya mawe. Hivi kama ni *investment* mimi nisingependa kuwaita makaburu, kama ni *investment* hizo ndiyo *investment* za uhakika, tuwaite hawa tuchukue ule ujuzi wao, wakiondoka watatuachia sisi ile teknolojia ya hapa. Hiyo ndiyo sehemu za kuwavuta kwa sababu sasa hivi viwanda vyetu vinazalisha chini ya kiwango hasa wawekezaji wanakataa kwa sababu wanaona kwamba gharama za umeme kusini mwa Jangwa la Sahara Tanzania tunaongoza kwa gharama hizo.

Lakini kuna *deposits* za makaa ya mawe pale mchuchuma zipo za kutosha. Sasa nafikiri niunge hoja mkono. Kwa nini tusitumie nafasi hii ya mahusiano mazuri na wawekezaji hawa kutoka *South Africa* tuka-tape uzoefu wao, tuka- *invest*, kuliko hii hali ya kutegemea *hydro* ambayo mara nyingi mvua si za kuaminika sana. Tuangalie kwamba on the long run kama ni kuwekeza fedha, tuwekeze kama tulivyofanya sasa hivi kwa ajili ya viwanja, yaani ya kiwanja cha mpira na mambo mengine. Siyo rahisi kutengeneza moja kwa moja lakini tuwekeze tuwe na lengo la kusema tuondoe kabisa kero ya umeme ndani ya nchi hii ili kupata wawekezaji wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya suala zima la ubinafishaji. Naomba nizungumze kitu kimoja. Waingereza wana usemi wanasema *you have to go the whole hog*. Unapoamua kufanya jambo fanya jambo kwa nguvu zako zote. Sasa mimi nina wasiwasi tukiendelea kulegalega katika dhana hii ya ubinafsishaji hatutafika mbali. Tutarudi katika zile karne za mwanzo ambazo wenzangu mtakumbuka ukichukua China, Tanzania na *Northern Korea* kwa nini tumeachana ni kwamba wakati wenzetu wameamua kujenga *scientific socialism* sisi tukasema *no, still tunaweza tukatengeneza African socialism*.

Kwa hiyo, tukawa tunajiondoa kwenye *principles* za *scientific socialism* tunasema sisi ujamaa ni asili yetu, watu walikuwa wanaishi katika mambo haya toka zamani. Tukafanya *modification* kwa njia hiyo tukiwa tunajirudisha nyuma. Sasa hivi naona *trend* hii inataka kuhamia kwenye ubinafsishaji, kwamba tunaanza sasa kulegalega ni kwamba

ubinafsishaji ni dudu kubwa sana ndiyo dunia ya sasa hivi. Unasema kama huwezi kumpiga adui yako jiunge naye. Sasa hii tabia ya kwamba tunakwenda katika ubinafsishaji tunarudi, tunakwenda hatutafika mahali tujenge uchumi amba ni stable. Tumeingia katika dhana ya ubinafsishaji *let us go the whole hog*. Hivi majeruhi hospitali wanasaidiana katika hali gani? Majeruhi wanasaidiana baada ya *histogram* kuonyesha majeruhi huyu ameanza kupata nafuu. Lakini katika *level* hii sisi wote ni majeruhi tutasaidiana na *indigenous economy* mnayoizungumza hiyo. Tutasaidiana vipi wakati wote ni majeruhi. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, lazima tujenge *base*, tuimarishe uchumi tuondo umaskini, tuimarishe *macro economy* ambayo ndiyo *corner stone* katika mambo ya ubinafsishaji, tuimarishe sekta binafsi, tuimarishe utawala bora amba ndiyo eneo ambalo nafikiri Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, katika Bajeti yake *perfomance* ya asilimia 52, asilimia 48 hazipo ninafikiri tatizo kubwa ni katika utawala bora. Kuna watu sasa hivi hawataki kabisa kufanya kazi. Tunazunguka huko maofisini wanaingia hii saa tatu, saa nne mtu hayuko ofisini na uki-*happen* kwenda ofisini basi kinachofanywa zinapita chips, kuku ndiyo kazi inayofanyika utendaji wa kazi umezorota mno. (*Makofi*)

Hiyo ndio tunayoita huma *factor decay*. Ni tatizo kubwa sana. Nilikuwa nataka uniambie kwamba Bajeti ni mchakato. Ni *process*. Sasa tumefikia hapo. Je, katika utekelezaji yaani *implementation stage* ambayo ndio *imetu-let down* mwaka jana, safari hii tumejiandaa kiasi gani? Mheshimiwa Waziri atueleze vikwamishi vyta utekelezaji mwaka jana vilikuwa ni vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hotuba zote hizi mbili kwa pamoja.

Kwanza na mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Wabunge wote wa CCM na *CUF* walioshinda uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. Nawapeni hongera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, vile vile napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Kigoda na Mheshimiwa Mramba kwa hotuba ya Bajeti nzuri yenye matumaini. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya hotuba hizi zote mbili ni kupambana na umasikini, kuwawezesha wananchi, wakulima, wafugaji, wavuvi pamoja na wafanyakishara wadogo wadogo. Hotuba imeleta mipango mizuri na ikiwa mipango hiyo itafanikiwa kama ilivyoordheshwa, tunaweza kusema wananchi wetu asilimia 80 watapata ukombozi wa kiuchumi. Kwa upande wa kilimo, mipango iliyotolewa kama itafanikiwa kikamilifu, tunaweza kuita kuwa mpango huu ni sawa kama *Green Revolution* iliofanyika India kwa upande wa kilimo na Tanzania, hii itakuwa ni *Green Revolution* kwa upande wa Tanzania. Kwa hiyo kwa sababu ni Bajeti, imemgusa kila

mwananchi. Imegusa wakulima, imegusa wafanyabiashara wadogo wadogo, wavuvi na wastaaifu. Kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mbinga Magharibi sina budi kuunga mkono bajeti hii mia kwa mia. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge walionitangulia wamechangia Bajeti hii kwa undani na kwa kina kabisa. Wametoa mapendekezo mengi mazuri na ninaafikiana nao. Lakini mimi nitachangia Bajeti hii sehemu moja kubwa. Kwa nini Bajeti zetu za miaka yote pamoja na Bajeti ya mwaka huu ni Bajeti tegemezi? Ni bajeti tegemezi na pili Bajeti yetu hii tukiilinganisha na Bajeti za nchi jirani katika kila viashirio inaonyesha waziwazi ama kila kipengele kinaonyesha kama sisi tunarudi nyuma. Sasa kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mawazo yangu, yapo mambo mawili. La kwanza Bajeti hii imekwishajionyesha mwelekeo wa kuwawezesha wananchi wanyonge. Bajeti hii imekwishaonyesha njia ya kuweza kutatua tatizo hilo. Hilo sitaliongelea zaidi kwa sababu hayo yamekwishaelezwa kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningependa vile vile niongelee, kwa nini Bajeti yetu ni tegemezi kwa muda mrefu? Tatizo la pili, uchumi wetu umebebesha mzigo mkubwa wa kuendesha Serikali wakati uwezo wa uchumi uko chini. Ndio tatizo moja kubwa sana. Uchumi wetu mdogo unaendesha Serikali kubwa. Sasa nini kifanyike? Kwanza, inatakiwa Serikali iweke mikakati ya kupunguza ukubwa wa Serikali yetu. Sehemu kubwa ya Bajeti yetu inagharamiwa na mikopo, wafadhili na misaada mbalimbali ya kutoka nje. Misaada hiyo baada ya kuelekezwa igharamie miradi mbalimbali ya nchi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, mikopo hii yote inagharamia gharama ya kuendesha Serikali. Hapo ndipo inaonyesha wazi kwamba kwa muda mrefu sana utaratibu wa kuweza kusaidia uchumi wetu ili uweze kubeba gharama inayotakiwa haikuweza kufanyika. Sehemu kubwa ya mikopo yetu inaendesha Serikali, kugharamia matumizi ya kawaida, wakati mikopo inatakiwa itumike kwa ajili ya kugharamia miradi ili miradi iweze kuongeza pato la Taifa, iweze kuongeza uwekezaji katika uchumi wetu na iweze kuongeza miradi mbalimbali katika uchumi wetu. (*Makofit*)

Sasa Serikali yetu inatakiwa iweke mikakati ya makusudi ya kupunguza gharama za Serikali. Kila Idara na kila Wizara iweke mikakati ya kupunguza gharama ya kuendesha Serikali yetu ili uchumi wetu uweze kuwa na nguvu ya kubeba gharama za Serikali. Misaada yote tunayoipata iweze kuelekezwa kwenye miradi inayoweza kuongeza nguvu ya uchumi wetu ili tuweze kupiga hatua ya maendeleo. Serikali inatakiwa iweke mipango ya kupunguza gharama. Kupunguza Idara mbili zinazofanya kazi zinazofanana. Kwa mfano leo hii hapa Bunge liko Dodoma lakini Serikali ipo Dar es Salaam. Hii yote inaongeza gharama ya Serikali. Inatakiwa Serikali na Bunge iwe mahali pamoja ili mambo yote yaende sambamba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ninaloweza kuongelea kidogo ni juu ya mgawanyo wa wataalam wetu. Wataalam wetu wote wamejazana Wizarani badala ya wataalam hao kuwasambaza karibu na walengwa ili waweze kutoa ushauri wao kwa walengwa na walengwa wakatumia ushauri wao wakaongeza uzalishaji, wakaongeza kipato chao na wakaongeza pato la Taifa. Kwa mfano, mimi sioni kama kuna usahihi

Idara ya Nyuki ikae Makao Makuu Wizarani Dar es Salaam wakati wafugaji wakubwa wako Tabora na wanahitaji ushauri wao. Kwa hiyo Idara kama hizo zinazoweza kufanana na hii zinatakiwa ziwe karibu na wazalishaji ili ziweze kutoa michango yao mikubwa kwa wahusika. (*Makofi*)

Jambo lingine ningependa nichangie juu ya wazo kuhusu mapendekezo kwamba kila Wilaya iwe na zao moja la biashara na zao moja la chakula. Wazo hilo ni zuri kwa Wilaya nyingine. Lakini Wilaya kama Mbanga tunalazimika kuchagua zao kutokana na hali ya hewa. Wale wanaokaa sehemu za joto wana zao lao, wale wanaokaa kwenye baridi nao wana zao lao. Sasa ukichagua zao moja, wengine utamwachia nani? Wengine waangalie tu maendeleo ya watu wengine? Inatakiwa kila Wilaya ipewe madaraka ya kuamua wafanye nini katika jambo hili. Huwezi kuacha zao moja na zao lingine likapata huduma zote zinazotakiwa kwa ajili ya kuondoa umasikini. Kwa hiyo, maamuzi hayo yangefanywa kwa kila Wilaya kulingana na mazingira yao.

Jambo lingine, ningependa kuongelea juu ya uamuzi mzuri na ninaipongeza Serikali kwa ajili ya kuongeza kima cha chini cha wastaifu kuwa Sh.20,000/=. Ningombwa vile vile wangekumbukwa wale wastaifu waliochukua kwa mkupuo. Walichukua kwa mkupuo bila kuelewa. Hawakufahamishwa ipasavyo. Nafikiri ni vema Serikali ikawakumbuka vile vile katika kima hiki cha chini cha wastaifu. (*Makofi*)

Ningependa niongelee juu ya kutoza kodi dawa za mbu za kuchoma na chandarua. Kwa sababu tunapambana na ugonjwa wa malaria, ni vyema kodi ikaondolewa katika dawa ya mbu na vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ningependa kuomba tu kwamba ili wananchi wangu aweze kuchangia kwa undani kabisa juu ya Bajeti hii, ningombwa miundombinu ifuatayo iboreshwe. Kwanza barabara, maji na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa mwisho kwa leo asubuhi. Katika kuchangia kwangu, kwanza napenda kutoa hongera kwa Wabunge wote wapya waliochaguliwa. Kwa sababu damu nzito kuliko maji, nawapongeza zaidi wale waliochaguliwa kupitia tiketi ya CCM. (*Makofi*)

Pili, nampongeza Ndugu Harry Kitilya kwa kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa *TRA* na Ndugu Luoga kuwa Naibu wake. (*Makofi*)

Tatu, ningependa kumpongeza sana Ndugu Sanare kwa utumishi uliotukuka kwa kuanzisha *TRA* ambapo wakati ule kwa mwezi tulikuwa tunapata Shilingi bilioni 35, lakini mpaka akiondoka ameacha *record* ya bilioni 100. (*Makofi*)

Nne, naomba niwapongeze sana Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda kwa Bajeti nzuri. Nasema ni Bajeti nzuri kwa kweli, unaiona

kabisa! Imeandaliwa sawasawa, kuwa dira ya CCM kwa uchaguzi wa mwaka 2005. Huu ni mwanzo mzuri na ninawapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. Hii Bajeti imeondoa kero nyingi sana na kwa sababu nataka kuzungumzia mengi kidogo, sitaki kurudia jinsi kero mbalimbali zilivyoondolewa katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nataka kuuelekeza kwanza katika Sekta ya Nishati. Hivi majuzi wakati Naibu Waziri wa Ujenzi akijibu swali langu kuhusu maendeleo ya *Mtwara Development Corridor*, alisema na ninamnukuu; “Hakuna miradi yoyote ambayo imeanza moja kwa moja kutekelezwa chini ya programu ya *Mtwara Development Corridor*, lakini kuna mafanikio ya kutia moyo kwa baadhi ya miradi miwili mikubwa *Anchor Projects* ambayo imepata wawekezaji.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa statement hii mimi ilinivunja moyo. Ilinivunja moyo kwa sababu nakumbuka katika Bunge hili hili mwaka 2000 mimi nilitoa mfano wa Askari wa Miavuli kuvamia Mtwara na nikasema, kama wasipofanya hivyo upesi watajikuta wananing’inia mitini kwenye nyaya za umeme na majumba. Sasa naona hili ndilo linaloelekea kutokea katika hii Idara ya Nishati. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi iliyobarikiwa katika Tanzania yote kama Mtwara. Kuna gesi nyingi, acha hii ya Songsongo; kuna *Mnazi Bay* na Msimbati. Hizi gesi, chukua ya Msimbati au ya *Mnazi Bay* inaweza kutosheleza kabisa kuleta umeme kwa Mtwara, Lindi na Ruvuma yote. Sasa kwa tunakalia uchumi! Watu wako mitini mpaka leo na hakuna umeme tumlaumu nani? (*Kicheko/Makofi*)

Sera kama ingekuwa sahihi, sasa hivi sisi wenyewe Watanzania ndio tungekuwa tunaongoza *Mtwara Corridor*. Sio kusubiri watu wa Msumbiji, watu wa Malawi, watu wa Afrika ya Kusini waje wufanyie kazi, hapana. Jamani mko wapi? Hamieni Mtwara! Anzeni kazi! (*Kicheko/Makofi*)

Mimi sidhani kwamba wenzetu huwa wanaelewa maana ya *Mtwara Development Corridor*. Labda jina lenyewe ni baya. *Maana corridor* ni sijui ni...

MBUNGE FULANI: Uchochoro. (*Kicheko*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Jamani ule si uchochoro. Ni ukanda wa maendeleo. (*Kicheko/Makofi*)

Kuna raslimali nyingi sana zitumieni zile. Zikitumika raslimali zile za, Mtwara tutaibadilisha na hata Tanzania yote tutaibadilisha. Nasikitika kusema kwamba mpaka sasa nimeangalia vitabu vyote vya Bajeti, *Mtwara Development Corridor (MDC)* na *NDC* ndio ambayo inayosemwa kwamba itaishughulikia *Mtwara Development Corridor* lakini haina kasma yoyote katika vitabu vyenu. Sasa hii maana yake nini? Kama hakuna kasma ya kuendeleza miradi hii hivi nani atakayeideleza jamani? Wananchi wa Mtwara waeleweje mambo haya? Sasa ikiwa tutaendelea hivi, kwa vyovyote vile hatutakuwa na maendeleo katika upande ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usambazaji wa umeme, inashangaza kuona kabisa kwamba Mtwara na Lindi ni ya mwisho kabisa katika mikoa kupata umeme katika nchi hii. Kwa nini? Kama nilivyosema gesi ya *Mnazi Bay* peke yake inahitaji dola milioni moja na nusu au Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuichimba gesi na kuisambaza umeme Mtwara. Sasa Waziri wa Fedha kweli huna bilioni tatu na sisi tukapatwa umeme wa uhakika? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wenzetu hao wa Wizara ya Nishati walitaka kuunganisha umeme kutoka Masasi kwenda Lindi. Lakini nataka kuliambia Bunge lako kwamba huu ni mwaka wa 15 toka mradi huu uanze mpaka leo haujakamilika. Aibu gani hii! Kinachotakiwa ni kutoka pale Masasi kuwe na transformer, Chikukwe, Chigugu, Chikundi, Mwena na nyaya za umeme kutoka Ndanda kuititia Nangoo na Nanganga. Mpaka leo miaka 15! (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimesema toka mwanzo ni nzuri sana na mimi naiunga mkono. Lakini hawa wa Nishati wanamharibia Waziri kwa miaka 15 bila kutekeleza mradi huu. Wananchi wa Jimbo la Masasi na Vijiji hivyo nilivyovitaja, wamenituma niondoe Shilingi katika Bajeti hii kwa ajili hiyo. Lakini mimi nasema sio kwamba nitatoa hiyo Shilingi, nataka maelezo ya Waziri wa Nishati anipe maelezo, hivi kwa nini? Kwa nini, miaka 15 imepita umeme haujaunganishwa katika maeneo haya ingawaje zile bakuli na kila kitu kimewekwa, lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika? Si dharau hiyo! Au kutuonea! Maana yake nini?! Hii bwana hatukubali. Kwa hiyo, Shilingi itatoka kwa sababu hiyo. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia kuzungumzia hoja ya mwenzangu Mheshimiwa Seleli alivyoeleza jinsi ya wafadhili wanavyogawanya katika nchi hii, akaitaja Mikoa minne ambayo mpaka sasa haina wafadhili. Sasa mimi nilitaka kutoa mfano wa Mtwara na Lindi. Kule tumepata wafadhili wanaitwa Wafini. Sasa hao Wafini kwa kweli wana roho nzuri tu lakini ni maskini kweli kweli kule Ulaya. Sasa katika kuletwa Mikoa ya Mtwara na Lindi, sijui nia yenyewe ilikuwa ni nini? Lakini katika kazi walizofanya, wamejisambaza kila mahali. Ukienda Afya wamo, ukienda Maji, wamo; elimu, wamo; nyuki, wamo; ufugaji mbuzi, wamo. Aah, jamani! Sasa itakuwaje? Kwa hiyo hakuna *impact* ya maendeleo. (*Kicheko/Makofî*)

Ninachoomba ni kwamba, Serikali iwasimamie ili kuondoa utitiri wa miradi midogo midogo ya namna hii, badala yake watamke kwamba fanyeni kitu kimoja cha maana. Kwa mfano sisi tuna shida ya ubanguaji wa korosho Vijijini. Hao wangeambiwa nendeni Vijijini huko mkaanzishe viwanda vidogo vidogo na teknolojia ili wananchi wabangue korosho kwa wingi katika Mikoa ile. Hiyo itakuwa na *impact* kuliko kufuga mbuzi na kufuga nyuki. Ningombwa sana kwamba kwa kweli tunavyowapeleka hawa wafadhili mbalimbali katika maeneo haya tuone *impact* yao itakuwaje. Hawa wenzetu wafini tunawashukuru, lakini uwezo wao ni mdogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka kuunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote, lakini tahadhari ile niliyompa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu ni

wananchi wenyewe wa Chigugu, Chikukwe, Mwena, Nangoo na Nanganga wanasema kabisa, kama mwaka huu hatupati umeme, Mbunge wetu aondoe Shilingi. Kwa hiyo, tafadhalii Mheshimiwa Waziri asinilazimishe kuondoa Shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninategemea kwamba hayo yote yatakelezwa. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii, nilitaka nitoe ufanuzi wa lile ambalo Mheshimiwa Nimrod Mkono alilisema. Yeye katika kuchangia alitaka ufanuzi kutoka kwangu na akasema ali-*quote* kifungu cha Kanuni Namba 50.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ili tuwe na ufanuzi sahihi, hiyo Kanuni kwa wale wenyewe vitabu vyta Kanuni inasema, nitasoma haraka haraka. “Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, Mbunge ye yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au kubahatisha tu na Spika au Mbunge mwingine yeyote aweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge aliyetakiwa kufanya hivyo, atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika, kwa ajili hiyo.”

Sasa Mheshimiwa Mkono ali-*quote* kifungu cha 37 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa maelezo yake aliamini kwamba hayo yalikuwa sio sahihi ya hotuba hii. Sasa kwa Kanuni zinavyosema, mimi natoa maelekezo kwa Serikali kutoa ufanuzi wakati wanajibu hoja hii, iwe hii ni hoja ya lazima ya kujibu, isiachwe bila kujibiwa. Kwa hiyo, hayo ndio maelekezo ambayo natoa kwa hili jibu. (*Makofî*)

Baada ya kusema hivyo sasa nasitisha shughuli za Bunge, mpaka Saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.58 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia jioni hii ya leo na pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuandaa Bajeti hii kwa kushirikiana na Watendaji wao. Naomba pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwakaribisha Bungeni Wabunge wote wapya ambao wamejiunga nasi hivi karibuni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya Fedha na Watendaji wote, kwanza kwa kukubali pendekozu nililotoa kuhusu mfumo wa kodi ya mapato. (*Makofî*)

Nawashukuru kwa sababu kwanza kwa mara ya kwanza Serikali itakuwa imekubali kuteremsha kiwango kile cha kodi ya mapato ili kuwawezesha wafanya

biashara hasa wadogo wadogo ambao kwa kweli kwa mfumo uliokuwa umepita walikuwa katika utendaji wa biashara zao hawafikii vile viwango vya mauzo ambavyo vilikuwa vinatumika kwa kutoza kodi ya shilingi 50,000/=. Hakuna wafanya biashara wadogo wadogo waliokuwa wanaweza kufikia angalau kiwango kile cha shilingi milioni 7 kwa mwaka. Wengi walikuwa chini ya hapo. Kwa hivyo nashukuru kwamba sasa wamekubali angalau kuanzia kiwango cha mauzo ya shilingi milioni tatu kwa mwaka na kuwa shilingi elfu ishirini kwa mwaka, badala ya shilingi elfu hamsini kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio makubwa yatapatikana. Kwanza idadi ya walipa kodi sasa itaongezeka na pengine nitoe mfano mdogo tu kwa manufaa ambayo Serikali itapata. Wakati kodi ikiwa katika kiwango cha shilingi elfu 50,000/= kwa mwaka, kwa mfano walikuwa wanalipa kodi wafanya biashara watano. Maana yake Serikali ilikuwa ikipata shilingi laki mbili na ishirini na tano elfu tu kwa wafanyabiashara hao watano. Kwa kuteremsha kiwango hiki sasa kuwa shilingi elfu 20,000/= kwa mwaka. Nina uhakika kwamba idadi ya walipa kodi itaongezeka na kwa mfano, wakifikia walipa kodi 15 tu zaidi maana yake sasa kwa shilingi 20,000/= Serikali itakusanya shilingi laki tatu kwa mwaka. Kwa hiyo, kuna ongezeko hapa kutokana na ongezeko la idadi ya watu kulipa kodi kutokana na kupungua kwa kiwango cha kodi iliyowekwa. (*Makofi*)

Sasa kazi moja iliyobaki ni kwa ndugu zangu wa *TRA*. Tunachotakiwa kufanya hapa ni kujenga mazingira mazuri sasa ili wafanya biashara wasiendelee kuziogopa Ofisi za *TRA*. Wafanya biashara wengi wanaziogopa kabisa Ofisi za *TRA* na kitu kinachowaogopesha ni wasiwasi kwamba watatakiwa kulipa kiwango kikubwa kuliko uwezo wao. Kwa hiyo, wakimwona mtu wa *TRA* kama kule Wilayani kwetu akitokea, maana wao ndiyo wenye uwezo wanavaa tai, basi akionekana mtu amevaa tai anajulikana ni mtu wa *TRA* anakuja. Unafunga milango, unafunga na madirisha. Sasa tujenge mazingira mazuri. *Friendly environment* ili wafanya biashara waweze kuzizoea Ofisi za *TRA* na waweze kuingia na kulipa kodi zao kikamilifu. (*Makofi*)

Sasa nasema hili kwa sababu ipo mifano mingi, wapo wafanya biashara ambao kwa sababu ya kutojua utaratibu wa namna ya ulipaji wa kodi ya *VAT* wamekuwa wakiwaandikia viongozi wa *VAT* katika Wilaya au katika Mikoa barua za kuomba ushauri na ushauri haukuwa unatolewa na matokeo yake baadhi ya wafanya biashara hao wamekuwa wanapigwa *penalties*. Mtu anaomba ushauri hapati, halafu baada ya mwaka anavamiwa na watu wa *TRA*, wakifika pale wanamwambia umefanya makosa hapa *penalty* milioni tano. (*Makofi*)

Hizi ni tabia za kuwaogopesha watu, tukizipunguza nina uhakika tutaendelea kukusanya kodi kwa kiwango kikubwa sana. Napenda kusema vile vile kwamba wafanya biashara wadogo hasa wale wa Wilaya ya Muheza, watafurahia sana uamuvi wa Serikali wa kufuta kodi ya maendeleo. Kwa sababu moja ya ziada na inawezekana hili nalo lilikuwa linatoka katika Wilaya nyingine kwamba wewe kama una biashara, wewe binafsi unalipa kodi ya maendeleo shilingi elfu tatu, lakini biashara yako nayo inatozwa kodi ya maendeleo shilingi elfu kumi na mia nne.

Ukiwa na biashara mbili, maana yake ni shilingi elfu ishirini na mia nane kodi ya biashara, pamoja na shilingi elfu tatu yako wewe binafsi. Sasa haya zaidi ni kwamba kina mama walikuwa hawalipi kodi ya maendeleo. Lakini anapoanzisha biashara mama, atapambana na kodi ya maendeleo, hiyo ya biashara atalazimika kulipa kodi ya maendeleo ya shilingi elfu kumi na mia nne katika kila biashara. Sasa kosa ni kuanzisha biashara. Lakini lazima tuelewe kwamba biashara zinalenga katika kutoa huduma na hivyo tukiwaogopesha watu kuanzisha biashara, maana yake tunakwamisha huduma kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda katika eneo la udhibiti na ukwepaji wa mafuta, kodi na mafuta ya petroli. Wafanya biashara katika eneo ambapo sasa tunakubaliana kimsingi kwamba tutaweka *floor meter* pale *Kurasini Oil Jet*. Mimi nawapongeza sana kwa uamuzi huu wa kuweka floor meter. Kwa sababu katika muda mrefu amba kwa bahati nzuri labda mimi nimefanya kazi *TPDC*, tulijaribu sana wazo hili la kuweka *Flow Meter*. Lakini limekuwa ikipingwa siku zote kila tulipokuwa tukijaribu na lilikuwa linapingwa kutoka pande zote mbili ikiwa ni pamoja na pande za waagizaji wa mafuta. Watu walikuwa hawataki udhibiti wa kujua kiwango cha mafuta yaliyoingia nchini. Kwa hiyo, wazo hili walikuwa wanalikataa. Sasa mimi napongeza sana kwamba sasa linakubalika. Lakini utatokea utata kwamba sasa *Flow Meter* tunaiweka wapi. Tutaiweka pale *manifold* au tunaiweka mwanzo, wakati meli zinaanza *discharge*. Sasa naomba hili tulifanyie maamuzi haraka ili lisije likachelewesha uwekaji *Flow Meter*. (*Makofi*)

Lakini alivyozungumza wenzangu, ni kwamba baada ya kukubaliana kuweka *Flow Meter*, basi tunachukua *figures* zinazotokana na *Flow Meter*, tunaachana na mpango wa kwenda kupanda kwenye matenki ya mafuta kule kwenye *installation* za makampuni, kitu ambacho naomba kurudia tena kama nilivyosema mwaka jana, viongozi wetu na watendaji wetu walikuwa hawapandi katika matenki yale. Wafanyakazi wale wa *installation* ndio walikuwa wanapanda na wao wanapata *figures* tu. Kwa hiyo, usizitegemee sana *figures* za makampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie hili suala la ulipaji wa kodi, baada ya kufanya *Tax Assessment*, baada ya mafuta kupita pale kwenye *Flow Meter*, muda wa siku 15 walizopewa makampuni ya mafuta ni mdogo sana. Labda nikumbushe tu kwamba makampuni ya mafuta yamekuwa yakilipa hii kodi kutokana na mauzo ya kipindi cha siku 10, kila baada ya siku 10 ndiyo wanlipa kodi. Mafuta ambayo yako kwenye matenki yao katika maeneo ambayo ni *Bonded Warehouse*.

Kwa hiyo, mafuta yakija pale hayalipiwi kodi mpaka mauzo ya siku 10. Kwa hiyo, walikuwa wanamu du kulipa hizi kodi baada ya kila siku 10. Sasa unapowaambia walipe kodi baada ya siku 15 kwa *consignment* kubwa ya zaidi ya tani 25,000 mpaka lita milioni 90 kwa kweli hapo hawatamudu. Maana matokeo yake ni kwamba watajitatihidi kwa kadri watakavyoweza kupunguza kiwango cha mafuta wanachoagiza. Kwa sababu hii itawakwamisha kwenye *Cash Flow* yao.

Kwanza wana *obligations* ya kuendelea kuagiza mafuta na *LC* nyingi ni za *ninety days*. Kwa hiyo, bado wana *obligations* ya kulipia mzigo wa mafuta yaliyokuja na bado ana *obligation* ya kulipia kodi. Hizi zote pamoja ukizichanganya unampa mzigo mkubwa. Kwa sababu kwanza kiwango cha mafuta anacholeta, wanaleta mafuta kwa ajili ya *stock* ya miezi miwili. Sasa hujayauza mafuta kwa miezi miwili unaambiwa uyalipie kodi yote na huku unalipia *LC*. Nadhani ni vizuri tukaangalia, tusije tukawa pengine tumechanganya wakati tulipokuwa tukitoa maamuzi haya tukidhani kwamba tuna-stick kwenye yale mauzo ya siku 10.

Naomba sasa niende kwenye suala lingine na hili ni suala ambalo pia limeguswa katika hotuba ya Waziri. Ni suala la kupunguza kodi ya *LPG* kwa asilimia 50. Mimi naliunga mkono sana. Kama ilivyozungumzwa leo asubuhi kiwango cha utumiaji wa mkaa kimeongezeka sana. Kwa hiyo, hii ni njia pekee ya kuweza kuhamasisha watu kuanza kutumia *LPG* na kuendelea kuitumia na kupunguza matumizi ya kuni.

Lakini kitu kimoja ni dhahiri kwamba unapoamua kuhamasisha watu kuna vitu vingine pia lazima viendane na uhamasishaji huo. Kitu kingine ambacho nakiomba kitazamwe ni kutazama uwezekano wa kuondoa kodi kwenye hizi *LPG Cylinders* ambazo sasa hivi vimeanza kuingia nchini. (*Makofî*)

Umeteremsha kodi ya *gas*, lakini vifaa vya kutumia *gas* bado viko juu. Kwa hiyo, teremsha kodi katika vifaa ili watu sasa waweze kutumia *gas* kwa wingi. Suala lingine nitagusia katika sekta mbili. Sekta ambazo zimesaidia sana kuchangia uchumi wa Taifa ni sekta ya madini pamoja na sekta ya Utalii. Sasa tulijitahidi kuboresha utalii hasa *ku-promote* utalii. Mimi naomba kuwapongeza sana wenzetu wa Shirika hili la Ndege la Tanzania, *Air Tanzania Corporation Limited*, kwa kukubali kurejesha ile nembo ya Twiga katika ndege zao. Walikataa, sasa wamekubali kurejesha na wanairejesha kwa kuchora twiga mkubwa zaidi na siyo kumweka mkiani kama mtu wa mwisho sasa yuko katika bodi ya ndege. Nawapongeza sana. (*Makofî*)

Lakini suala lingine ni suala la Sekta ya Madini. Napendekeza kwa sababu Tanzania kweli ni nchi moja yenye madini mengi sana na ya aina nyingi sana za madini kuliko nchi nyingine yoyote katika Bara la Afrika, sasa bila kuweka elimu kwa wananchi wetu katika sekta hii ya madini, basi tutaendelea kuibwa kila siku. Ninapendekeza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hasa ile *Section* ya Kitivo cha *Engineering*, tuanzishe Kitengo Maalum pale, ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo katika *Planning Engineering* na wapo watalam kutoka nje Watanzania wanaofanya kazi katika Vitengo vya aina hiyo. Wengine wamekwishaomba kazi ya kusaidia Chuo Kikuu kuanzisha kitengo hicho. Naomba Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu waangalie maombi ya wenzetu hawa watusaidie. Vinginevyo tutaendelea kuibwa kwa sababu hakuna watalaam ambao watatusaidia kutupa *information* za uhakika wa kitu kinachofanyika.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi mafao yao. Mimi napongeza sana jambo hili. Litasaidia sana kupunguza migogoro. Lakini naomba pia Wizara ya Fedha iangalie na kwa mpango

wa kusaidia kuboresha mazingira katika milima yetu ya Amani katika Wilaya ya Muheza. Wananchi wameitikia vizuri sana na Serikali ya Finland imeshasaidia kulipa fedha katika eneo la mipaka. Wananchi wameshakubali kuhama na kutoa nafasi. Sasa sijaona humu kama fedha za kusaidia kulipa fidia kwa wananchi wale wa Amani kama zimetengwa.

Finland wamethibitisha kwamba wao wako tayari kusaidia Serikali lakini ni lazima Serikali ya Tanzania nayo iweke chochote kujazia nguvu, kama hatujatenga fedha hizo maana yake ni kwamba tutapata matatizo ya wananchi hawa wanaodai fidia. Kwa sababu sasa hivi hakuna kazi zozote zinazoendelea kule, wanangojea kupata fedha zao waweze kuhama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele ya kwanza imeshalia, basi naomba kutoa kauli kwamba ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nashukuru kwa kupata nafasi hii. (*Makofî*)

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda nichukue nafasi hii nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa mimi nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja hizi mbili muhimu kuhusu mpango wa maendeleo pamoja na Bajeti ya mwaka huu 2003. (*Makofî*)

Ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichaguliwa kwa kishindo katika uchaguzi uliopita. Nami naungana na wenzangu kuwakaribisha Bungeni hapa na kuwatakia kila la kheri katika harakati zao za kutumikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga kwa kuteuliwa kushika nafasi kubwa na nzito ya kuongoza *TRA*. Tunawatakia mafanikio mema katika kazi zao hizi na kuwatakia kheri. Ningependa vile vile kuchukua fursa kumpongeza sana Ndugu Sanare kwa kazi kubwa na nzito ambayo alitumikia Taifa hili katika kulijenga Shirika hili kubwa na muhimu la *TRA*. Namtakia kila la kheri, afya njema na mafanikio mema katika wadhifa mpya aliopewa kulitumikia Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili kwa kazi kubwa ambayo wamefanya kuandaa na kuleta hotuba nzuri sana za Mipango na Bajeti Bungeni kwetu hapa. Ningependa vile vile kuwashukuru Manaibu Waziri wao pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wengine ambao wameshirikiana nao na Wizara nyininge kuweza kuleta mipango hii. Kusema kweli mipango hii ni mizuri, iliyo wazi na yenyе kuleta matumaini makubwa kwa maendeleo yetu. Mambo mengi ambayo yamezungumzwa mle ndani yamezingatia kwa dhati kabisa kwanza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2000, Dira yetu ya Maendeleo 2005 na Mpango wa Kuondoa Umaskini.

Kusema kweli kero nyingi kubwa zimeondolewa katika Bajeti hizi na vile vile imezingatiwa hatua ambazo ni muhimu, kuboresha na kuuendeleza uchumi wa Taifa letu

pamoja na kuendeleza sekta mbalimbali. Nawapongeza sana kama vile wenzangu wengine walivyowapongeza na kwa vile Waheshimiwa Wabunge waliotangulia walisema maneno mengi kuunga mkon, mimi naungana nao na mimi napenda kuchukua fursa hii kabla sijafika mbali kuunga mkono hoja hizi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wenzangu waliotangulia wameshazungumzia karibu kila kipengele, nisingependa tena kuchukua fursa hii kuyarudia yale yale, bali nitajaribu kuzungumzia masuala ambayo kwa maoni yangu hayajazungumziwa vyakutosha au yale ambayo yanahitaji mkazo. Suala moja ambalo limetiliwa mkazo, ni suala la kuongeza kasi ya mauzo nchi za nje. Nashukuru kwamba katika hotuba zote mbili, suala hili limetiliwa mkazo katika sehemu nyingi sana.

Vile vile nafurahi sana kwamba Serikali imechukua hatua nzuri mpaka sasa hivi kujaribu kutekeleza kwa makini mapendekezo yaliyomo katika Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Tanzania yaani *Export Development Strategy*. Pamoja na mambo mengine, tunaona hatua za kutangaza *Export Credit Guaranteed Scheme* zimefanikiwa na zinaendelezwa zaidi. Mambo ya kutengenezea *Export Processing Zone* yameanza na yanaendelea kwa kasi. Vyombo vingine vyakutangaza kuuza biashara kama vile *Market Development Centre* ya Wizara ya Ushirika na Masoko inaendelea. Inatoa ajira nyingi sana, zinanufaika katika masula haya.

Lakini pamoja na hayo, bado inahitajika hatua nyingine zifanyike ili kuweza kuchukua nafasi mbalimbali ambazo zinajitokeza katika soko la dunia sasa hivi. Tukichukua kwa mfano, *WTO*. *WTO* ina utaratibu mle ndani ambazo zinatuwezesha sisi kupata *market access* kubwa zaidi na kulinda viwanda vyetu katika hatua hizi za awali.

AGOA imetupa nafasi nzuri, ushirikiano wa *SADC* umetupa nafasi nzuri, ushirikiano wa *East African Community* umetupa nafasi nzuri. Lakini ili tuweze kuchukua nafasi hizi vizuri, kusema kweli tunahitaji maandalizi mengi sana. Nashukuru jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Serikali kusisimua kilimo, kusisimua utalii, kuendeleza madini na sekta nyingine mbalimbali. Lakini ili hayo yaweze kupata mafanikio, uzalishaji pekee hautoshi. Uzalishaji unahitaji kuendana na kuboresha bidhaa zenyewe na kuboresha masoko.

Ni jambo la kusikitisha kidogo kwamba Wizara ambayo ina majukumu ya kufanya kazi hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara. Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo ambazo zina kazi kubwa ya kufanya utafiti, kufundisha, kufufua hatua za kukuza masoko, imepewa fedha ndogo sana. Kwa kweli Wizara ya Viwanda ya Biashara imepewa fedha kidogo kuliko hata vile ambavyo ilipata mwaka jana. Sasa hili ni jambo la kukatisha tamaa, kwamba wakati tuna nia kubwa na mkazo mkubwa katika kuendeleza shughuli hizi Wizara husika na Taasisi zake husika hazikupewa fedha za kutosha kwenye masuala haya. Kama tunavyoolewa utafiti, mafunzo, shughuli za ukuzaji masoko, ni shughuli ghali sana, zinahitaji fedha nyingi sana na bila kufanya utafiti na bila kufanya mafunzo kwa watu wetu mbalimbali hatuwezi kupata mafanikio yanayotarajiwa.

Kwa hiyo, naiomba Serikali, Wizara ya Mipango, Wizara ya Fedha, Wizara nyingine zinazohusika zijaribu kuona kwamba kama mwaka huu haitawezekana, kwa miaka inayokuja Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zake mbalimbali za utafiti na masoko ziweze kupewa fedha maalum katika suala hili.

Suala moja ambalo lilikuwa limewekwa katika *Export Development Strategy* ni suala la kutengeneza *Export Development Fund*. Hili tumezungumzia muda mrefu, lakini sijaona dalili ya kuelezwewa humu ndani katika mpango wa mwaka huu au mpango wa miaka miwili mingine inayokuja.

Kwa hiyo, hili ni suala ambalo nakumbushia kwamba hili ni suala muhimu ili kuwasaidia wananchi mbalimbali wadogo wadogo. Bahati mbaya, hapa kwetu tuna fikra ya kuendeleza biashara, kuendeleza masoko, labda na shughuli ambazo zinastahili kufanywa na wananchi au mfanya biashara mmoja mmoja. Hili linawezekana kwa mashirika makubwa *Multinationals* au *Trustnationals*.

Lakini wananchi wadogo wadogo bado wanategemea sana huduma za mashirika kama *SIDO*, *TIRDO*, *CARMATEC*, *BET*, vitu kama hivi ili waweze nao kuwa na uwezo wa kuingia katika soko la kisasa hasa ukizingatia ushindani uliopo katika soko la utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya suala hilo la kukuza mauzo nje, vile vile kuna masuala ambayo yanahusiana na hilo. Kwa mfano, suala la *VAT*. Waheshimiwa Wabunge wengi waliopita walizungumza juu ya suala la *VAT*, kwamba wakati wenzetu ambao tunashirikiana nao katika soko la Afrika Mashariki na ambao tunashinda nao katika soko la dunia wateremshe *VAT* sisi tunapandisha *VAT*. Kusema kweli hii ni kujiuwa wenyewe. Na hili suala lazima lifikiriwe tena tuone vipi tunaweza kufanya sisi tukahimili ushindani katika soko la dunia kwa kuweka kiwango cha chini cha *VAT*.

Masuala ya gharama za nishati, gharama za usafirishaji, ni masuala ambayo tumeyazungumzia na kuyapigia kelele mara nyingi sana. Lakini inaelekea suala hili linachukuliwa kwa wepesiwepesi tu. Tukifanya kiepesiepesi na kupuuzia kama inavyoonekana, kusema kweli suala la kusema tutaongeza mauzo yetu katika soko la dunia itakuwa ni ndoto tu. Kwa sababu hapa hatuwezi kushindana na wenzetu ambao wana bidhaa bora, bei nafuu, na uwezo wa kuzipeleka kule kwa wenzetu. Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusisitiza hilo.

Suala la pili ambalo limejitokeza katika hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ni suala la uwezeshaji wananchi na ubinafsishaji. Hili ni suala muhimu sana. Mambo mengi yamezungumziwa mle ndani, hatua nyingi zimezungumziwa pamoja na kufungua Benki mbalimbali ambazo zitawezesha wananchi kufanya masuala haya. Na imeelezwa kwamba upendeleo maalum utatolewa juu ya suala hili. Maneno haya ni mazuri ni maneno ambayo kusema kweli yamefurahisha wananchi wengi sana pamoja na wananchi wa Jimboni kwangu kama vile lilivyowafurahisha suala la kuondolewa kodi ya maendeleo kama kero, na hili ni jambo ambalo limewafurahisha sana kwamba litawekewa uwezo wa kuijendeleza katika suala hili. (*Makofii*)

Lakini sasa katika maelezo mbalimbali yaliiyotolewa na Wizara hizi mbili, kuna benki nyingi sana zimetajwa. Kuna benki ya Ushirika, kuna Benki ya Maendeleo ya Kilimo, kuna Mfuko ule wa kuendeleza wafanya biashara wadogo wadogo mbalimbali. Sasa hii kidogo ni vizuri tukafafanua na ikaelezwa wazi wazi kwamba itasimamiwa na nani na utaratibu gani. Vinginevyo itakuwa ni vurugu na kama walivyoeleza Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, kwa nini shughuli hii kwa kuanzia isiendeshwe na *National Micro Bank*. (*Makofî*)

Suala lingine ambalo nimelifurahia Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwamba katika ushirikiano wa Afrika Mashariki ziko barabara ambazo zinatengenezwa. Moja ya barabara hizo ni barabara inayotoka Chalinze, Tanga hadi Hororo. Pamoja na kwamba tunatumaini kwamba masuala haya yatakelezw na Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini suala hili halikujitokeza mahali popote ama katika Wizara ya Ujenzi au katika Mkoa wa Pwani, Tanga au mahali pengine popote.

Sasa hilo ni vizuri likafafanuliwa kwamba itakuwajekuwaje, je sisi hatuhusiki kabisa, tunawaachia wao moja kwa moja na kazi yetu sisi ni nini? Kusema kweli inatia aibu sana kwamba katika barabara zetu za kuunganisha nchi zetu hizi mbili, barabara ya Tanga-Hororo ndiyo peke yake ambayo haina fedha. Tafadhali sana. Kama alivyo sema vile vile Profesa Mbilinyi, nafikiri lilikuwa ni jambo la mantiki zuri zaidi iwapo barabara ile isingekua Chalinze-Tanga-Hororo peke yake, lakini ingeunganishwa na barabara ya Pwani kupitia Pangani kuja Dar es Salaam, hivyo itatusaidia sana kukuza biashara yetu ya utalii kwa ujumla. (*Makofî*)

Suala lingine Mheshimiwa Naibu Spika, ambalo tumekuwa tukilizungumzia kwa muda mrefu ni kero tunayoipata sisi Waheshimiwa Wabunge kuhusu fedha za matumizi ya Ofisi zetu Wabunge na matumizi ya kule. Tumekuwa tukiambiwa kwamba fedha hizi zinapatikana Ofisini kwa Mkuu wa Mkoa, mara Ofisini kwa Mkuu wa Wilaya na katika vitabu hivi vya Bajeti ambavyo nimepitia, sijaona hilo suala limejitokeza wapi? Je, liko fungu, iko Kasma imewekwa na Kasma hii iko wapi? Wabunge wafuatilie wapi suala hili. Hilo tungependa lifafanuliwe ili tusiendelee kupata kero hii ambayo haitusaidii sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema yote hayo, nimefurahi sana kwamba Mawaziri katika hotuba zao hizi wamesisitiza umuhimu wa sisi, wananchi kujituma.

Sisi viongozi kushirikiana katika kazi zote. Mipango yote mizuri hii iliyopo haiwezi kufanikiwa, haiwezi kupata maendeleo, haiwezi kuendelea kama sisi tutazembea, kama sisi hatutafanya kazi kwa bidii, kwa maarifa zaidi na juhudii zaidi na wakati mwingine tusiogope kuitwa wanyapara ili tuweze kufanikiwa. (*Makofî*)

Ni muhimu baada ya Bajeti hii vyombo vyote mbalimbali, Wizara, Mikoa, Ofisi za ma-DC wakawa na mipango ya utekelezaji mahususi ambayo inaeleza wajibu wa kila mtu, afanye nini, lini ili kuweza kutekeleza mambo haya mbalimbali. Kwa hiyo, hayo Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo muhimu sana ili tupate mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumzwa nashukuru sana kwamba mwaka huu imeonekana kwamba Wizara zote mbili pamoja na Benki Kuu na wengine wametoa takwimu karibu zimefanana ukiacha zile chache ambazo amegusia Mheshimiwa Janguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la kufurahisha sana na tunaomba kwamba kwa siku zijazo jitihada hizi ziendelee kufanywa hivyo. Isipokuwa hii *Micro Economy* imefasiriwa namna mbili. Waziri mmoja anasema uchumi mpana, mwingine anasema uchumi jumla. Sasa tungeshukuru kwa maana neno hili lingepewa tafsiri moja tukaendelea kufanya kazi kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ulionipa. Ningependa kusema tena kwamba nimefurahishwa sana na hotuba hizi. Wananchi wa Jimboni kwangu Mkinga wamefurahishwa sana na hotuba hizi. Nami napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ISSA MOHAMED SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba mbili hizi jioni hii ya leo. Napenda kumpongeza Kamishna Mkuu mpya wa *TRA*, Ndugu Kitilya, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Kamishna Mkuu wa *TRA*. Pia napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya wanne wa Chama cha Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwao kuja kushiriki na sisi katika Bunge hili kuanzia mwaka 2003 mpaka mwaka 2005 na ninategemea wataendelea mpaka mwaka 2015. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri ambazo zina mipango mizuri ya nchi yetu ya mwaka 2003 kuelekea mwaka 2004. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake hususan pale ambapo amerekebisha baadhi ya kodi kwa sababu ilikuwa kero kubwa sana kwa wananchi kama vile kodi ya maendeleo na utiriri wa kodi nyingine ambazo zilikuwa zinawapa kero sana Watanzania. Kwa hiyo, katika hilo nampongeza kwa kuondolewa kwa kodi hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa fika kwamba, Serikali ina nia ya kuweka uwazi wa shughuli hizi kama za kodi ili kila Mtanzania asipate kero ya namna yoyote ile katika shughuli zake. Lakini kuna tatizo kidogo, baadhi ya sehemu bado napenda nimfahamishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, kuna kero kubwa sana ya walipa kodi juu ya baadhi ya kodi zimerekebishiwa au mfumo wa kulipa kodi umerekebishiwa lakini kuna baadhi bado zina kero kubwa na walipa kodi wanalamika sana lakini bahati mbaya wale wanaolalamika labda hawana mwakilishi wa kuja kuwasemea hapa. Kwa hiyo, tukiona matatizo tunataka tuitumie nafasi hiyo ili kuwawakilisha wananchi kwa sababu na wao vile vili ni Watanzania.

Wafanyabiashara wa Dar es Salaam, kwa Makamba, wana matatizo sana ya ulipaji wa kodi, wana kero kubwa sana hususan katika Bandari ya Dar es Salaam. Leo

wafanyabiashara wa Dar es Salaam kutokana na kero iliyopo katika Bandari ya Dar es Salaam wanaikimbia Bandari ya Dar es Salaam wanakwenda kushusha mizigo yao Bandari ya Mombasa. Hii ni kero ambayo haina sababu ya kuwepo katika nchi hii, kwani wafanyabiashara wanaoitumia Bandari ya Dar es Salaam wamekosa nini mpaka Bandari ile washindwe kuitumia na kwenda kuitumia Bandari ya Mombasa, mbona wafanyabiashara wa Mombasa hawaji kuitumia Bandari yetu ya Dar es Salaam? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam wanasema wakishusha mali zao pale wanachukua siku ambazo hazipungui 90 kutoa mizigo yao Bandarini na adhabu wanazozipata wanasema anazijua Mungu hata kuzitaja wanashindwa kwa sababu mtu anaweza akanunua mali ya dola 10,000 lakini akakutana na adhabu pale hatimaye mabwana kodi wanamfilisi moja kwa moja, wanaweza wakamlipisha kodi labda 10,000 mara kumi. Wanasema wakishusha mali zao Bandari ya Mombasa haichukui zaidi ya wiki moja mali zao wanakuwa wamezitoa katika hali ya usalama bila kuwa na bughudha yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kikubwa kinachowafanya waichukie Bandari ya Dar es Salaam, ni ukiritimba. Baada ya kuwahoji sana ni nani anayesababisha ukiritimba huo, wakasema kuna Kampuni ya *Inspection Control Services*, hii ndiyo inayowanyanyasa sana. Katika kuifuatilia ni kweli hii kampuni inawanyanyasa sana walipa kodi kwa sababu kama unaleta mali yako hawa watu wa *Control Inspection Services* wanakuwa na power kuliko mtu mwingine yeyote pale na pia kuliko hata *TRA*, ambayo ina mamlaka ya kukusanya kodi yote katika nchi hii, basi inakuwa haina nguvu kama inavyokuwa na nguvu hii Kampuni ya *Inspection Control Services*. Hawa watu ukileta mali yako ya dola 10,000 wanakwambia hii mali si ya dola 10,000, ukiwaliza ni kiasi gani mali hii nimeinunua, basi mara nyingi wanaikadiria mara tano ya ile *amount uliyolipia wewe*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa matatizo haya yanakuwa yanawapa taabu sana wafanyabiashara kwa sababu kila mfanyabiashara anataka alipe kodi katika mazingira mazuri, Serikali ailipe katika mazingira mazuri ipate mapato yake na yeye pia aweze kufanya biashara ili ajikidhi katika mahitaji ya maisha yake. Kwa hiyo, kero kama hii inawarudisha nyuma na inawavunja moyo. Pia wakikimbilia Mombasa hawaishii kwa kumkandamiza mfanyabiashara tu, lakini hata Serikali inakosa baadhi ya mapato kwa sababu mzigo ule ukishushwa Dar es Salaam, meli ikishusha mali pale kwenye makontena kuna wafanyabiashara ambao wanalipa *handling charges, port charges* na gharama nyingine za kuweka mizigo na pia watu wanapata ajira.

Kwa hiyo, ikiwa wanashushia mizigo yao Kenya kisha wanakuja kulipa ushuru Tanga, hizo gharama nyingine kama za *handling charges, port charges* na kadhalika, Serikali haitazipata, inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali waliangalie zaidi suala hili na hii kampuni tunayoizungumzia mara nyingi lakini cha ajabu inakuwa ukitoka Bungeni hapa unaweza ukaambiwa hii haina muda baada mwezi mmoja itaondolewa, lakini ukienda unakuta bado wanaendelea kutuna na kuwanyanyasa watu bila sababu yoyote ile. Serikali naomba waichunguze kampuni hii kwa kina na usumbufu

wanaoupata wafanyabiashara *at least* haya matatizo wayashughulikie ili wafanyabiashara wasipate matatizo ambayo si ya muhimu kuyapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba labda kwa mawazo yangu, Serikali najua ya kwamba imefanya baadhi ya marekebisho ya kodi lakini ingeliweka uwazi kwa walipa kodi ili kila mlipa kodi aelewé kile anachostahili kukilipa wakati wa kulipa ile kodi ya Serikali. Tatizo si kupunguzwa kwa kodi Tanzania, tatizo la kupunguzwa kwa kodi lipo lakini baada ya kupunguza kodi pia uwazi unakuwa hakuna. Walipa kodi wanakuwa hawaelewí kwa uwazi ile kodi wanayostahili kuilipa. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, amesema samaki wanapunguzwa kodi kutoka asilimia mbili mpaka asilimia moja, mfanyabiashara atanunua samaki wa Sh.100/= kwa mvuvi lakini akipeleka kwa bwana kodi haikubali Sh.100/= anakwambia umenunua samaki kwa Sh. 1,000/=, akilipishwa asilimia moja ya Sh. 1,000/= ni sawa na kuwekewa asilimia mbili. Kwa hiyo, nafikiri hilo nalo ni muhimu liangaliwe ili watu wasilalamike kwa sababu wakilalamika ni kwamba, matatizo ya watu wachache ndiyo maana watu wanailaumu Serikali, wanailaumu *TRA* na wanawalaumu mabwana kodi pengine wabaya, ni wachache tu siyo wote, Serikali siyo mbaya na wala chombo chenyewe kinachokusanya kodi siyo kibaya. Kwa hiyo, napenda kuiomba Serikali iliangalie hilo. (*Makofi*)

Kuna tatizo lingine pale Dar es Salaam kwenye *Container Terminal*. Ile *Container Terminal* imebinafsishwa lakini cha ajabu wale watu wa kwanza ambao walikodi ile *Container Terminal* siyo wanaoientesha sasa hivi, mkataba bado ni ule ule lakini wanaoientesha siyo wale! Kwa hiyo, sijui Serikali inaelewa wale walioko sasa hivi wameingia katika kuiendesha ile *Container Terminal* kwa mikataba gani, kwa sababu inawezekana wamepeana kienyeji wanaendesha wengine, walioingia mkataba na Serikali wameuza kienyeji bila ya Serikali kujua. Kwa hiyo, napenda kuiomba Serikali ifuatilie ili kama kuna tatizo hilo lisimamiwe kwa sababu kama unavyoju, bandari ndiyo lango letu kuu la nchi, tukiliacha likilega lega kiholela tunaweza kupata taabu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hayo niliyoyaeleza ameyasikia na atayaangalia. Kwa hiyo, napenda niende katika kudhibiti mafuta ya *petrol*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuliona hili na niipongeze sana Serikali kwa hatua hii hasa sababu zinazonifanya niipongeze Serikali ni sababu mbili. Kwanza, ni kwa sababu sekta hii inatoa mchango mkubwa wa kodi ya mapato yote ya Serikali kwa karibu asilimia 20. Kwa hiyo, kuweka udhibiti wa kutokuvuja kwa mapato ya Serikali zaidi ya asilimia 20, katika hili ni lazima niipongeze Serikali. Jambo la pili, kulegezwa kwa masharti ya biashara kunakuwa na uratibu finyu kwa hiyo hatua hizi zitarekebisha kasoro zilizojitokeza na kuimarisha sekta hii kwa ukusanyaji wa kodi. Huu ufungaji wa *flow meter* utaisaidia sana Serikali na siyo tu kwa kukusanya mapato, bali tutajua kwa uhakika ni kiasi gani cha mafuta yanayoigizwa nchini. Kwa hiyo, tutaweza kujua nchi hii inatumia mafuta kiasi gani ili kurahisisha mipango yetu ya baadaye. Suala hili nalipongeza kwa sababu hizo. Napenda kuishauri Serikali kwamba, hatua hii iende sambamba na tathmini ya uingizaji wa mafuta

kwa malori ili ifutwe na mafuta yote yaingizwe kwa meli na reli ili tudhibiti zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ulipaji kodi kwa mafuta ya ndani. Uagizaji wa mafuta kupewa muda wa siku 15, napenda kuipongeza sana Serikali kwa sababu kukamilisha malipo yote ya kodi kwa siku 15 ni vizuri kwa kuwa Serikali hapo nyuma ilikuwa inapata gharama kubwa katika kuhifadhi mafuta ya biashara kwenye bohari kwa muda mrefu. Pia si vema makampuni ya mafuta kuhodhi kodi ya Serikali na kuifanyia biashara nyingine, haya makampuni ya mafuta yasitoe mikopo zaidi ya siku 15 ili na wao waweze kuhimili huu utaratibu wa kulipa kodi ndani ya siku 15. Katika hili mimi naipongeza Serikali na sioni sababu ya kulalamika juu ya matatizo haya ya kusema siku 15 ni ndogo kwa walipa kodi wa mafuta kwa vile hususan mafuta si biashara ya kukopeshana, ni biashara mara nyingi ya *cash*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishauri Serikali juu ya ulipaji kodi ya mafuta yanayokwenda nchi jirani. Ni vema Serikali ikawa na usimamizi mzuri wa biashara ya *transit*, iwapo Serikali itaona inafaa, uwekwe utaratibu wa kuwasiliana na nchi hizo ili wawe wanathibitisha mafuta yao nchini mwao kwa taratibu za kwao na kwamba kodi ambayo italipwa kwa wale wanaoingiza mafuta ya *transit* iweze kurejeshwa ndani ya siku 15. Kwa hiyo, pia hilo naiomba Serikali waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine pia naishauri Serikali iangalie mianya mingine wanayoitumia baadhi ya Taasisi katika ukwepaji kodi katika haya mafuta kama vile miradi ya kujenga barabara, miradi hii ya makampuni yanayojenga migodi na Taasisi nyingine za Kidiplomasia za Mabalozi pia huku kuna mianya nako ya ukwepaji kodi ya mafuta, kwa hiyo Serikali ilipaswa nako iangalie. (*Makofi*)

Napenda nimalizie jambo moja, Serikali ni vema pia ikaangalia haya makampuni yanayofanya biashara ya mafuta kienyeji hasa yakikutwa hayana vifaa kama vya zimamoto. Pia Serikali inapaswa ilyaangalie ili yaweze kusimamiwa na kuyabana ili yasifanye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nianze moja kwa moja na mimi kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, walioingia katika Bunge hili kutokana na uchaguzi mdogo uliopita. Lakini niwapongeze zaidi Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, walioingia ndani ya Bunge hili kupitia Chama cha Mapinduzi hasa wale kutoka Majimbo ya Kigoma Kusini, Mpanda, Bukoba Vijiji na Kilombero. Naomba na mimi niungane na wenzangu katika kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti yetu kusema kweli ni nzuri na mimi ninaziunga mkono hoja zote mbili. Kusema kweli Bajeti hii inaleta matumaini kama itatekelezwa

kama ilivyowasilishwa hapa mbele yetu na Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza lakini kwa ushauri tu kwamba, ni vema mambo fulani fulani ndani ya nchi yetu yakaenda vizuri zaidi kuliko yalivyo kwa sababu kwanza sisi si nchi maskini ila ni nchi tajiri. Hii ni nchi tajiri kwa sababu raslimali zake ni nyingi lakini matumizi yake ni mbaya. Ushauri mwangi unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kwa njia ya kuboresha tu ili huko mbele tunakokwenda tuwe na Tanzania iliyo bora zaidi, maana maendeleo hayana itikadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizungumza kwamba, *future* ya nchi yetu inahitaji tuwe *tactical, selective and very careful* na matendo yetu ni muhimu sana kuweza kui-direct *future* ya nchi hii. Sasa naomba nimpe pole Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, kwa kufanya kazi ngumu sana katika Taifa hili. Nilikwishasema katika Bunge hili kwamba, *you can not have effective planning without a Budget function*. Lakini ni ushauri wangu kwa muda mrefu umekuwa tunahitaji sasa kuwa na *a National sink tank*, kwa sababu *current planning mechanism is efficient and ineffective, for obvious reasons of our own making*. Unakuwaje na *Planning Commission* isiyokuwa na *Commissioners* katika nchi yenye *serious inter-ministerial collaboration?* (*Makofi*)

Mipango tulionayo ni ya zimamoto, duniani watu wanaishi kwa malengo na huwezi kuwa na malengo kama huna mipango mizuri, tena katika hali ya utandawazi mipango hii inatakiwa iwe mizuri kweli kweli. Pia nilikwishasema ya kwamba kuna *a weak link between policy and practice* katika nchi hii na ni muhimu kwa hiyo, katika Taifa letu *to define parameters of the National Economy*. Ni kweli lazima tuelewe habari ya dunia, lazima tuelewe habari ya *globalization, IMF, World Bank* na *WTO*, lakini kufanya hivi tunahitaji kuwa *tactical, selective and very careful* kama nilivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *the mercenary of future development* ya nchi hii has been given to us kama wanasiasa. Kama hii ni kweli ni namna gani tunabebe mzigo wa maendeleo ya Watanzania na ni namna gani tunachukua mawazo mapya katika mchakato mzima wa maendeleo ya nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie kwenye *specifics*. Tumefanya nini na madini ya Taifa hili? Tumetoa tu wengine wakatajirika wala hatujali, hakuna kitu sisi tunachokipata, tutabaki tulivyo na umaskini wetu utaendelea. Je, hali hii tunaendelea nayo hivi hivi na tunakubaliana nayo hivi hivi, wakati tunawawakilisha watu maskini, tunatunga mikataba isiyofaa! Mwaka 1998 nilisema Mkataba wa Madini ulikuwa na kasoro nyingi, wale waliokuwepo mnakumbuka, mimi nilisema humu ndani. Nafikiri wakati sasa umefika wa kuingilia Mikataba yote ya Madini, ili sisi tuliookabidhiwa amana ya maendeleo ya Taifa, hili tuwajibike ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya nini na mali zetu zinazouzwa hapa, mashirika ya umma, nyumba za Serikali? *Our style is wrong, tufanye nini sasa?* Kama nchi, yako mambo ambayo yametokea, moja, tume-succumb to the class limitation of Post Independence African Nationalism, acting in collaboration with hostile transnational corporate and multinational process whose interests are opposite to our

Constituencies. Miaka 40 iliyopita sisi tulipopata uhuru kulikuwa na mtu mmoja anaiyetwa *Frans Fanon*. *Frans Fanon* aliandika katika kitabu chake “*The Rest of the Earth*” na alisema: “Sisi wote tulipo humu tunaweza kujia *middle-class* lakini *middle-class* waliopo humu ndani tunazidiana, wengine wamepanda kidogo ngazi”. Kwa hiyo wengine wamevuka ile wanayoita *the compra door class*. Sasa naomba mnivumilie, mimi msinipigie makofi kwa kweli. (*Kicheko/Makofi*)

Naomba niseme hivi: “*The National middle-class discovered its historic mission that of intermediary, seen through its eyes, its means has nothing to do with transforming the Nation*”. Ndiyo tunayofanya katika Taifa hili. Kama tungkuwa na utashi wa kisiasa wa ku-transform nchi hii siamini kama baadhi ya mambo tunayoyafanya tungeyafanya. Tunazungumza habari ya *globalization, globalization* iliyoja *lack of transparency, IMF* iliyoja *lack of transparency* na *World Bank* iliyoja *lack of transparency*. Wanakwambia kafanye hivi wewe unasema nimeambiwa na hawa na lazima niwaambie Wabunge wangu haya ndiyo yenyewe, siyo yenyewe! Leo mbona tunesema tunatoa *subsidy* kwa mbolea na tungetoa kwa nchi nzima, tunatoa Mikoa minne tu kwa nini, *who is saying that?* (*Makofi*)

Tumewaliuza kwamba watu wetu ni maskini sasa tunataka kuwapa *subsidy* wamekataa, maana tunawaambia na sisi sababu zetu. Bahati mbaya mimi ni *supporter* wa kitu kinachoitwa *the large list approach to economic reform*. Hii tunayofanya ya *shock therapy* itatupeleka kubaya Watanzania. Malalamiko dhidi ya uwekezaji ambao uko Tanzania katika maeneo kama madini, *TTCL, NBC, IPTL* na sehemu nyingine, katika mtazamo wangu ni ya kweli na yanahitaji kufanyiwa kazi. Hawa Waheshimiwa na wenyewe wameandika kuna kitabu hapa ambacho ninacho, ngoja niwasomee kidogo wanavyosema, nina kitabu kinachoitwa *Globalization and its Discontents*, nitasoma page moja tu *page 71*.

MBUNGE FULANI: Yote?

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Hapana, *paragraph* moja. Anasema: “*There is more to the list of legitimate complaints against its foreign direct investment. Such investment often flourishes only because special privileges extracted from the Government are given. While standard economics focuses on the distortion of the incentives that resulting from such privileges, there is a formal insidious aspect often more privileges as a result of corruption, the bribery of Government officials*”.

Namaliza *quotation* yangu kwamba, kama tungkuwa tunayafanya yote haya *sincerely*, leo kweli tunapanga mipango ya Taifa hili tunasema yote yanakwenda vizuri watu wanalamika hapa, tukitoka hapa ni mambo *as usual* haiwezekani, lazima kuna kitu, rushwa. (*Makofi*)

Nimewapongeza Waheshimiwa Mawaziri wangu na mimi nina imani wanafanya kazi kubwa, kama ningeruhusiwa kuzungumza hata saa moja ningemaliza, lakini niseme hivi, hivi kwa nini miradi mikubwa na mizuri ambayo tunazungumza tunasema hii ndiyo iwekewe kipaumbele kama *Stigler's Gorge*, ambayo ingetupa umeme katika Taifa hili na

umeme ndiyo chanzo kikubwa cha maendeleo ya Taifa hili, leo tunaambiwa tunazungumza tu kama linapita linapita. Tunazungumza habari ya Mchuchuma, ninyi mnakwenda mnasema Songo Songo gesi kwa sababu Benki ya Dunia wamesema, wanatu-*miss direct*, kule tunakwenda siyo kuzuri na mipango ya nchi hii ni kama nilivyosema ya zimamoto, tunakwenda kwenda tu. (*Makofi*)

Sasa *Mtware Corridor* wakati mmoja hapa ilikuwa ni *real issue*, ikaenda sasa hivi imepoa, hatuisikii tena, habari ya Mchuchuma inaanza kufisia! Hivi mamilioni tunayotumia kutupa *we are actually losing these money, is bad. IPTL* pesa tunazozitupa na hatujali kama tunataka kuelewa nani alifanya hivyo. Ujenzi wa barabara ni wa maneno, tumeipongeza Serikali kwa sababu kweli imejenga barabara kwa jitihada sana lakini tunahitaji *focus* inayotupeleka kwenye maendeleo. Tumesema fungueni mipaka yote ipitike ili Mikoa ya pembezoni nayo iingie katika kushirikiana na Mikoa mingine, hayo yatuyaoni. *Development funds* zinazokuwa *allocated* kwa Mikoa hii *very negligible*, hazistahili kuzungumzia kwamba tunapeleka maendeleo huko. (*Makofi*)

Nimalizie kwa kuzungumza neno moja tu. Watu wakikosea sijui kama tuna *collaborate* nao, watu wakikosea tunazima moto eti ili watu waone kwamba tumefanya *action*. Leo hii tumekuwa tunazungumzia sakata ya mchele bandarini, sasa nasikia wamemfukuza kazi na kumfungulia mashtaka Katibu wa *Counterpart Fund*, lakini uamuza wa kutoa tenda ulikuwa wa huyu mtu mmoja? Haya ndiyo tunayoyaauliza. Kuna mambo mengi *which don't make sense in the eyes of a listener* na sisi ndiyo tunaowawakilisha watu maskini, tunawatetea ipasavyo?

Hata hawa ndugu zangu walioko mbele, wote ni marafiki zangu, haya tunayofanya ndio yenyewe au ni aibu kwa Taifa hili? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ni aibu.

MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana wale Mawaziri ambao wamekuja na *revolution* za kutengeneza bajeti nzuri lakini yako mambo ambayo kwa kweli tutawaomba wazidi kuendelea kuyaangalia na kisha wazidi kusafisha njia kwa CCM mbele ya safari. Maana kwa kweli tunavyozungumza CCM ni Chama ambacho kimezoea kujikosoa na tutaendelea kujikosoa, tutaendelea kukosoana ndani ya Chama cha Mapinduzi mpaka tufike mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ningepewa saa nzima ningeendelea na mengine, ningezungumzia mipango mbalimbali. Lakini kwa sababu muda hakuna na mimi huwa sipendi kupigiwa kengele, naomba nikushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KIDAWA H. SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu ingawa baada ya Waheshimiwa Wabunge wengi kuchangia, kwa kweli najikuta nimefilisika. Lakini hata hivyo, nitachangia tu mchango wangu wa jumla jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu wa Mipango na Fedha, kwa mipango yao mizuri na bajeti waliyoandaa. Kwa kweli ni bajeti ambayo imeandaliwa kuwatumikia wananchi walio wengi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa upande wa Wizara ya Mipango. Sehemu ya kwanza nitachangia kuhusu ukuaji wa Pato la Taifa na umaskini. Napongeza jitihada za Serikali na hatua mbalimbali inazochukua ili kufanya uchumi wetu ukue na hatimaye kuleta maendeleo kwa azma ya kupunguza umaskini uliokithiri katika nchi yetu. *Trend* inaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 1997 Pato la Taifa limekuwa likikua. Katika mwaka 2002 limefikia kiwango cha asilimia 6.2 na kiwango hiki kilivuka lengo lililowekwa kwa mwaka huo kwa 5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wote tutakubaliana kwamba kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi bado hakitoshi kupunguza lile tatizo la umaskini ambalo tunalo. Ripoti nyingi za kitaalam zimeonyesha kuwa tatizo la umaskini bado lipo na limejikita zaidi kule vijijini, labda katika Jiji la Dar es Salaam ndio kuna dalili za kuonyesha kupungua kwa baadhi ya familia. Aidha, ile tofauti ya kimapato baina ya familia inazidi kuongezeka. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kufanya ili kutatua tatizo hili zito na kuweza kufikia lile lengo ambalo tumeliweka katika Dira yetu ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mikakati na mipango mizuri imeandaliwa kwa ajili ya kushughulikia suala hili. Kwa hiyo, tunasisitiza kuwa ni budi Serikali itekeleze mipango na mikakati iliyowekwa ili kupunguza tatizo hili isiwe mikakati na mipango hiyo imo tu kwenye karatasi lakini tujitahidi kwa nguvu zetu zote kutatua tatizo hili kwa kutekeleza hiyo mikakati iliyowekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Serikali katika gawio lake kuna asilimia 42 zimekwenda katika kuboresha sekta za kijamii na vile vile katika kuboresha na kuimarisha sekta za kiuchumi kuna gawio la asilimia 16. Kwa maana hiyo, mwishoni mwa mwaka tunataka tuje tuambiwe fedha hizi zimetumikaje. Ni kweli zimetumika kwa mipango iliyowekwa ya kuimarisha sekta hizi na sekta hizi zimeimarika kwa kiasi gani? Tusije kuletewa ripoti kwamba kuna upotevu wa fedha za Serikali, fedha zimeenda na maji. Fedha haziwezi kupotea kwa sababu sio mtu wala si mnyama kama atapotea njia. Kwa hiyo, suala la kutumia fedha hizi kinyume na mipangilio iliyowekwa labda zimekwenda kuboresha sekta za matumbo ya watu, jambo hili lidhibitiwe kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la ajira. Kwa kweli kama wenzangu walivyozungumza, kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi angeweza kufanya kazi tatizo la umaskini lingeweza kupungua, lakini hali halisi sivyo ilivyo. Tumeelezwa kuwa kuna Watanzania milioni 2.3 ambao wamekaa tu hawana kazi na wanakaa vijiweni na kuzurura bure. Hili ni tatizo. Watu hao kwa kweli wanabebesha mzigo wale wenzao ambao wanavuja jasho na kufanya kazi. Wanawabebesha mzigo kwanza kwa kuwashudumia wengine wanaotoka katika miji na vijiji mbalimbali wanakuja Dar es Salaam kwa sababu tumeambiwa karibu asilimia 46.5 ya watu wasio na kazi wako pale

Dar es Salaam. Kama ni *extended family* wanaishi kwa wenzao na wanawabebesha mzigo wa kimaisha kwa kweli kwa sababu inabidi wawasadie kuwahudumia, hiyo ni kuwasaidia *directly*. Lakini *indirectly* vile vile wanabebesha mzigo wenzao wanaofanya kazi ya kuwahudumia kwa njia ya kodi. Wale wanaofanya kazi ndio wanaolipa kodi na wao wapo tu kutumia zile huduma za jamii bila mchango wowote. Kwa hiyo, ni lazima suala hili litafutiwe dawa. Tumezungumza kuna ardhi nzuri, bahari na maziwa watu hawa wasaidiwe na kuweka vivutio vya kutosha waende wakajajiri katika sekta hiso. Aidha, tuimarishe viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda na mboga mboga ili watu hawa waweze kwenda kujajiri huko badala ya kukaa na kuzurura ovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la uzururaji ni tatizo sugu sana kwa sababu ndani yake ndiko kunazaliwa wizi, ujambazi na vibaka. Watanzania hawaishi kwa amani kutokana na tatizo hili. Kwa kweli sisi wengine ambao tuna woga tunaotoka kule Zanzibar ukifika pale Dar es Salaam pengine kuna mikutano ya Kamati ukimaliza Kamati zako ukirudishwa hotelini saa kumi na mbili hutoki tena, hata upigwe rungu toka nje hutoki unaogopa. Kwa hiyo, tunaishi kwa wasiwasu kutokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Ubinafsishaji ni Sera za Chama cha Mapinduzi na tumezipitisha kwa nia nzuri tu ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya wananchi. Lakini kuna baadhi ya malalamiko yanayotolewa na wafanyakazi wanaofanya kazi katika mashirika haya ambayo yamebinafsishwa. Juzi tu nilipokuwa nikisoma gazeti niliona wafanyakazi wanalamika wanasesma kuna mtindo wa hawa wawekezaji kuajiri ajira za mikataba mifupi mifupi. Unamwajiri mtu miezi mitatu halafu unamwajiri tena kwa mkataba wa miezi mitatu kwa kuwa unakimbia suala la kulipa mafao ya baadaye. Pia kuna tatizo pengine ni mtaalam alikuwa anafanya kazi pale anaachishwa kazi lakini mtaalam yule yule anakuja kuajiriwa kwa mkataba wa muda mfupi. Hili ni tatizo ambalo inabidi tuliangalie. Kuna lingine, hata kama kuna kada ya utaalam pale pale na mtaalam alikuwa anafanya kazi anaachishwa kazi na kuchukuliwa mtu kutoka nje anakuja kufanya kazi zile zile ambazo yule mtu alikuwa amazifanya kwa ufanisi mkubwa zaidi. Vile vile kuna ubaguzi wa mishahara. Mtaalam wa kada moja analipwa tofauti na mtaalam mgeni anayefanya kazi ile ile na uzoefu ule ule na utaalam ule ule. Tatizo hili lipo. Aidha, kuna tatizo la kuwafukuza kazi wanawake kwa sababu tu ni wanawake sio kwa sababu wameshindwa kufanya kazi. Kwa hiyo, haya malalamiko ni lazima tuyafuatilie tuangalie ukweli uko wapi na hatimaye tupitie hii mikataba ya watu hawa ili kuhakikisha kuwa wananchi wetu hawadhalilishwi katika nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda Wizara ya Fedha, naipongeza Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri inayofanya na hasa *TRA* kwa kweli inastahili pongezi imejitahidi sana. Lakini hapo isiwe kikomo tunaamini kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa mapato kama tukijitahidi kuziba hii mianya ya wakwepa kodi. Nakubaliana na Mheshimiwa Isaac Cheyo, aliposema kuwa hawa wakwepa kodi wakubwa watangazwe, wawekwe wazi kwenye *public* kwa sababu hawa ni wahalifu kwa sababu ukwepaji kodi ni uhalifu kwa nini tuwafiche? Tuwatangaze na tuwape adhabu zote zilizomo katika sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa kubadilisha hivi viwango vya *Presumptive Income Tax*, kwa kweli ilikuwa ni kero wafanyabiashara wadogo walikuwa wanatozwa kodi hii kubwa mno ambayo hawawezi kuibeba. Kule Zanzibar wafanyabiashara wadogo walikuwa, akina mama na wenye magari ya daladala waliniufuata unajua kule Zanzibar magari ya abiria yamekuwa mengi kuliko abiria wenyewe. Kwa hiyo, utakuta magari yanapangiwa zamu unakwenda leo kesho unalala. Sasa ole wako gari yako iwe mbovu kwani gari ikiharibika inabidi hata zile siku 15 za mwezi huwezi kufanya kazi hatimaye unajikuta kipato chako cha mwezi ni kidogo mno na kwa mwaka hakifiki hata shilingi milioni mbili wakati unatakiwa ulipe Sh.70,000 kwa mwaka na kuna leseni, *road licence* na madudu mengine chungu nzima, ambayo mtu huyu anatakiwa kulipia. Pia ukiangalia kwamba Wanzanzibar tunaza sana katika familia moja utakuta kuna watu zaidi ya tisa, huu ni mzigo mkubwa mtu anashindwa kuwashudumia wale vijana wake katika familia. Kwa hiyo, nakupongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la *Excise Duty*, naipongeza Serikali kwa kuongeza kodi katika vileo. Kuna *principle* ya kodi ambayo inasema *tax heavily commodities which are complimentary to leisure* na hivi vileo, sigara, mambo ya music yote haya hata ukitoza kodi vipi watu watanunua tu, wanywaji watakunywa tu. Kwa hiyo, hili nalipongeza, kimapato hili ni sahihi kabisa. Lakini vile vile tuangalie upande wa pili, maadam watu hawa wanaendelea kunywa na kwamba kipato cha familia kikibakia kile kile kwa maana hii kodi inaweza kuathiri ile *expenditure pattern* ya ile familia. Kwa hiyo, baada ya muda fulani tujaribu kufanya *study* tuone uamuzi huu umeathiri VIP familia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili tatizo la Ushuru wa Forodha kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Ni kweli wafanyabiashara wanalamika wanapopitisha mizigo yao kule Zanzibar wanalipa, wanachekiwa kila kitu, wakiletu huku wanapata bughudha. Kwa hiyo na hili sio la kulinyamazia lifanyiwe uchunguzi na likionekana ni sahihi litafutiwe matibabu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuweka kodi katika mifuko ya plastiki. Kwa kweli naipongeza Serikali yaani hii mifuko ya plastiki imekuwa ni kero mazingira yamechafuka kweli kweli. Ukienda kule Zanzibar unarukiwa na ile mifuko kwa sababu inapeperuka kama *balloon*. Kwa maana hiyo, naipongeza Serikali kwa sababu sasa ile mifuko yetu ya vijijini kwa mfano mikopo ya ukili, vikapu na vinginevyo vinaweza vikapata soko, kwa sababu vilikosa soko sababu ya mifuko hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lile la *harmonization* ya *tariff rate* baina ya Zanzibar na Bara. Tumekubaliana vizuri na kwa kweli ilikuwa mkataba mzuri tu kule Zanzibar wamekubali kuweka uwiano sawa wa kodi hata kwa zile sheria ambazo zimetungwa na Baraza la Wawakilishi, mojawapo ni Sheria ya *VAT*. *VAT* sio Sheria ya Muungano, kuna *VAT* tulioitunga hapa na kuna *VAT* imetungwa na Baraza la Wawakilishi. Lakini kuweka *harmony* katika mambo haya tumekubaliana. Mgao wa kimapato *issue* hii itashughulikiwa na Tume ya Fedha iliyoundwa juzi. Lakini kuna watu ambao waliathirika hapa kiajira, wale ambao walikuwa wanategemea mapato yao kutoka

kule Bandarini kutokana na kupakua mizigo iliyokuwa inaingia kule Bandarini. Kwa hiyo hili suala nalo liangaliwe namna gani watu hawa watatafutwa na kuweza kusaidiwa hata kama kwa kuwapatia hii mikopo midogo midogo waweze kujisaidia wao na familia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la UKIMWI na athari za UKIMWI mojawapo ni watoto yatima. Jana asubuhi tuliuliza swali tukataka kujua hivi tunaweza kujuaje idadi halisi ya hawa watoto yatima? Tukaambiwa haijulikani tunasubiri wafadhili waje tufanye kazi, tufanye utafiti. Lakini ningeshauri *structure* zilizokuwepo za *Government* ambazo ziko mpaka huko vijijini zitumike kwa sababu watu wako vijijini, Maafisa wako kwa nini mtu akifiwa na baba na mama yake kusiwe na sehemu maalum ya kwenda kujisajili. Hiki kitu sio lazima tusubiri fedha za wafadhili sisi wenyewe tunaweza tukakifanya vizuri tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala moja la mwisho kuhusu *revenue retention*. Nilikuwa nikipitia vile vitabu vyta bajeti nimeona kuna maeneo mengine hasa Polisi kuna sehemu ya mapato inatakiwa ibakie kwa matumizi yao lakini kwa kule Zanzibar nimeona pale ni *zero percent*. Sasa hivi kule Zanzibar hatukusanyi mapato au kwa nini haikuungizwa katika utaratibu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. NAZIR M. KARAMAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza baada ya kuchukua kozi ya takriban wiki moja hivi nikiwa katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wabunge wapya, nikiwa na uhakika sana kwa wale watokanao na tiketi ya CCM, kwa mapokezi yenu mema tuliyoyapata hapa Bungeni. Vile vile napenda kutoa shukrani kwako wewe Naibu Spika na naomba uzifikishe kwa Spika mwenyewe na Ofisi yenu kwa maandalizi mazuri mliyotuwekea hasa kutupatia miongozo mbalimbali na maelekezo ambayo tuliyapata kwa maandishi na kwa maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, kikao chetu cha kwanza tulichohudhuria hapa lilikuwa darasa tosha la kuweza kutusaidia na katuonyesha mambo gani sisi kama Wabunge, inabidi kuyazingatia kama wawakilishi wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Bukoba Vijijini, napenda kuwasilisha pongezi zao kubwa kwa Serikali kupitia kwa Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, kwa bajeti inayobatizwa na haya maneno nimeyapata kutoka Jimboni kwetu, hii bajeti inabatizwa kwamba ni bajeti ya watu (*Peoples Budget*), kwa mwelekeo wa bajeti unaowajali wananchi hasa wale wenye kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuwaondolea Kodi ya Maendeleo ambayo kwa wengi ilikuwa ni kero tu kwani mchango wake ulikuwa ni mdogo sana na tamko la kukusudia kuondoa kodi nyingine zenyenye kama hiyo limepokelewa na wana Jimbo la Bukoba Vijijini kwa furaha na shangwe. Kitendo hiki kimechukuliwa kama uthibitisho tosha wa kuonyesha jinsi ambavyo Serikali inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, kwa kuwapunguzia wananchi kero na inapowezekana kuziondoa kabisa. Hatua hii iliyo chukuliwa na Serikali itakuwa ya manufaa zaidi kama itatumwa kuwa kichocheo cha kuwawezesha wananchi kushiriki ipasavyo bila hofu au woga katika shughuli za maendeleo ili kuongeza maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja mbili zilizo mbele yetu, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga, kwa nafasi walizoteuliwa na vile vile kumshukuru Ndugu Senare na kumtakia afya njema na kazi njema kwa kazi alizopangiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, sasa napenda kuchangia mapendekezo ya hotuba za mipango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 kwenye vipengele vifuatavyo: Kipengele cha kwanza ni dhamira ya Serikali kuanzisha Benki ya kuhudumia wavuvi, wafugaji na wakulima. Napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha chombo kama hiki ili kuhakikisha kuwa sekte muhimu kama hizi ambazo zinahusisha zaidi ya 80% ya Watanzania hazidumai kwa sababu ya kukosa mitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kushauri kuwa kwa kuzingatia uwezo wetu mdogo tulionao, ni muhimu sana kutumia raslimali ndogo tulizonazo kwa ufassaha na maarifa. Kwa hiyo, ni vema kuepuka uundaji wa utiriri wa vyombo vyenye madhumuni yanayofanana maana tukifanya hivyo tutakuwa tunatumia raslimali zetu vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pendekezo ambalo samahani Waheshimiwa Wabunge kidogo ni tofauti ne wale waliopendekeza kuwa *NMB* ibadilishwe na kuwa Benki ya Wakulima. Tofauti yangu hii inatokana na kuelewa kwangu kuwa *Micro-finance* kama shughuli ya *ki-macro-finance* bado ni muhimu katika maendeleo ya Taifa hasa wakati huu wa mpito tukielekea urchumi wa kibepari. Kwa wakati huu umuhimu wa *Micro-finance* hatuwezi kuupuuza au kuuweka chini. Kuanzishwa kwa Benki inayokusudiwa na Serikali kusiwe na maana ya kuua madhumuni na sababu zetu za awali za umuhimu wa kuwa na *Micro-finance Bank* yenye majukumu ya kuwahudumia wafanyabiashara wadogo wadogo, wenye miradi au viwanda vidogo vidogo (*Micro-enterprises*), wafanyakazi, huduma za Kibenki kwa wananchi wa kipato cha chini na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa *NMB* tuiache kama *NMB*, lakini Mikoa au Wilaya ambazo tayari kuna Benki za Wakulima kwa mfano, Benki ya Wakulima ya Kagera basi badala ya Serikali kuunda chombo kingine, nguvu iwekwe katika kuziwezesha Benki hizi kimitaji na wataalam. Nina hakika kuwa madhumuni ya

Benki hizi na yale yanayokusudiwa na Serikali yanafanana hivyo ki-nchi raslimali za wadau wote zitakuwa zimetumika kwa ufanisi (*efficiently*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho napenda kuchangia ni kipengele ambacho kimezungumziwa sana cha shilingi yetu kupungua thamani. Katika mfumo wa uchumi huria ambao nchi yetu imeukumbatia pesa ya nchi hupungua thamani pale inaposhindwa kuhimili mikiki (*pressure*) ya currency ya nchi nyingine. *Currency* ya nchi ikishuka basi huvutia bidhaa za nchi ile kuuzwa kwa wingi nje hivyo ina *encourage exports*. Hivyo sishangai kuona kuwa tuliiza zaidi mwaka 2002 baada ya thamani ya shilingi yetu kuporomoka. Pamoja na kuunga mkono pendekezo lililotolewa na Wabunge wenzangu la kuziba mianya yote ambayo inaweza kutumika kutorosha fedha za kigeni kutoka nchini mwetu au kuweka vipingamizi uagizaji wa bidhaa zisizo za muhimu kwa pesa za kigeni, bado nasisitiza kuwa naungana na Mheshimiwa Mwandoro kwamba, kazi kubwa kwetu iko katika uzalishaji wa mali za kuuza nje (*exports*). Tukifanikiwa ipasavyo kwa hili nina hakika mikiki inayoipata shilingi yetu itapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kipengele cha *Privatization Trust* ama *Unit Trust* kama itakavyobadilishwa. Chombo hiki ni muhimu sana na nakubaliana na madhumuni ya Serikali kuunda chombo hiki kama njia pekee ya kuwawezesha Watanzania wa kipato cha chini kwa sababu zifuatazo: Kwanza, wananchi wa kipato cha chini wataweza kushirikishwa kumiliki hisa katika makampuni yaliyobinafsishwa na Serikali. Pili, wananchi wa kipato cha chini wataweza kushiriki hata kama ni *indirectly* kwa sababu hizi ni *Unit Trust* katika ununuzi na uuzaaji wa hisa na amana mbalimbali zinazouzwa au zinazonadiwa katika minada ya masoko ya hisa. Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kuwa waliofaidika na hisa za Serikali zilizobinafsishwa kupitia Soko la Hisa la *Dar es Salaam Stock Exchange* ni Watanzania wachache tu na sana sana waishio maeneo ya mijini. Watanzania walio wengi hasa waishio vijijini hawana habari na mipango hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo katika utekelezaji wa *Unit Trust of Tanzania*, napendekeza mambo yafuatayo yazingatiwe. Kwanza kama Wabunge wenzangu walivyoshauri, suala la elimu kwa wananchi kwa ujumla ni muhimu sana na elimu hii iteremshwe chini hata ikiwezekana katika ngazi ya vijiji. (*Makofi*)

Pili, kwenye makampuni yaliyobinafsishwa na Serikali tayari inazo hisa ilizobaki nazo, basi kati ya hizo hisa zilizobaki kwa Serikali, napendekeza hisa ambazo zitatengewa hii *UTT* zijulikane toka awali ili *UTT* nao waweze kuweka mipango yao ya muda mrefu. (*Makofi*)

Tatu, napendekeza kwamba *UTT* iwe na muundo wa Kitaifa utakaozingatia kuwa walengwa ni wakulima, wavuvi, wawindaji na wafanyakazi wa kipato cha chini, wafanyabiashara wadogo wadogo ambao kwa ujumla wao ni asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania. Kwa hiyo, *UTT* itabidi wajitahidi sana na vishawishi vyta kuwa na miundo rahisi kiutawala ambavyo vinaweza kuishia kuwashudumia wachache tu hasa waishio mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimeshagongewa kengele, itabidi vipengele vingine niviache, napenda kuzungumzia kipengele ambacho ni cha muhimu sana nacho ni umeme vijijini. Wakati nasikiliza mchango toka kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimeshangaa kusikia mmoja wao akisema kuwa Jimboni kwake kumebaki vijiji viwili tu au vitatu havijapata umeme. Wakati nampongeza Mheshimiwa Mbunge husika kwa mafanikio hayo waliyoyapata Jimboni kwake, nasikitika kusema kuwa Jimboni kwangu mambo ni kinyume kabisa, zaidi ya asilimia takribani 95 ya vijiji vya Jimbo la Bukoba Vijijini havina huduma ya nishati hiyo. Marehemu Mheshimiwa Kinyondo, alikuwa amekwishawakilisha ombi hili mbele ya Serikali na kwa sababu mimi ndiye mrithi halali basi nakumbusha ombi hili tena. Kati ya mambo mawili makubwa waliyonitura wananchi wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kipaumbele wamekitoa kwa suala la umeme. Wanajua fika kuwa changamoto ya maendeleo haiwezekani kupatikana bila nishati hii na maendeleo yao yataendelea kuwa nyuma kulinganisha na Majimbo jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nina dakika moja au mbili, nitaendelea kuchangia suala la bajeti kuunga mkono zao moja la kilimo na zao moja la chakula. Sote tunakubali kwamba Serikali haina uwezo wa kuunga mkono bajeti mazao yote kwa sasa Serikali najua haina bajeti ambayo inaunga mkono zao lolote hapa nchini. Kama nimemwelewa vizuri Waziri, Serikali kuunga mkono bajeti zao moja haina maana ya kuacha mazao mengine pamoja na Serikali kuunga mkono zao moja la biashara na moja la kilimo mazao mengine basi yaendelee kwa mtindo ambao tunao sasa hivi. Kama mwanzo tuishukuru Serikali kwa wazo hili na sisi kama wawakilishi wa wananchi, tulilieleze Majimboni kwetu kwa mtizamo mzuri (*Positive Attitude*) itakuwa vigumu kuwaeleza wananchi kuwa Serikali ilitoa nafasi ya ku-support bajeti angalau zao moja la chakula na moja la biashara na sisi Wabunge tukakataa. Nguvu za kujitegemea katika bajeti hii zikikua huenda huko siku za usoni mazao mengi muhimu yakaingizwa kwenye mfumo huo. Namwomba baadaye Waziri aeleze kama tafsiri yangu hii ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja hizi mbili za Serikali mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja mbili za Waziri wa Mipango, pamoja na Waziri wa Fedha. Lakini awali ya yote ningependa niwapongeze Wabunge waliochanguliwa katika chaguzi ndogo zilizopita, nawakaribisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyochangia ni bajeti ya aina yake. Katika historia nadhani ya nchi yetu bajeti hii imekuwa ni ya kuwajali sana wananchi kwa maana ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kwa uzuri wa bajeti hii wananchi wengi wameshaanza kuandamana kuipongeza Serikali kwa hilo. Juzi Mwanza kulikuwa na maandamano, wananchi kuitia Chama cha Mapinduzi wamefanya maandamano

wanaipongeza Serikali. Pia jana nilikuwa naongea na Mkuu wangu wa Wilaya, anasema wananchi wa Geita wanapanga kufanya maandamano ya kuipongeza Serikali kwa sababu ya bajeti hii nzuri sana ya mwaka huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo limekwenda moja kwa moja kwa wananchi ni lile la kufutiwa kodi ya maendeleo. Kodi ya maendeleo kwa kweli ilikuwa ni kero na sisi tumesema sana hapa Bungeni kwa sababu Watendaji wa Kata, ambao walikuwa wanafanya kwa kulazimishwa na masharti ya kazi yao walikuwa Miungu watu. Mimi katika Jimbo langu nimewahi kuona matukio mawili ya kusikitisha sana.

La kwanza ni kwamba mgambo alitumwa kwenda kufanya msako, wakaenda kwa mwananchi mmoja ambaye alikuwa amealika watu kuvuna pamba. Wakavamia wale watu kwenye kazi ile ya jumuiya, wananchi wakakimbia wakaacha kuvuna pamba. Halafu tukio la pili ni kwamba katika nyumba moja kulikuwa na msiba, watu walikuwa kwenye matanga, lakini mgambo walivamia pale kufanya msako wa kodi na wananchi wakasambaa. Sasa hii ni mifano ya kero ambayo iliwapata wananchi na ndiyo maana watu wanaandamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo naomba niipongeze tena Serikali kwa kuwafikiria Watendaji wa Vijiji kuwapa ajira. Hawa mara nyingi walikuwa wanaishi maisha ya kufanya kazi ya kujitolea. Kwa sababu kuna Wilaya ambazo Halmashauri ziliwu haziwezi kuwalipa na wengine walikuwa wanlipwa kutokana na asilimia ya makusanyo yao ya kodi. Sasa kwa kuwa sasa watalipwa na Serikali Kuu nadhani sasa wataongeza zaidi kasi ya kusimamia maendeleo ya Halmashauri zao. Lakini pia ningeshauri hasa *WEOs*, Watendaji wa Kata, ambao kwa sasa hivi wanlipwa na Halmashauri zao ambazo nyingi zinakuwa hazina uhakika na mapato yao, wangewekwa kwenye malipo ya Serikali Kuu kama vile Watendaji wa Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kada moja hapa imesahauliwa, nayo ni ya Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani kwa *nature* ya kazi yao hakuna tofauti na Wabunge, Diwani ni Mbunge wa Kata yake. Anafanya kazi, anasimamia mapato ya Halmashauri yake, anapokea hata kero hizi ambazo Serikali imezifuta, anapokea matatizo, kwa mfano, tetemeko kama limo kwenye sehemu yake wa kwanza kuambiwa ni Diwani. Vile vile mafuriko, njaa, ukame na kila kitu na wanafanya kazi sana. Lakini sasa hawana mshahara na hawana mshahara kwa sababu sheria iliyopo ya Halmashauri ya Serikali za Mitaa haiwatambui kama wao ni waajiriwa wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba sana hawa wafikiriwe. Kwanza, kama Serikali imeamua kuwalipa mishahara Watendaji wa Vijiji ambao kwa mfano Wilaya yangu ya Geita kuna Watendaji zaidi ya 180, hawa wote watalipwa lakini Madiwani ni arobaini na tisa, ukitoa Wabunge wanabaki arobaini na nne. Sasa utashindwaje kulipa watu arobaini na nne na ukawalipa watu 180 na wakati wanafanya kazi hiyo? Sasa fikiria, Mtendaji wa Kata kwenye eneo lake analipwa mshahara, Mtendaji wa Kijiji analipwa mshahara, Katibu Tarafa analipwa mshahara, Diwani ndiyo yuko pale sijui anabaki kuwa ni omboomba au nani. Sasa ningefikiri hawa nao wawekewe utaratibu huo wa mshahara. Ni watu muhimu sana, tubadilishe sheria kama zipo ili tuwaingize kwenye

mishahara hawa Madiwani, sasa hivi wanategemea posho za madarasa kutoka katika Halmashauri zao. Lakini kuna Halmashauri zingine zina hali mbaya sana. Inaweza ikafika mwisho wa mwezi posho hakuna na Diwani anaendelea kufanya kazi, nadhani tuwafikirie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye suala moja ambalo ni nyeti sana na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisema hapa kuhusu Mikataba ya Madini. Mtu muungwana anapokuwa amekosea huwa anakubali kukosolewa. Nataka kusema kwamba, kama hapa Serikali ilitereza basi ikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijui kwa nini hata Benki ya Dunia haijaiambia Serikali kama imefikia hapa mpaka tunasamehewa madeni, tunafanya mazuri kwa nini hawajatuambia suala la Mikataba ya madini? Asilimia tatu ya mrahaba wameitoa wapi? Mlikwenda kuuliza nchi gani wanayofanya hivi? *South Africa* tumeambiwa ni asilimia kumi, *West Africa*, Senegal, Botswana ni zaidi ya asilimia tatu, hii asilimia tatu mliipata wapi? Ni huruma gani hiyo ya kuzidi hata huruma ya Mungu? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vitabu vya dini, mimi ni Mkristo wa *Roman Catholic*, tunasema kuna sheria ya Kanisa kwamba ulipe zaka kwa mwaka ambayo ni moja ya kumi ya mapato yako yaani ni *ten percent*. Kwa hiyo, Mungu anakwambia ulipe *ten percent*, sasa kama ni fukara au uwe vipi ni moja ya kumi ya mapato yako. Sasa kama Mungu hahurumii yule fukara wewe huyu tajiri unamfanyiaje huruma hiyo wakati huna kitu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetoka wapi hata zaka ni *ten percent*, sasa sisi *three percent* imetoka wapi? Jamani, zamani sana nilikuwa nasoma historia, wakati nipo shule ya msingi kwamba, zamani huko enzi za mababu zetu, enzi za giza, walikuja Waarabu wakachukua pembe za ndovu na faru, wakawapa shanga, wanabadilishana pembe za ndovu na shanga na zeze. Sisi tunasoma, tunashangaa sana. Sasa hapa baada ya miaka ishirini historia ikiandikwa kwamba walikuja wawekezaji wakachukua madini na mchanga wote wakatoa asilimia tatu, watatushangaa. Tufike mahali Serikali isione aibu wala kigugumizi, Mikataba ije hapa, ipitie kwenye Kamati, Bunge lifahamu, lishauri ili turekebishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu watu hawa tunasema pamoja na kwamba wanachukua bure tunawasamehe kodi kwa miaka mitano. Nao ni wajanja kweli, kuna Mkataba mmoja kwenye kampuni moja nadhani ni Ashanti, walifunga sina hakika zaidi, mwaka 1999 walifunga Mkataba na Serikali. Lakini hapa katikati nadhani leseni imebadilishwa sasa hivi wanaitwa *Geita Gold Mining*, mwaka 2001. Kwa hiyo, hapa ina maana kwa utaratibu wetu wale wa kwanza ilikuwa *Tax Hold* yao iishie mwaka kesho, lakini sasa kwa sababu wamebadilisha jina itabidi tena miaka mingine mitatu nadhani itaishia mwaka 2006, sijui sina hakika, lakini watakuwa wanachukua bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki ya jana wakati Waziri wa Fedha anatoa hoja yake alisema kwamba, unajua kuna msemo kwenye vitabu vya dini unasema kwamba mwenye kingi ataongezewa na mwenye kidogo atanyang'anywa hata kidogo alichonacho. Sasa

katika ukurasa wa 60 wa hotuba yake amesema kwamba amerekebisha kipengele namba 7 cha jedwali la tatu la Sheria ya Kodi ya *VAT* ya mwaka 1997, ili kuingiza *subcontractors* wanaoajiriwa na makampuni ya madini kwenye msamaha wa *VAT*. Hawa walikuwa wanalipa *VAT*, sasa nao wamesamehewa kama wale ambao wanachukua miaka mitano na *for your information* kuna malalamiko makubwa sana kwamba hawa wenye migodi hawaajiri *subcontractors* Wazalendo, wengi ni wa nje. Sasa ndiyo tunawapata tena bure. Naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Mikataba iwe wazi na tuifahamu. Mikataba inakuwa ya siri, kuna fununu kwamba katika Mkataba kati ya *Geita Gold Mining* na Serikali, mbali na mrahaba kuna sehemu wanapaswa kuilipa Halmashauri fedha fulani.

MBUNGE FULANI: Enhee, dola laki mbili kwa mwaka.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Naambiwa dola laki mbili kwa mwaka na kwa kuwa wame-*operate* sasa ni miaka minne, Halmashauri ya Geita inapaswa kudai dola laki nane. Sasa mbona halisemwi? Tunalia kila siku hapa barabara mbovu, maji hakuna, matatizo mengi, Serikali ipo kimya, kama mnafahamu mbona hamtuelezi hilo? Naomba Waziri mwenye dhamana wakati anafanya majumuisho kama ni kweli tunapaswa kulipwa hizo fedha atuambie hapa na kwamba ye ye mwenyewe atusaidie kuzidai ziingie kwenye Halmashauri ya Wilaya yetu na kama si kweli akanushe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa niingie kwenye suala la ulinzi na usalama. Nimpongeze sana Mheshimiwa Makamba, kwa kuwa na utaratibu mzuri sana wa kudhibiti ujambazi, lakini pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Jenerali Tumainieli Kiwelu. Yeye ameanza siku nyingi sana, amefanya *operation* mara mbili na sisi tumeomba sana hapa ifanyike *operation* kwani wapo Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi sasa hivi hawana kazi na wana silaha, magari na kila kitu. Ukiwatumia kwa kusaidiana na Polisi na Sungusungu wakafanya *operation*, itasaidia. Wamefanya *operation* Kagera na sasa hivi Kagera ujambazi hakuna. Sasa ndiyo hao wanakimbilia huko Dar es Salaam ambao wanatoka katika nchi zenyе vita. Nimesikia watu kutoka Kaskazini huko na labda kwa sababu kule Kagera sasa wameshadhibitiwa. Sasa tufanye basi kwa nchi nzima ili kupunguza suala la ujambazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Wilaya ambazo tunapakana na nchi hizo, kwa mfano, Wilaya ya Geita ni kubwa sana na ina watu laki saba, ina misitu na ina migodi. Kwa hiyo, majambazi hujificha sana lakini gari ya mpelelezi wa Wilaya ipo kwenye mawe na ni moja. Kwa siku gari inatembea kilomita mia tano, *allocation* ya mafuta kwa mwezi ni lita mia mbili, maaskari wanafanya *patrol* kwa miguu au kwa kuomba lifti kwenye magari ya abiria au ya Wabunge. Unawakuta pale wamenyeshewa mvua na *SMG* zao wanafanya *patrol*, kwa kweli unawahurumia. Naiomba Serikali, tafadhalii sana, tupeni magari angalau matatu, muongeze na askari, vitendea kazi, mafuta na *OC* kwa sababu mtu anayedaiwa sana na visima vya mafuta ni *OCD* na hawa ni lazima wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja ambalo limekuwa ni kero kwa wengi kuhusu Maveterani wa Vita ya Pili ya Dunia. Waliahidiwa kuna fedha zao kutoka Uingereza, *NGO* ya Uingereza imetoa kwa hawa Maveterani wapiganaji wa *KAR*, sasa hawa ni wazee na mpaka sasa hakuna fedha na Serikali haijatoa kauli ya kueleweka kuhusu hawa. Sisi Wabunge tunaulizwa, tunakuwa na vigugumizi, hivi fedha hizo ziko wapi? Waliambiwa kuna elfu tisini na sita kila mpiganaji atapata, wakaitwa Wilayani, wakaandikishwa majina, *Force Number* na wakafanya na *association* zao huko lakini mpaka leo hakuna kinachoeleweka. Naomba Waziri au Serikali wakati inatoa majumuisho, hebu toeni tamko kuhusu hawa wazee maana sasa hivi wanakufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwangu watatu wameshaaga dunia na waliobaki wanasema unaona sasa Mheshimiwa tunaziacha hela zetu. Sasa naomba mseme kama zipo au wafanye nini? Tuwaambie Wakuu wa Wilaya ili wawaambie, sisi tunakuwa hatuna majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze sana Serikali upande wa kilimo kwamba kila Wilaya sasa itatenga mazao mawili, moja la chakula na moja la biashara. Nilichokuwa naomba ni kwamba sasa mipangilio hii isiwe kwenye kitabu tu ifanyike kama ilivyoandikwa hapa. Tuangalie kitu kimoja, sisi katika Kanda kwa mfano, Kaskazini tuna misimu miwili ya mvua, mvua za vuli na masika, kwa hiyo, tunaanza kulima mwezi wa kumi. Sasa hii bajeti kama itatekelezwa mwaka kesho mwezi wa tatu, watu tumeshalima itakuwa haijatusaidia sana. Lakini napenda vile vile nimwambie Waziri wa Kilimo na Chakula kuna ukame mkubwa sana kwenye Wilaya yetu hasa kwenye Jimbo langu katika Kata ya Nyugwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili muhimu, hoja za Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha. Napenda kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao wameingia kwenye Bunge hili hususan Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Nawapa hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Ndugu Kitilya, pamoja na Ndugu Luoga, kwa kuteuliwa kwa nafasi ambazo wanazo. Pia nimshukuru Ndugu yetu Sanare kwa kazi nzuri aliyoifanya hadi kuifikisha *TRA* hapa ilipo hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabla sijaongea niunge mkono hoja kwa sababu naweza kusahau. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Dr. Kigoda, pamoja na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, kwa hotuba zao nzuri ambazo wameziandarda na mimi nasema kwa kweli kama wenzangu walivyosema, ni hotuba nzuri na ni bajeti nzuri. Lakini naomba niseme kwamba, tunapopongeza kitu hiki ni vizuri tukawa na *data* ambazo zinatufanya tunapongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bajeti zote zilizopita, ukisoma bajeti ya mwaka huu kila kitu kimeongezeka. Katika huduma za jamii tulikuwa na asilimia 39.2, mwaka huu tuna asilimia arobaini na mbili, huduma za uchumi zilikuwa ndiyo chini kabisa asilimia 2.8, safari hii tuna asilimia kumi na sita, utawala ilikuwa ni asilimia ishirini, sasa hivi ni asilimia ishirini na moja, ulinzi wa mzee wangu mzee Sarungi ilikuwa asilimia 11.8, sasa hivi ni asilimia kumi na nane. Kwa hiyo, hiyo inaonyesha wazi kabisa kwamba, bajeti hii kwa kweli mipango iliyowekwa ni mipango ya maendeleo, hakukuwa na lelemama kwa sababu isingekuwa imepanda, kwa hiyo ni mipango mizuri. Mipango ingekuwa mibaya mambo haya yote yasingeweza kutendeka. Kwa hiyo, naomba nimshukuru sana Dr. Kigoda, Wizara yake na wataalam wake wote, kwa mipango mizuri ambayo imewezesha kuonekana kwamba hali ya uchumi na masuala mengine yote yanakua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa na mimi nichangie yafuatayo kutokana na nilivyoipitia bajeti:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na hili suala la uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo katika hotuba ya Dr. Kigoda amesema moja ya kitu ambacho kimefanya hali ya fedha yetu ishuke thamani ni kasi ndogo ya mauzo ya nchi za nje na ningependa niseme kwamba katika hotuba ile Mheshimiwa Waziri alisisitiza kwamba bado kilimo ni uti wa mgongo na ni vizuri tunapoyazungumza haya pia tuongozwe na *data*. Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba, tunahitajika kufanya kazi kwa juhudili ili tuweze kuzalisha zaidi na tukizalisha zaidi maana yake Taifa litapata pato kubwa zaidi. Lakini *data* hapa zinatuonyesha kwamba katika mazao yote ya biashara katika nchi yetu, pamoa na kujisifia, bado hakuna hata zao moja ambalo limefikisha asilimia arobaini.

Labda ningetoa mifano hapa kwa mfano, zao ambalo linaongoza ni korosho, lakini uzalishaji wake ni asilimia 33.6, kahawa ni asilimia 27.7, pamba asilimia 26, sukari asilimia 16, tumbaku asilimia 3.1, mkonge wa kwetu Tanga ni asilimia 0.4, aibu. Kwa hiyo, unajikuta kwamba, kutokana na jinsi tunavyozalisha hatuwezi kutegemea kupata pato kubwa na fedha nyingi katika Taifa letu. Kwa hiyo, ni *challenge* kwetu kwamba, bado tuna kazi kubwa katika kilimo kuhakikisha kwamba, tunazalisha zaidi. Asilimia arobaini ni ndogo mno maana hata asilimia hamsini hatujafika, kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kufanya na kuhamasisha na kuweza kufufua mazao ya biashara ili angalau na sisi tuweze kupambana na wenzetu wengine. Kwa hiyo, ni *challenge* kwa Serikali kwamba bado tuna kazi kubwa.

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, *challenge* ambayo mimi naomba niiweke, ukitazama nitoe mfano mzuri, kama watu wangefanya kama ambavyo wenzetu wanafanya kwenye sukari, sukari lilikuwa ni zao ambalo linalegalega sana lakini ziara ambayo tulikwenda Kamati yetu ya Kilimo na Ardhi kule Kilombero na Mtibwa, ilitufanya tuweze kuona kwamba kwa kweli wenzetu wanafanya kazi. Kwa sababu unakuta Kilombero walipokabidhiwa wawekezaji, hapo ndiyo faida ya ubinafishajji, walikuwa wanatoa tani ishirini na tano, sasa hivi wanazalisha tani mia moja. Kule

Mtibwa walikuwa wanatoa tani kumi na tano, sasa hivi wanatoa tani thelathini na saba na mashamba yote yamelimwa na wakulima wadogo wadogo angalau wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe tu Serikali kwamba, kwa mazao mengine yote kama vile pamba, kahawa, korosho, tumbaku na mkonge, tujaribu kusukuma tuweze kupata tani nydingi zaidi. Mimi nasikitishwa kwa mfano, mkonge huko nyuma ilikuwa ni tani 260,000 kwa mwaka, sasa hivi ni tani 23,000 kutoka tani 260,000. Sasa haya ni mazao ambayo kwa kweli tungeweza kuyasukuma tukawa na mkakati mzuri ambao tungeweza kuinua uchumi na pato kubwa la Taifa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake pale amezungumza kwamba wale wawekezaji ambao wanaonekana uwezo wao ni mdogo wanyang'anywe mashamba, wapewe watu ambao wana uwezo wa kuendeleza mazao haya ambayo tumewapa hasa wale ambao wamepewa mashamba na wameweza kuwekeza, hii itatusaidia. Mfano mzuri ambao lazima niutoe ni mashamba ya *Mohamed Enterprises*, ambao wamechukua mashamba kule katika Mkoa wa Tanga na *Katani Limited* ambao wamechukua mashamba katika Mkoa wa Tanga, mashamba mengi mtu mmoja amechukua mashamba manane yana hekta labda elfu nne, hekta zilizolimwa ni elfu mbili na bado anatazamwa. Hivi tutafika kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hatuwezi kufika. Tufikie mahali Serikali iwe *serious*, ione toka mwaka 1990 umekabidhiwa shamba, umepewa hekta ngapi na hizo hekta ulizopewa umelima ngapi, umepanda ngapi na unavuna ngapi. Lakini kipindi cha muda wa miaka karibuni mitano, sita au saba hakuna uzalishaji na bado watu tunawatazama hivi kweli tunaitakia mema nchi hii? Naomba kwa kweli Serikali sasa ibadilike, wale ambao uwezo wa kuwekeza wameshindwa wanyang'anywe wapewe watu ambao wana uwezo wa kuzalisha ili mazao ya biashara yapande tuweze kupata kipato kikubwa zaidi katika nchi yetu. Hilo ni suala ambalo naliomba sana na mimi kwenye suala la mkonge, kama masuala haya yataendelea, siku moja nitakuja humu ndani na hoja binafsi, kwa sababu nimechoka kulizungumzia suala hili kila mwaka tunalizungumzia, watu hawawezi kuzalisha, wanaachiwa mashamba. Kama hawawezi watuachie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1974 Mkoa wa Tanga ulikuwa wa kwanza katika kilimo cha mahindi wakati Mzee Ngombale-Mwiru, alipokuwa *Regional Commissioner* katika *big four*. Sasa kama wameshindwa tung'oe mkonge, tupande mahindi ama tupande machungwa. Waheshimiwa Wabunge, juzi walipopita Korogwe, Mombo, Muheza, wameona machungwa, tupande iwe ni *zone* ya machungwa tu na matunda kuliko kutuwekea zao ambalo hata kuliwa haliliwi na wala haliendelezwi, tumebakiwa na mapori tu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ilisikie hilo, ilione na ilifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilikuwa naomba nilizungumzie ambalo Mheshimiwa Waziri pia ameligusia ni hili linalohusiana na uwezo wa kuondoa umaskini na mikakati yake kufikia ngazi ya Kijiji. Mipango yetu kwa kweli sasa hivi inakwenda vizuri, tunaanza kuirudisha Serikali chini, sasa naomba mipango hii ifike

Kijijini, ifike kwenye *level* ya Kijiji, kwenye Kata, Mipango Kata ya Vijiji na naishukuru sana Serikali kwa kitu ambacho katika bajeti hii imefanya kuwezesha Vijiji kuwa na watu wa kudumu kufanya kazi ambao watasimamia maendeleo, hawa Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru sana kwa sababu zamani ilikuwa ni shaghalabaghala tu watu wapo pale, Mtendaji wa Kijiji analipwa na Serikali ya Kijiji, uwezo hawana, lakini hawa watu wa kuajiriwa na Wizara ya Mipango ikawapatia taaluma watu hawa, tunaweza kupata mabadiliko makubwa sana kwa sababu kila Kijiji sasa kinaweza kuwa na programu ya Kijiji, ambayo wataweka maendeleo yao ya Vijiji na miradi yao itajulikana mradi wa kwanza, wa pili, wa tatu na kuwahamasisha wananchi katika maendeleo yao. Kwa kweli mimi nalipongeza sana hili na naomba sasa mipango hii iende chini zaidi ambako ndiyo kwenye watu maskini wanaotakiwa kusaidiwa zaidi, wananchi hawa ambao wengi ni wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba, wenzetu wa mipango waone hilo. Wawe na programu maalum kabisa ya kufika Kijijini na namna gani wanaweza kuwasaidia wenzetu katika Vijiji hivi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilikuwa naomba nilizungumzie katika hotuba ya Mipango ni suala la kudhibiti Ukimwi. Tanzania tutakwisha wote kwa sababu *data* zinaonyesha hakuna kupungua, Ukimwi unazidi tu *2.2 million*, laki saba wana Ukimwi na hakuna dalili za kupungua. Hii inaonyesha kwamba mikakati yetu na utekelezaji wetu una kasoro. Ni lazima kuna kasoro, haiwezekani mambo yaendelee hivyo, wenzetu wa Uganda umepungua, kwa nini Uganda umepungua? Umepungua kwa sababu wana utaratibu ambao unajulikana. Kwa hiyo, naomba Serikali ilitazame hili na ile Kamati ifanye kazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mramba, kwa bajeti yake. Jana nimepata simu kutoka Korogwe kuna mzee mmoja baiskeli yake alikuwa ameiweka, kwa muda wa miezi sita alikuwa hajaendesa, lakini jana kaiendesa. Kwa sababu alikuwa anaogopa kipande, lakini sasa hivi mambo safi, watu wamefurahia. Kwa kweli wamesema zile kodi zote za ubabaishaji na kodi za kudhalilisha watu zimeondoka kwa hiyo mambo safi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mramba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze tena Mheshimiwa Mramba, kwa kufikiria michezo, yaani bajeti ya Serikali kufikiria michezo. Kwa hilo nampongeza. Suala la kujenga uwanja wa kisasa ni suala muhimu sana lazima tukubali kwamba mchezaji yejote *performance* itapanda kama atacheza kwenye kiwanja kizuri, kama kiwanja ni kibovu mambo yote yanakwenda. Tunaita *influencing factors of performance*, mojawapo ni kiwanja. Sasa niombe kabisa kwamba, suala la michezo mmeanza na kiwanja lakini Serikali iendelee, timu zetu za Taifa zinafungwa na zinapofungwa msifikiarie ni aibu ya mtu, ni ya nchi nzima na bajeti ya michezo ni ndogo sana. Kwa hiyo, naomba suala la michezo nalo tulipe kipaumbele kwa sababu michezo ni uchumi wa hali ya juu sana. Kwa hiyo, mimi nampongeza kwa hilo ameanza lakini pia aangalie na bajeti. Sasa hivi timu yetu inakwenda kwenye *All Africa Game* kule Abuja, inataka milioni mia tatu hakuna, michezo yote. Naomba Mheshimiwa Mramba, ufikirie hilo ili timu yetu ipate *training* na timu zinazoshiriki katika mashindano ya Kimataifa. (*Makofit*)

Lingine ambalo naomba nilichangie ni hili suala linalohusiana na kusaidia wakulima wa Mikoa ya *big four* kwenye masuala ya mbolea. Niombe tu kwamba, suala hili limeanza kwa Mikoa minne, lakini lisiishie kwenye Mikoa minne, iwe ni chachu kwamba Mikoa mingine kwenye mazao mengine siyo mahindi tu kwa sababu mazao ya chakula siyo mahindi tu, kuna maharage, mpunga, nao wapewe *subsidy* hii ili tuweze kuendelea katika nchi yetu na ndizi na masuala mengine yote. Kwa hiyo, kama limeanza Mikoa mingine, nasema ni changamoto kwa sababu hatuwezi kuanza kwa jumla jumla, lazima twende polepole ili tufike mahali ambako kunaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niunge mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia, kwa jinsi ambavyo imejitokeza. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ALLY A. KARAVINA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushuru na mimi kwa kunipa fursa hii adimu, ili niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali. Awali ya yote na mimi nitoe pongezi kwa Wabunge wote wale waliochaguliwa kwenye chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni na wale wote waliorudishwa baada ya matatizo ya kusimamishwa Ubunge wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Mawaziri wote wawili na kwa kweli nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili, kwa namna ambavyo wamekuwa wanalamika toka mwaka 2001, inaonekana sasa Serikali inasikiliza na kwa kweli vitendo vingine vinavyofanyika ni vyta kimapinduzi na ni wazi kabisa masuala mengine yaliyochukuliwa sasa hivi, kwa kweli yanaelekea kabisa kufanana na Chama chenyewe cha Mapinduzi katika sera zake na Ilani yake ya Uchaguzi. Kuondoa kodi ya maendeleo ilikuwa kero tu, kwa kweli hii sasa iko *in line* na Chama cha Mapinduzi. Kutoa *subsidy* kwa mazao tulikuwa tunamwogopa nani, Waheshimiwa Wabunge tumezungumza sana toka mwaka 2001, kwamba kilimo chetu hakiwezi kuendelea kama tunakubali kweli kilimo ni uti wa mgongo, basi lazima *subsidy* na misaada mingine itolewe na Serikali ndiyo tutaendelea. Kwa hiyo, kwa kweli hapa nawapongeza sana kinaonekana hiki ni kitendo cha kimapinduzi na nafikiri huu ni mwanzo tu huko mbele ya safari tutafika mbali zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kwa zile sehemu tatu za Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji alizozitoa. Eneo la kwanza lile, nampa pongezi kwa kweli huo uchumi unakua ndugu yangu hongera sana. Sehemu ya pili ile ya mafanikio yale yanayopatikana sasa ili yatiririke kuwanufaisha wananchi mpaka huko vijijini, hili bado ni tatizo na ndiyo swali ambalo Waheshimiwa Wabunge wote wanaulizwa wakienda kwenye Majimbo yao.

Haya maendeleo tunayosikia nchi inaendelea yako wapi (*distribution of that income*) na haya mafanikio iko wapi, mbona haionekani. Hili mimi naamini pamoja na azma nzuri iliyoelezwa hapa kwenye ukurasa wa 4, lakini nafikiri hili bado ni tatizo na lazima tulitafutie ufumbuzi kama kweli tunataka wananchi wetu wasituelewe vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile la tatu ni la kuweka mazingira mazuri kwa Watanzania ambao wanunua viwanda vile vinavyobinafishwa kwa kweli ni la

muhimu mno na isiwe kwa namba ya viwanda tu, kwamba ni kiwanda fulani na fulani iwe kwa maana ya *value* ya viwanda. Iwe kwa maana ya thamani ya viwanda ili kuhakikisha kwamba ni Watanzania hao kufuatana na Ilani yetu na mwelekeo wetu wa sera kwamba kweli wana-*control* uchumi wao na wana-*control* *destiny* ya nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi nizungumze hili jambo kwa kweli bado linakera sana. Mafanikio yote haya tunayoyaeleza hapa yamepatikana kwa kuongeza utegemezi katika bajeti yetu asilimia 45 tunategemea misaada ya kutoka nje, kwa hiyo, mafanikio yote haya yametokana kwa sababu tumeongeza utegemezi. Kama nchi, hili halikubaliki lazima tuwe na mipango kila mwaka kadri tunavyokwenda tuonyeshe kwamba, tunapunguza utegemezi. Sasa tunafanya nini? Tumejaribu kupunguza sehemu nyingi sana. Hivi maana yake misingi ya *revenue* yetu ni kilimo peke yake, hivi maana yake misingi yetu ya kuongeza *revenue* katika nchi hii ni madini peke yake, hivi hakuna namna nyingine? (*Makofî*)

Mimi nafikiri pamoja na haya mazuri yote yaliyofanyika, bado kuna ngwe nyingine tunaisahau na mimi nitaendelea kuizungumzia. Mimi naamini ni lazima sasa Serikali itoe bajeti ziwe zinakwenda kufuatana na hali ya nchi hii ilivyo tofauti na nchi nyingine. Tanzania mimi naamini bado hatujai-*define* sawa sawa. Tanzania hii ni *Maritime Nation* jamani mimi narudia tena, hebu liangalieni lile jiwe lililoko pale Singapore, wale Singapore jiwe tu lile wamefanya nini lakini kwenye lile jiwe hebu oneni Singapore ilivyo leo hii. Kwa hiyo, kwa kutumia *comperative advantage* walijonayo tu pale, sisi Tanzania hapa tunayo. *Maritime Nation* hapa sisi ndiyo tuna mpaka mkubwa na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, bidhaa zinapita zinakwenda Afrika Kusini, njia rahisi ya kwenda bandarini ni kupita Tanzania. Kuna *potential* pale tunayo kubwa sana ya ule mzigo kupita tu hapa fedha peke yake, kwani fedha ya kigeni tunayoitafuta ni ipi, si Dola hizo hizo? Jamani *potential* kule iliyoko ni karibu tani milioni saba, uwezo wa reli yetu hii ni tani milioni moja, *installed capacity* kwa mwaka. Tuna *divert* ile *traffic* yote ambayo ni yetu, inakwenda nchi nyingine na kwa sababu ni *traffic* yenye *value* fikiria inaweza kupita Afrika Kusini bila kutetereka na inabeba *component* ya ile *transit cost* yake, fikiria kwa kuchukua bei tu za *TRC* sasa hivi, ambayo imeshindwa hata siku moja haijapata ku-*satisfy demand* ya mizigo ile ya Maziwa Makuu hata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, chukua Dola 60 katika tani milioni saba toa tani milioni moja ambayo *TRC* ndiyo ina uwezo wa kubeba na haiwezi ikabeba hiyo *transit traffic* yote haijawahi baki na milioni sita kwa gharama hizo za Dola 60 wanazo-*charge* kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam, hizi Dola milioni 460 mniamwachia nani? Sasa mnafikiri hii *gap* tutafanyaje, kosa dogo tu, kwa nini hatufanyi *ranking* katika kuweka *infrastructure* zetu ambazo zitatufanya sisi tuweze kuchuma uchumi huu wa *Jiografia*? Gavana wa Benki Kuu uko wapi sikeliza haya maneno. Hizi fedha ndiyo tunatafuta, kwa kutumia uchumi wa *Jiografia* wa nchi, tunatafuta fedha tunasema hapa. Tuna *gap* ya asilimia 45 kutegemea misaada kutoka nje, hakuna uhakika na hizi fedha, tunataka fedha za uhakika. Tanzania ina *advantage*, nchi 9 huko zimefungwa katika hizo 6 hazina uwezo lazima zipitishie mizigo yake hapa, mnazilazimisha zipitishe hiyo mizigo Afrika

Kusini kwa nini? Hii mizigo inapita Afrika Kusini tu kwa sababu ina uwezo huo wa *value*.

Halafu tunalalamika hatuna *sources* nyingine za *income* maana yake nini? Mimi naomba maana yake kwenye mipango yetu huku sioni kama kuna mpangilio kweli unaoonekana tunakwenda kuvuna raslimali hii ya uchumi wa jiografia, katika mipango yetu sioni. Tunaacha hii reli iliyokaa kwa umri wa miaka 100 iweze kubeba kweli uchumi wa jiografia wa nchi hii. Kwa nini wafadhili wengi wanakataa kuwekeza kwenda Kigoma, hivi nyie hamjapata kujiuliza, jiulizeni hata siku moja. Hivi kwa nini wale Wabelgiji kila siku wanaipenda ile *tender* ya *Kigoma Port* toka ukoloni mpaka leo, hata ukiigeuza vipi wanabaki wao tu ndiyo wanaochukua hiyo *tender* ya kuendesha *Kigoma Port*, hamuelewi hii maana yake nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni wendawazimu wale Wabelgiji kweli, hivi kwa nini hakuna mipango ya makusudi, tupeleke barabara kule isaidiane na reli na tuimarishe na hiyo reli iweze kubeba zaidi ya hapo. Sasa leo hii Serikali jamani tumeomba ile reli hata *infrastructure* hiyo ambayo ni ya kwetu, fedha kidogo tu zile zimetangazwa *PSRC* anai-advice Serikali kwamba, toa hata hizo fedha kidogo za kusaidia hilo Shirika la Reli, *Central Line*. Kwani nyie *PSRC* hamjui kwamba kuna Dola milioni 60 kwa mwaka tunapoteza hizi, ndiyo *loss* yenye hii, kwa kutokuimarisha reli na kutokujenga hiyo barabara ya kwenda huko.

Mimi naiomba Serikali irudishe hizi fedha angalau za kusaidia hii *interim assistance* tu *TRC* iweze kufanya kazi yake kikamilifu izirudishe fedha hizi, siyo za kutangaza tu kwenye magazeti kirahisi rahisi kwamba, zimetoka bila *explanation* yoyote. Tusifanye mchezo tunakaa tunakazania vitu ambavyo haviwezi kuinua uchumi kwa haraka haraka, tunaacha sehemu zote ambazo zina uchumi kuweza kutuinua kwa haraka haraka. *Mtwara Corridor* kule sasa kimya. Hivi ule mradi wa kutoa umeme *Mnazi Bay* tulioelezwa hapa kwamba mwaka huu ungekuwa unafanya kazi huko wapi? Nani anazuia mradi huu, Serikali itueleze? Mradi tulioletewa Bungeni hapa, mfadhili yuko tayari ana fedha na anasema baada ya mwaka mmoja akiruhusiwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay*, gesi ile atatoa umeme umefia wapi, uko wapi tunataka maelezo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baada ya kuzungumza hayo, nizungumzie kidogo juu ya simu. *Excise duty* hii kutoka asilimia 5 mpaka asilimia 7, imenishangaza kidogo kwa sababu moja. Kwa sababu *Mobile Company* sasa hivi zina *serve* asilimia 80 ya *Telecommunications Market* hapa Tanzania. Sasa ukiangalia katika hali hii ukipandisha hiyo asilimia 5 mpaka asilimia 7 maana yake asilimia 40 kwenye *airtime* maana yake nini? Watu sasa waanze kuwa wanamong'ona, watakuwa mabubu wasizungumze. Sasa watapata wapi uwezo wa kuzungumza na hizi *mobile telephone* ambazo zilikuwa ndizo zina-expand vizuri, zina-contribute kwa hali ya juu sana katika uchumi wetu. Wana utitiri wa kodi na hata kama ni *harmonization* na *East Africa*, basi *harmonization* huwezi kuifanya kwa kitu kimoja, lazima uifanye kwa vitu vyote, kama unapandisha *excise duty*, lazima u-harmonize na *VAT* vilevile, lazima u-harmonize na kodi nydinge zote ili sambamba na hiyo, *the total sum* ya hizo kodi iwe *harmonized*

kweli na umeme uwe wa bei ndogo ili uweze ku-harmonize sawasawa, una-harmonize viyi sasa kitu kimoja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kueleza tu kodi zilizopo hapa kwenye hii simu. Fikiria wao wanachajiwa *VAT* asilimia 20, *excise duty* sasa imepanda kuwa asilimia 7, *royalty fee* iko asilimia 1 mpaka asilimia 1.5, *regional levy* wanachajiwa 0.4, *comparative tax* 22 huko, ziko *Local Municipality Tax* za ajabu kabisa kwenye *towers*. Sasa mimi nashangaa hivi kweli hii kodi sasa inakwenda kwenye zaidi ya asilimia 35 ya gharama yote ya mtu kuzungumza maana yake nini? Tuna *limit market* hii isi-expand, tuna-*limit market* hii isi-extend au tunafanya nini? Maendeleo ya Sekta ya Kisasa (*Modern Sector*), yanategemea sana *telecommunications*. Ni lazima tuangalie sana suala la hii kodi. Mimi naamini tunaweza kukaiangalia vizuri, tukai-review, tukafikiria namna gani tunaweza kupata fedha sehemu nyingine. Siamini kama hapa ni mahali pake kamili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kuhusu kilimo na kuhusu hii kodi ya maendeleo ilioondolewa, tunashukuru. Mimi nina *suggest* tu kwamba, tutapoanza kuzipelekea *Council* kwa kuzingatia historia yake ya kukusanya mapato tusije tukajikuta wale wenye vingi ndiyo tunawapelekea vingi zaidi na wale wasiokuwa nacho tunazidi kuwanyang'anya zaidi. Naomba iende kwa maana ya kwamba, wale ambao hawana kabisa hebu wapelekewe zaidi kidogo. Mimi nafikiri ile *formula* ingebidi ibadiliike kidogo, *formula* iwe kwamba, kwa wale maskini zaidi wainuliwe wanaanze kujaribu kwenda sambamba na wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adimu na ninaunga mkono hoja hizi mbili asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Naibu Spika na mimi napenda nichukue nafasi hii kwanza, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuongea. Lakini nianze kwa kutoa pongezi tu kwa Waheshimiwa Mawaziri wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa bajeti zao nzuri za mwaka huu, zinatafsirika ingawa kumekuwa na tafsiri nyingi mitaani. Lakini usiposoma vitabu vyao vizuri, ndiyo utakuwa na taabu ya kutafsiri. Bajeti zao ni nzuri sana.

Napenda pia kuwapongeza Wabunge wapya kwa ujumla wao, bila kuangalia Chama, kwa kuja Bungeni, tunawakaribisha sana. Lakini nianze kwa kusema kuwa namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuchagua tena viongozi wapya wa *TRA*, yule wa mwanzo ametia nguvu na wao hawa waliokuja nafikiri wanazona alipoishia mwenzako na bila shaka na wao sasa Bwana Kitilya na Ndugu Luoga, wataangalia yale maeneo ambayo kwa kweli tunayasema tangu siku nyingi. Lazima tukubali kazi ya Senare ilikuwa nzuri sana, hasa ya kuongeza makusanyo ya kodi mpaka tulipofikia. La muhimu ni kuendeleza ushirikiano na hawa viongozi na wale waliokuwa wanafanya kazi zao kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema bajeti ni nzuri, mimi kwangu kule ni sherehe tu kwa sababu Waziri wa Fedha, anajua amewahi kukaa kule. Wakati wa kusaka

kodi hii watu wengi walikuwa wanapata matatizo sana, wale wanaokaa karibu na Ziwa wakimwona mkusanya kodi wanakimbilia Ziwani na mitumbwi humpati mtu. Halafu wengine hawalali majumbani kwao, wanakaa porini na ilikuwa tabu sana. Kuna siku niliulizwa swali nikashindwa kulijibu, nikaambiwa aah sasa huyu mtoza kodi akija saa saba za usiku na wewe umelala utamfungulia? Ikawa ni swali gumu nikawaambia waulizeni wanaokuja kusaka kodi maana yake masuala ya kodi tunasaidiana jinsi ya kukusanya. Lakini niseme kwa ufupi kwamba, tumeondo kero kubwa sana kwa wananchi wetu. Kero ambayo tumekuwa tukipongezwa kwa namna mbalimbali huko Majimboni kwetu. Kama walivyosema wengine ni kwamba, hii isiwaondoe wananchi wetu katika kusaidia maendeleo katika vijiji vyao, bado tunawahitaji wananchi wetu waweze kusaidia maendeleo mbalimbali katika maeneo yale hasa katika ujenzi wa Taifa ambalo tunaendelea kuliboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kuna tafsiri mbalimbali katika bajeti hii, lakini kama hujasoma vitabu vyenyewe utapata matatizo kweli kweli. Labda mimi niseme tu nataka kuboresha maeneo machache ambayo kama mwenzangu alivyosema mwanzo, amemtaka bwana Balali, asikilize na mimi ningewomba asikilize eneo hili dogo Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie. Lipo eneo ambalo tumeshindwa kwa muda mrefu na tumekuwa tukiuliza hapa, eneo la *exchange rate* kupanda kila siku. Wabunge wengi wamelizungumzia na katika Kamati mbalimbali tumekuwa tukilizungumzia, Mheshimiwa Leonard Derefa na Waheshimiwa Wabunge wengine, tumediriki hata kumwuliza Gavana aliyepita, hivi mnashindwa kweli kukaa kuizua hii shilingi isiporomoke? Hata maswali hapa Bungeni yamekuwa yakiulizwa, *some times* tumemwuliza Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kuwa unashindwaje na majibu yapo anakwambia aah bwana hatuuzi nje bidhaa za kutosha. Hayo ni majibu ambayo yapo ya kinadharia .

Lakini mimi nasema kuna maeneo ambayo tunaweza kuyazuia kama wenzangu walivyosema, mojawapo ni eneo la benki, ambalo linatuchezesha sana katika *fluctuation* ya *rates*. Kuna wakati sijui ni vizuri kusema, kuna wakati hizi *banks* zetu wanakuwa na *transaction* kubwa, anavinzia apate angalau Dola 5 tu kufanya ile *transaction* ipite pale. Sasa nyie viongozi hamna habari, labda wale watu wanao-deal na *exchange rates* anaambiya inapita ile na ikishapita tayari ameshapitisha mzigo wake pale. Sasa huku matokeo yake huwezi ukajua *next day* au nyuma yake huko kulitokea nini, utakuta shilingi inakwenda inakwenda. Sasa hayo mambo nilikuwa nasema Bwana Balali angeiimarisha hii Idara na iwe katika macho yake ili amsaidie Waziri wa Fedha, kuweza kuangalia ni jinsi gani ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande *money rounding*, mambo mengi yapo, lakini mimi nasemea kwa hizi benki kama walivyosema wenzangu na wale wanaosafirisha fedha nje. Eneo lingine ni kuhusu *exports* zetu. Katika jedwali namba 3 la kitabu cha hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, linaonyesha dhahiri mapungufu yetu katika baadhi ya bidhaa tunazo-export, hasa bidhaa asilia tuna-deficit pale inaonyesha na sijui kuna mikakati gani? Sijui kabisa kama tuna mikakati ya kweli ya kuiokoa nchi yetu hii kwa bidhaa hizi ambazo zinakuwa *exported*. Utakuta kahawa imeshuka bei, hilo badiliko la mwaka 2001 na mwaka 2002, sijui la mwaka huu. Sasa

mimi ninachotaka kusema ni kwamba, bado tuna haja ya kuboresha au kuimarisha uwezo wa wananchi wetu *ku-export* bidhaa nje kwa kutumia fedha kama zipo Wizarani au Benki Kuu. Wananchi wetu wanakosa *training*, wanakosa maelekezo au kuonyeshwa jinsi gani wafanye na wengine wanajaribu kuchukua matunda au maua wanapeleka *Kilimanjaro Airport*, wakifika pale wanakuta ndege imejaa wanayakimbiza matunda yale mpaka Nairobi, wakifika Nairobi nako kule wanapewa mambo ya ajabu ajabu. Sasa hilo ni eneo mojawapo ambalo kwa nini tusiboreshe hali ya usafiri kwa ajili ya matunda yetu au *export* zetu hapa hapa nchini kama kweli tunataka kuboresha uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna tatizo lingine haya haya matunda ya Muheza, machungwa hayo, pamoja na *avocado* ya Moshi utakuta yanakuwa *repacked* Kenya, unashangaa wanaya-*sort* pale vizuri, wanaweka kwenye maboksi vizuri, kesho yake au usiku huo huo unayakuta London watu wanakula kule. Sasa mimi nashangaa kwa nini sisi hatuoni hayo. Hivi tuna Balozi kweli Kenya anaangalia hayo halafu tunasema eti uchumi wa Kenya unatuzidi, tuna *argument* nydingi za ajabu ajabu. Ukiangali nchi zote zinazotuzunguka ni maskini kweli kweli kuliko sisi kama wanavyosema wengine, lakini tunaangalia, tunaacha na wenzetu wengine wanakwenda kwenye maeneo wanakuta hayo mambo, unakwenda katika hoteli moja ya London unakunywa kahawa, bei ni zaidi ya kilo moja ya kahawa ya kwetu. Sasa mantiki yake ni nini ukirudi hapa si unasema jamani eeh tuboreshe hili zao tuliweke katika hali ya kuwauzia kama zao lililokamilika. Nilitaka nisemee hili eneo na ninaomba kupata majibu yake au mwaka kesho tuone mabadiliko kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema bajeti ni nzuri upande wa kilimo kwa Mikoa ya Kusini wamesaidiwa, lakini lazima tuangalie pia jinsi gani mkulima atasaidiwa jinsi ya kupata dizeli. Hilo ni eneo mojawapo ambalo nalo lingeangaliwa kwa sababu tukitumia jembe la mkono na ng'ombe wa maksai tu hatuwezi kufika mahali popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni eneo la samaki. Eneo la samaki kwa bahati nzuri limeelezwa katika bajeti vizuri, lakini nina hoja ya *deep sea*. Hivi samaki wanakuja kuvuliwa hapa nchini na watu tuna meli tunaziona meli kubwa kubwa zinachukua *prawns* nani anaangalia na kweli huyu Mama Meghji, ndiyo kwenye bajeti yake atatuonyesha ile *figure* kamili ya mapato ya kule? Lakini eneo hili nalo lingeangaliwa tuweze kujua mikakati yake na tuweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zao mbadala mimi nilivyoolewa ni kwamba, karibu kila eneo lina hali ya hewa inayokubaliana na zao, inaweza ikawa Wilaya moja au Jimbo moja lakini maeneo tofauti kama kwangu kule mimi nina eneo ninalima kahawa, kuna eneo nalima tumbaku, kuna eneo nilikuwa nalima pamba, eneo la Ngwala nalima kahawa, eneo lingine hili la Gua, Kapalala na Kininga nalima tumbaku na maeneo haya ya Kata ya Galula, Kanga, Mkwajuni na maeneo mengine nilikuwa nalima pamba. Tuliambiwa tungepewa majibu au Wabunge wangepewa nafasi ya kusafiri kwenda kuangalia wenzetu wanafanya nini juu ya zao hili. Nafikiri ahadi ya Serikali ipo na

mwenye dhamana huyo aliyetwambia, atatupa majibu yake kwa sababu bado tunahitaji kulima pamba katika maeneo yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa kuwa Waziri ndiye mwenye dhamana ya *PPF*, ningewomba kama walivyofanya pale Dar es Salaam, ajenge mabweni ya wanafunzi pale Mzumbe, ni tatizo ambalo lipo na vilevile matatizo ya kompyuta, vitabu vyta *Library* na mengineyo kama walivyosema wengine, nayo yanatuathiri. Lakini hili pengine nitapata majibu kwa Waziri mwenye dhamana, lakini kama naye hajaweka basi tunaomba ile akiba ambayo imesalia itusaidie katika eneo hilo. Kuhusu malipo ya *PPF* ile sheria ingeangaliwa vizuri zaidi kwa sababu kuna watu wanakufa wanaziacha zile fedha, tumeweka sheria moja kwa kutokuangalia miaka, miaka ni mingi sana. Ingawa ukiangalia duniani kote ndivyo inavyofanyika, lakini tungeangalia pia inakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono bajeti hii. Nashukuru sana. (*Makofit*)

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji wa mwisho kwa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuchangia hoja hizi mbili za Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji. Bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge ambao wamechaguliwa katika chaguzi ndogo nawatakia kila la kheri, karibuni muungane pamoja na sisi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hizi mbili kwa asilimia mia moja. Niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Katibu wake Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Basil Mramba na Manaibu Mawaziri wake wote wawili na Makatibu Wakuu na wasaidizi wao wote. (*Makofit*)

Vilevile niwapongeze wafanyakazi wa *TRA*, wale ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais, ninaamini kabisa ni utendaji wao mzuri wa kazi ndiyo uliopelekea kupata nafasi hizo, Ndugu Kitilya kwa nafasi ya Kamishna Mkuu, Ndugu Luoga kuwa Kamishna Mkuu Msaidizi, naamini wataongeza jitihada kubwa za kuboresha mapato katika Mamlaka ya *TRA*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana bajeti hii, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hii ni bajeti ya tatu tangu nimejiunga na Bunge hili, bajeti hii imeweza kutoa *record* kubwa, wananchi wote wa maeneo yote ya Tanzania wameifurahia, wanaandamana na kutoa pongezi kubwa kwa Mawaziri wote waliotoa hotuba zao zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawishika kuchangia katika hoja hizi kwa furaha kubwa kwa mambo muhimu kama saba ambayo yamenigusa ndani ya bajeti hii. Nikianzia hasa kwenye upande wa kodi ya maendeleo. Wengi ambao mmesoma gazeti la Jumapili la Taifa Letu, wapiga kura wangu wa Wilaya ya Mbarali walikuwa wa kwanza

kukesha kusherehekeea kuondolewa kwa kodi hii ya maendeleo. Walikuwa na sababu za msingi kabisa za kusherehekeea kuondokana na kodi hii ya maendeleo. Kwa mwaka huu imekuwa ni ukame mkubwa kwa hiyo asilimia 80 ya wananchi wa Mbarali wana tatizo kubwa la chakula na hawana kipato kingine. Lakini la pili, kwa kutokulipa kodi ya maendeleo wakawa wanaogopa janga la kushikwa na kuingia mahabusu na kwa kuingia mahabusu wakawa wanahofia majanga ambayo waliyapata wenzao. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote, mnafahamu matatizo yaliyowapata mwaka 2002. Hasa wakihofia kwamba tatizo hili utafika wakati wa kulipa uwezo hawana, kwa njia moja au nyingine lazima watashikwa na kuwekwa mahabusu na ndiyo maana walisherehekeea kwa furaha kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limenipelekea kuchangia katika hotuba hizi ni kwa upande wa kuongeza pensheni kutoka shilingi 10,000. Bajeti ya mwaka 2002 ilikuja shilingi 12,000/= na mpaka sasa tumefikia shilingi 20,000/=. Lakini pamoja na kupongeza nilikuwa nafikiri kwamba, kuna eneo moja ambalo limesahaulika kwa muda mrefu. Nikisema pensheni maana yake inawagusa hata wale ambaao walikuwa wanafanya kazi kwenye Mashirika ya Umma. Wakati ongezeko la shilingi 12,000/= linafanya mwaka 2002 hawa watu ambaao wanapata pensheni kupitia *PPF* hawakuguswa kwa njia moja au nyingine. Kwa bahati mbaya zaidi wakawa wameguswa na hii sheria mpya ambayo ilipitishwa na Bunge kwamba, hata hivyo viwango vya shilingi 10,000/= kama hujafikia muda wa kustaafu ziliweza kusitishwa. Lakini sababu ambazo zilipelekea wasiongezewe walisema kwamba inahitaji tathmini kubwa ifanywe ili kuweza kuongeza hiki kiwango. Lakini hawa wafanyakazi wa Mashirika ya Umma ni wengi na wao wangependa kunufaika na ongezeko hili. Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Waziri awasukume wataalam wake ama tunahitaji utaalami wa kutoka nje kuweza kufanya hii tathmini kwa haraka ili wastaafu hawa waliokuwa wanafanya kazi katika Mashirika ya Umma waweze kufaidika na ongezeko hili la pensheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine ningependa kuchangia kuhusu kufanya hizi Wilaya zetu kuwa *vote holder*. Hili mimi naomba nilipongeze sana. Nakumbuka mwaka 2002 nilikuwa ni mmojawapo ambaye nilipendekeza jambo hili na nilikuomba Mheshimiwa Waziri wakati tunapitia Bajeti ya mwaka 2002. Kwanza, kwa kweli Wakuu wa Wilaya wanapata matatizo sana na utendaji unashuka. Kwa sababu hata gari likiharibika inabidi liende mkoani *RAS* alitengeneze. Mafuta wakiishiwa inabidi waombe kwa *RAS*. Sasa kwa kuwapa uwezo wa kushika au Ma-*DAS* kuwa na *vote holder* itasaidia sana kurahisisha kazi za Ma-*DC*. Nao ukikumbuka kuna Wilaya ambazo ni pana. Umekuwa Mkuu wa Mkoo wa Mbeya kwa muda mrefu, Wilaya ya Mbarali unaifahamu ilivyo pana, sasa ukipata *DC* ambaye sio *committed* inakuwa sio rahisi kabisa kufanya kazi katika Wilaya kama hii. Nashukuru tu Mkuu wangu wa Wilaya amekuwa Mbunge kwa muda mrefu na ni mtu ambaye ni *committed*, anaweza akajitahidi wakati mwingine akatembea kwa miguu, akisubiri gari litengenezwe kwa zaidi ya wiki wakati hana usafiri. Kwa hiyo, hilo na mimi nimelifurahia sana na ninaomba nikupongeze sana ndicho kilichonifanya nione Bajeti hii kwa kweli imekuwa ni Bajeti shirkishi, imesikiliza mapendekezo ya wadau wengi na naamini kabisa wote tulipo tunasherehekeea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu kutoa ajira kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji. Pamoja na sisi tulivyopata taarifa wakati tukiwa Bungeni tukasema kwamba wataajiriwa kuanzia mwezi wa Julai. Lakini niungane na Mheshimiwa Waziri kwamba, utaratibu mzima utakamilika Januari waanze kulipwa mishahara. Naelewa matatizo Hatuwezi kuanza mwezi Julai, tunahitaji maandalizi mengi. Vijiji vingi vilikuwa bado havina Maafisa Watendaji, vingine vilikuwa havijasajiliwa, kwa hiyo kwa muda huu utatufunga tuweze kuwa na utaratibu mzuri na kupata Maafisa Watendaji wa Vijiji ili mwezi Januari tuanze rasmi kuwa na Maafisa Watendaji wa Vijiji ambao wanalipwa mishahara na kero nyingi zitapungua. (*Makofii*)

Mwisho kilichonipelekea nichangie katika Bajeti hii ni kwamba, kwa upande mzima wa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi katika kutilia mkazo miundombinu hasa kwa upande wa barabara na mawasiliano ya simu. Tulikuwa na matatizo kwa muda mrefu sana kwa upande wa mawasiliano ya barabara. Lakini Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imeweza kuboresha kwa haraka zaidi Mikoa imeunganishwa, Wilaya zinaunganishwa na Vijiji vinaungwanishwa. Mimi kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Mbarali, walifurahi sana baada ya kusikia kwamba kuna mkataba umesainiwa wa barabara kutoka Kata ya Rujewa, Mawindi na Madibira na hatimaye kuunganika na Wilaya ya Mafinga. Kwamba katika mpango wa mkataba huu, barabara hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami na ni barabara ambayo iko vijiji. Sasa wana kila haki ya kufurahia na kusherehekeea kwamba, Serikali yao sasa inawaona na wao wako tayari kufaidi matunda ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu Waziri wa Kilimo atakumbuka kuna mradi kule Madibira wa umwagiliaji wa kilimo cha mpunga. Mwaka 2002 tumekuwa na malundikano ya magunia ya mpunga, tumekosa soko kwa sababu hakuna njia ya kupita kwenda kuchukua mazao haya na kuuza nje. Kwa hiyo, mpaka sasa bado tumekuwa tukihangaika ni vipi magari yataingia kuja kuchukua mazao haya. Lakini kwa jitihada ambazo zinaonekana ninaamini kabisa tatizo litaondoka na wananchi wetu wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu wamekuwa wakichangia kuzungumzia ni vipi uchumi wa nchi umekuwa haukui. Lakini naomba niwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba, kukua kwa kipato kunategemea na nchi, ni nini vyanzo vya mapato yetu, ni nini kinachangia zaidi kwenye uchumi na ndio Serikali yetu imeanza utekelezaji wake, wametathmini na kuona asilimia hamsini ya Pato la Taifa linachangiwa na kilimo. Sasa nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri Kigoda kwa mpango wao mzuri wa kuamua kutufanya sisi mikoa minne tuchague mazao hayo mawili, moja la biashara na moja la chakula ili tuweze kuzalisha kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, naomba mikoa hii ya Kusini ni watendaji wa kazi wazuri na sisi tunahakikisha kwamba hiyo *subsidy* tunayopata itakuwa ni faida kwa taifa zima la kwetu na kuboresha uchumi mzima wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo ambalo ningependa kuchangia ni kwa upande wa mashamba hasa Wilaya ya Mbarali. Ardhi ya kulima ni ndogo, ardhi yetu

imegawanywa katika makundi matatu. Kuna upande wa ufugaji na upande wa hifadhi lakini kwenye sehemu ya kulima shamba sehemu kubwa ya ardhi ilikuwa imechukuliwa na mashamba ya *NAFCO*. Bajeti iliyopita ya mwaka 2002 tuliambiwa kwamba, shamba litabinafsishwa na ndiyo ardhi ambayo wananchi wanaitegemea. Bajeti hii nategemea Waziri wa Kilimo atasema. Lakini kwa Bajeti ya mwaka 2002 Waziri alisema mashamba haya yatabinafsishwa na *PSRC* walikuwa wanashughulikia kubinafsishwa shamba hilo kwa maana ya kugawa sehemu ndogo ndogo, kubinafsishwa kwa watu binafsi. Sasa wananchi wamekuwa bado wakiyumba wakihangaika hawajui ni nini ambacho kitafanywa. Lakini na wao wanataka wafaidi hiki ambacho Serikali itakitoa kwa maana hiyo ruzuku ya pembejeo na mchango wa kuchagua mazao gani walime. Sasa bila ya *PSRC* kuharakisha ugawaji wa hili shamba au kutoa kauli ya mwisho kwamba ni lini watagawa katika hizi sehemu ndogo ili wakulima waweze kunufaika. Kwa sababu msimu wa Wilaya ya Mbarali unaanza mwezi wa Oktoba, sasa ningemwomba Waziri kama ugawaji huu utakuwa chini ya dhamana ya *PSRC*, wajitahidi kwa kila hali baada ya Bajeti hii kupitishwa kuhakikisha kwamba, shamba hili linagawanywa na wakulima wanapata ili waweze kulima zao lao muhimu ambalo ni zao moja tu la mpunga na ni zao la chakula na ndio wanategemea kama ni zao la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa zao la biashara ni tatizo kwa Wilaya ya Mbarali, Mheshimiwa Mramba, anafahamu alikuwa Mkuu wa Mkoa, sahamani nam-*quote* tena tulikuwa tunazalisha pamba. Lakini kwa bahati mbaya ule mwaka ambao tulikuwa tunahamasishwa tuzalishe pamba ikatokea tatizo kwamba pamba haiwezi kulimwa tena na aliweza kuitangaza hii akiwa Wilaya ya Mbarali, sasa itakuwa bado kwetu ni tatizo ni zao gani la biashara tulime. Kwa hiyo, naomba kama inawezekana, kama alivyopendekeza kwamba kuna uwezekano mkubwa kabisa wa zao hili lilimwe tutashukuru Mungu, lakini kama haiwezekani basi tunaomba utafiti ufanywe haraka wa kujua ni zao gani la biashara litalimwa Wilayani Mbarali ili na sisi tuweze kunufaika kati ya hii mikoa minne yote ambayo imechaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi niipongeze sana Bajeti hii na nilikuwa na kila sababu ya kuipongeza kwa sababu imetushirikisha sisi wote, wadau, wananchi wetu na tutaondokana na umaskini na ninaamini kukua kwa uchumi, mtu mmoja mmoja atawenza kubadilika kwa sababu ameamua kupeleka maendeleo Vijiji wale *individuals* watabadilika kwa sababu tumekuwa tukizungumza tu kwamba uchumi unakua lakini hatuangalii huyu mtu mmoja mmoja ni vipi anabadilika kimaisha ya kila siku ni vipi anaongeza kipato chake. Naomba nikushukuru sana ahsante sana. (*Makofi*)

(*Saa 01.40 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 19 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi*)